# KUTATHMINI USAWIRI WA MWANAMKE KATIKA RIWAYA YA MFADHILI

**HEMED SAID MASOUD**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A KIWAHILI FASIHI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2018**

**UTHIBITISHO**

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kuwa, ameisoma tasnifu hii yanye mada: **Kutathmini Usawiri wa Mwanamke katika riwaya ya Mfadhili** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya kupatiwa Shahada ya Uzamili ya Sayansi ya Jamii katika Kiswahili (Fasihi) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

**………………………………**

**Dkt. Mohamed Omary Maguo**

**(Msimamizi)**

**………………………**

**Tarehe**

## HAKIMILIKI

Tasnifu hii ni mali yangu binafsi, hairuhusiwi kuihifadhi, kuibadili na kuiga kwa namna yoyote, kielektroniki, kirudufu nakala, kwa kupigwa chapa, kuirikodi kwa utaratibu wowote  ila kwa ruhusa ya mwandishi wake au ruhusa ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

## IKIRARI

Mimi, **Hemed Said Masoud**, nathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na halisi na kwamba haijawahi kuwasilishwa, katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada ya uzamili au shahada nyengine yoyote.

……………………………

Sahihi

…………………………..

Tarehe

# TABARUKU

Kwa heshima na udhati wa moyo wangu, natabaruku tasnifu hii kwa marehemu wazazi wangu wapenzi: Mama yangu kipenzi marehemu Bimkubwa Jaffar Khamis na marehemu baba yangu bwana Said Masoud Said, kwa juhudi zao za kunizaa, kunilea, na kunisomesha bila ya kuchoka hadi kufikia hapa nilipo. Pia naitunuku kazi hii kwa marehemu kaka yangu Masoud Said Masoud aliyenihamasisha kusoma katika fani hii ya Uzamili. Nawaombea dua kwa Mwenyezi Mungu (S.W) awasamehe makosa yao na awajalie wawe miongoni mwa waja wema wa Peponi kwa Rehema na mapenzi yake Allah (S.W) Amin.

## SHUKURANI

Kabla ya yote kwanza sinabudi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu (Subhanahu Wataalah) kwa kunijaalia uzima na afya, uvumilivu, uwezo, busara na hekima kwa kuweza kufanya kazi hii ya utafiti kwa uangalifu sana hadi kuimalizia. Natoa tamko kwa kusema, Alhamdulilah Rabil alamiin, Mwenyezi Mungu atupe taufiki na kheri katika kufanikisha kazi hii.

Pili, shukurani za dhati na za pekee ziwafikie marehemu wazazi wangu wapenzi mama Bimkubwa Jaffar Khamis na baba yangu mpenzi bwana Said Masoud Said kwa juhudi zao za kunizaa, kunilea na kunisomesha bila ya kuchoka na kuvumilia shida zote ambazo nilikuwa nikiwafanyia. Nawashukuru kwa kuendelea kunijali hadi kupata mafanikio haya makubwa. Namuomba Mwenyezi Mungu (S.W) awasamehe makosa yao na wawe ni miongoni mwa waja wake wema wenye kupata uradhi wake na waingie peponi kwa rehema zake Allah (S.W) Amiin.

Tatu, shukrani zangu zisizo na kifani zimfikie msimamizi wangu Dkt. Mohamed Omary Maguo ambae amekuwa msaada mkubwa sana kwangu na kiongozi mahiri katika tasnifu hii. Daktari Mohamed Omary Maguo licha ya kuwa ni mwalimu wangu katika masomo ya Utafiti na Riwaya, pia amekuwa akinilea na kuniongoza kinadharia na kitaaluma hadi kufikia kiwango kizuri. Hatua hii ya kitaaluma hapo awali sikuwa nayo. Amekuwa akinisimamia bila kuchoka na kunitia

hamasa ili niweze kumaliza kazi yangu hii kwa wakati muwafaka. Sinabudi kumuombea malipo mema kutoka Mwenyezi Mungu (S.W) Amin.

Shukrani zangu nyengine naomba ziufikie uongozi wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania (OUT) kuanzia makao makuu Dar es Salaam hadi tawi la Pemba. Pia napenda nitowe shukurani kwa walimu wangu Profesa Emmanuel Mbogo, Profesa Tigiti S.M.Y. Sengo, Dkt. Hilda Pembe, Dkt. Zelda Elisifa na Dkt. Hadija Jilala. Shukurani maalum napenda zimfikie mwanzilishi ambae pia ni mlezi na mshauri, kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu Huria kwa hapa Pemba Mw. Bakari Kombo Bakari. Allah (S.W) ampe lenye kheri na ampe uradhi wake Amin.

Mwisho na kwa umuhimu mkubwa napenda kutoa shukurani zangu kwa muongozaji wangu kipenzi ambae amekuwa msaada mkubwa kwangu siku zote bila kuchoka Mw. Sharif Juma Fakih. Namshukuru, kwa kuniongoza katika tasnifu hii. Pia napenda kuwashukuru wake zangu wapenzi Bi Fatma Juma Salim, Bi Zaina Omar Othman, Bi Ziada Ali Hamad, na Bi Khadija Rashid Masoud pamoja na watoto wangu wote kwa uvumilivu waliouonesha. Sitoacha kuwashukuru wanafunzi wenzangu wote wa M.A. Kiswahili fasihi Pemba kwa mashirikiano makubwa tuliyokuwa nayo katika kipindi chote cha kusoma. Shukurani za pekee ziende kwa viongozi wenzangu wa Idara ya Mafunzo ya Ualimu hususan Mratibu wangu bwana Mkubwa Ahmed Omar aliyenivumilia na kunipunguzia majukumu katika kipindi chote cha masomo yangu. Kwa ujumla nawashukuru wote waliochangia kwa nanma moja au nyengine, niliowataja na nisiowataja nawaombea kwa Allah (S.W) awalipe kheri za duniani na akhera. Amin.

## IKISIRI

Utafiti huu unahusu, Kutathmini usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Mfadhili*. Kwa nia ya kufanikisha lengo kuu la utafiti huu ambalo ni Kutathmini usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Mfadhili*, utafiti uliambatanishwa na malengo mahususi mawili yafuatatyo: Mosi, Kubainisha taswira mbalimbali za mwanamke alivyochorwa katika riwaya ya *Mfadhili*. Pili, Kuelezea sababu zinazomfanya mwanamke huyo asawiriwe hivyo alivyosawiriwa katika riwaya teule ya *Mfadhili*. Utafiti huu umetumia mbinu ya maktabani kupitia usomaji makini na upitiaji wa nyaraka. Sambamba na hayo mkabala wa uchambuzi wa data uliotumika ni wa Kimaelezo kwa kiwango kikubwa na mkabala wa kitakwimu kwa kiwango kidogo. Katika kufikia malengo ya utafiti huu, mtafiti alitumia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kwa lengo la kumsawiri mwanamke kwa undani zaidi na kuweza kuelewa ni kwa jinsi gani msanii au mwandishi alivyotumia ufundi wake kumchora mwanamke katika hali chanya na hasi. Mtafiti ameweza kuyaona hayo kwa kupitia riwaya hiyo teule ya *Mfadhili*. Miongoni mwa usawiri huo mtafiti ameona mwanamke amesawiriwa kwa tabia / matendo chanya (mema) kama kiongozi bora, mshauri mwema, msamehevu, mwenye huruma, msuluhishaji, mwenye mapenzi ya dhati nk. Pia utafiti huu umebaini tabia hasi (mbaya) kwa mwanamke kama vile, ulevi, usaliti, kukosa msimamo, mwenye uchu wa madaraka nk. Pamoja na hayo mtafiti amebaini sababu za mwanamke kusawiriwa hivyo ni pamoja na kutekeza wajibu wake kazini, kujenga upendo na huruma. Bila shaka mtafiti hapa amekusudia kusema kwamba tabia nzuri ndizo za kufuatwa na tabia mbaya ndio za kuachwa na hiyo ndio siri ya mafanikio.

## YALIYOMO

**UTHIBITISHO** ii

**HAKIMILIKI** iii

**IKIRARI** iv

**TABARUKU** v

**SHUKURANI** vi

**IKISIRI** viii

**ORODHA YA MAJADWELI** xiv

**ORODHA YA VIFUPISHO** xv

**SURA YA KWANZA** 1

**1.0 UTANGULIZI WA JUMLA** 1

1.1. Utangulizi 1

1.2. Usuli wa Mada 1

1.3. Tatizo la Utafiti 7

1.4. Malengo ya Utafiti 8

1.4.1 Lengo Kuu 8

1.4.2 Malengo Mahsusi 8

1.5. Maswali ya Utafiti 8

1.6. Umuhimu wa Utafiti 9

1.7. Mipaka ya Utafiti 9

1.8. Mpangilio wa Tasnifu 10

**SURA YA PILI** 12

**2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALAWA KINADHARIA** 12

2.1 Utangulizi ..... 12
2.2 Ufafanuzi wa Istilahi Mbalimbali ..... 12
2.2.1 Dhana ya Riwaya ..... 12
2.2.2 Dhana ya Usawiri ..... 14
2.2.3 Dhana ya Wahusika ..... 15
2.3 Uainishaji wa Wahusika ..... 17
2.3.1 Wahusika Wakuu ..... 17
2.3.2 Wahusika Wadogo ..... 17
2.4 Mapitio ya Kazi Tangulizi ..... 18
2.4.1 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Mwanamke ..... 19
2.4.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Mwandishi Hussein Issa Tuwa ..... 26
2.5 Pengo la Maarifa ..... 28
2.6 Mkabala wa Kinadharia ..... 28
2.6.1 Nadharia ya Ufeministi ..... 30
2.7 Hitimisho ..... 41
**SURA YA TATU** ..... 42
**3.0 MBINU ZA UTAFITI** ..... 42
3.1 Utangulizi ..... 42
3.2 Eneo la Utafiti ..... 42
3.2.1 Sababu za Uteuzi wa Eneo la Utafiti ..... 43
3.3 Kundi Lengwa ..... 44
3.4 Sampuli na Usampulishaji ..... 45
3.4.1 Sampuli Lengwa ..... 46
3.5 Ukusanyaji wa Data ..... 46

3.5.1 Data za Awali (Msingi) ........ 47
3.5.2 Data za Upili (Fuatizi) ........ 47
3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data ........ 48
3.6.1 Mbinu ya Maktabani ........ 48
3.6.2 Usomaji Makini ........ 48
3.7 Mbinu za Uchambuzi wa Data ........ 49
3.7.1 Mkabala wa Kimaelezo ........ 49
3.8 Usahihi wa Data za Utafiti ........ 50
3.9 Hitimisho ........ 51
**SURA YA NNE** ........ 52
**4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI** ........ 52
4.1 Utangulizi ........ 52
4.2 Usuli wa Mwandishi: Hussein Issa Tuwa ........ 52
4.3 Muhutasari wa Riwaya ya Mfadhili ........ 53
4.4 Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya ya Mfadhili ........ 55
4.4.1 Mwanamke kama Mshauri Mwema ........ 56
4.4.2 Mwanamke kama Muhusika Muwajibikaji Kazini (Bidii katika Kazi) .. 58
4.4.3 Mwanamke kama Muhusika mwenye Mapenzi ya Dhati ........ 60
4.4.4 Mwanamke kama Chombo cha Starehe kwa Mwanamme ........ 62
4.4.5 Mwanamke kama Muhusika Mlevi ........ 65
4.4.6 Mwanamke kama Mtu mwenye Busara na Hekima ........ 66
4.4.7 Mwanamke kama Msaliti ........ 67
4.4.8 Mwanamke kama Kiongozi Bora ........ 69
4.4.9 Mwanamke kama Rafiki wa kweli na Mwenye kutimiza Ahadi ........ 71

4.4.10 Mwanamke kama Mtu Msuluhishi ........................................................ 73

4.4.11 Mwanamke Kama Mtu asiyetaka Ushauri ............................................... 75

4.4.12 Mwanamke kama Mtu mwenye Huruma na Imani ................................. 76

4.4.13 Mwanamke kama Mroho wa Madaraka .................................................. 78

4.4.14 Mwanamke kama Mtu aliyedhalilishwa................................................... 79

4.4.15 Mwanamke kama Mtu mwenye Kusababisha Mgogoro ............................ 81

4.4.16 Mwanamke kama Mtu asiyekata Tamaa .................................................. 82

4.4.17 Mwanamke kama Mtu aliyekwepa Majukumu na asiye na Maadili ya Kazi ........................................................................................................................ 84

4.4.18 Mwanamke kama Mtu aliyekata Tamaa ya Uhai ..................................... 85

4.4.19 Mwanamke kama Mtu Mwenye Msimamo ............................................. 87

4.4.20 Mwanamke kama Mtu Msomi (Mwenye Elimu ) ..................................... 89

4.4.21 Mwanamke kama Mtu Msamehevu ......................................................... 90

4.5 Sababu za Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya Teule ya Mfadhili........... 92

4.5.1 Kuimarisha Uhusiano Mwema Baina ya Watu ........................................... 93

4.5.2 Kutekeleza Wajibu kama Mfanyakazi ....................................................... 94

4.5.3 Kujenga Imani, Uhusiano wa Kweli usio na Shaka ................................. 94

4.5.4 Sababu ya Tamaa, Matamanio, na Kujridhisha Kimwili .............................. 96

4.5.5 Sababu ya Kuondoa Mawazo Potofu ......................................................... 97

4.5.6 Kujenga Upendo wa Dhati na Huruma ...................................................... 98

4.5.7 Sababu ya kujenga Imani na Demokrasia, Mashirikiano, na Uhusiano Mwema ......................................................................................................... 100

4.5.8 Sababu ya Ujeuri, Chuki Binafsi na Kujionyesha ................................... 102

4.5.9 Sababu ya Kukosa Maamuzi ya Busara, Hekima na Ustahamilivu ........... 103

4.5.10 Sababu ya Kushikilia Msimamo alionao Mwanamke ................................ 104
4.5.11 Sababu ya Kukosa Mfadhili wa Ini ................................ 105
4.5.12 Sababu ya kupata Maendeleo ya Kielimu, Kijamii, Kiuchumi na Kifikra... 106
4.5.13 Sababu ya Kujutia Makosa aliyoyafanya ................................ 107
**SURA YA TANO** ................................ 110
**5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** ................................ 110
5.1 Utangulizi ................................ 110
5.2 Muhtasari ................................ 110
5.2.1 Lengo Mahsusi la Kwanza ................................ 112
5.2.2 Lengo Mahsusi la Pili ................................ 113
5.3 Hitimisho ................................ 113
5.4 Mapendekezo ................................ 114
5.4.1 Mapendekezo ya Kitaaluma ................................ 114
5.4.2 Mapendekezo kwa Serikali ................................ 115
5.4.3 Mapendekezo kwa Jamii ................................ 115
5.4.4 Mapendekezo kwa Watafiti wengine ................................ 116
**MAREJELEO** ................................ 118

## ORODHA YA MAJADWELI

Jadweli 4.1: Muhtasari wa Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya ya Mfadhili ........................................................................................ 92

Jadweli 4.2: Muhtasari wa Sababu za Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya teule ya Mfadhili ........................................................................ 109

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| BAKIZA | Baraza la Kiswahili Zanzibar. |
| JUUJIA | Jumuiya ya Usawa wa Jinsia Afrika |
| Mh. | Mheshimiwa |
| N.K | Na kadhalika/ mifano mengineyo |
| NGO’s | Non Gorvenment Organisation |
| OUT | Open University of Tanzania |
| SUZA | State University of Zanzibar |
| T.Y | Tafsiri Yangu |
| TAMWA | Tanzania Media Women Association |
| TAWLA | Tanzania Women Lawyers Association |
| TGNP | Tanzania Gender Network Programme |
| TUKI | Taasisi ya Ukuzaji Kiswahili |
| U.N | United Nation |
| ZAFELA | Zanzibar Female Lawyers |
| ZLSC | Zanzibar Legal Service Centre |

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI WA JUMLA

### 1.1. Utangulizi

Utafiti huu unahusu mada isemayo: **Kutathmini Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya ya *Mfadhili.*** Sura hii imezingatia vipengele vifuatavyo: Usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, mpangilio wa tasnifu na hitimisho.

Lengo la utafiti ni Kutathmini kwa kina usawiri wa mwanamke kama ulivyojitokeza katika riwaya ya *Mfadhili* (2007). Utafiti huu pia unalenga kuangalia sababu za kumsawiri mwanamke huyo katika nyanja zote za kijamii, kielimu, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Kwa ujumla ufafanuzi wa vipengele tajwa umezingatiwa katika kufanikisha sura hii kama ifuatavyo:

### 1.2. Usuli wa Mada

Katika kipengele hiki kwanza tutangalia jinsi Jumuiya mbalimbali za kimataifa ulimwenguni na nchi za Jumuiya za Madola zilivyowatetea wanawake na jinsi walivyotoa misimamo yao dhidi ya ukandamizwaji wa wanawake. Pia tunakusudia kuangalia wanataaluma mbalimbali kupitia taasisi, mashirika na jumuiya zao ziwe za binafsi (NGOs) na hata zile za serikali jinsi walivyochukua jitihada za makusudi katika kufanya tafiti mbalimbali kuhusu mambo kadhaa yakiwemo jinsia, wanawake na watoto. Pia kipengele hiki kitaangalia wasomi na wanafalsafa ambao nao pia wametoa mchango mkubwa kumueleza mwanamke katika hali na

tabia tofauti. Tutaangalia pia wanafalsafa na wasomi hao walivyozifafanua juhudi za mwanamke, mafanikio na changamoto anazokabiliana nazo, utetezi na namna ya kupambana nazo. Miongoni mwa jumuiya na taasisi hizo ni pamoja na hizi zifuatazo: Umoja wa Mataifa - (United Nations of Women) (2014) katika kuhakikisha kuwa wanawake wanapatiwa fursa sawa na kuondokana na mfumo dume ambao unawakandamiza wanawake, uliandaa mkutano wake maalum uliohusu maswali ya wanawake. Mada kuu ya mkutano huu ilikuwa ni *Usawa wa Jinsia na Maendeleo Endelevu.* Katika ripoti ya mkutano huo kupitia aya ya mwisho Umoja wa Mataifa unasema:

> "….Katika kuimarisha na kutekeleza kwa vitendo sheria na hata sera, hatuna budi kuhakikisha kwamba suala la usawa linatiliwa mkazo kwa jinsia zote. Wanawake lazima wathaminiwe na washirikishwe katika nafasi mbalimbali za kijamii na hata za kiserikali ikiwa ni pamoja na kuwawezesha na kuwapatia nafasi za uongozi ili na wao waweze kujikomboa kifikra, kijamii na kiuchumi katika kukuza maendeleo yao. Tuondoe mawazo potofu juu yao na kamwe wasikandamizwe ili waweze kushiriki katika masuala muhimu ya kitaifa."

Kwa kiasi kikubwa maelezo haya yanapinga ile hali ya mwanamke kukandamizwa kutokana na ule mfumo dume ambao upo kwa sasa dhidi ya wanawake na badala yake umoja huu unawataka wanawake waamke na waendelee kutetea haki zao ipasavyo.

Tukirejelea Beijing nchini China (1995) katika mkutano mkuu wa Kimataifa kuhusu wanawake. Mkutano uliozishirikisha nchi mbalimbali duniani zikiwemo zile za bara la AfrikaMkutano huu ulikuwa na kauli mbiu ya "Pinga uonevu na aina zote za Unyanyasaji na Udhalilishaji dhidi ya wanawake". Mkutano huu

ulikuwa kitovu cha kuwatetea wanawake wote duniani na kuzaa kauli moja kwamba: sasa uonevu dhidi ya wanawake basi. Maazimio ya mkutano huo yalikuwa kumi na mbili ambayo ni kama yafuatayo:

> "Wanawake na mazingira**,** Uchumi na wanawake, Unyanyasaji dhidi ya wanawake, Elimu na Mafunzo kwa wanawake, Wanawake na migogoro ya kivita, Mamlaka kwa wanawake na utoaji wa maamuzi, Wanawake na Haki za Binaaadamu,Wanawake na Afya, Wanawake na Habari, Usichana wa kitoto, Wanawake na Umasikini,. Njia na mbinu mbalimbali za kuwainua wanawake katika sekta zote kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni, kielimu, kiujasiri amali na hata kifikra".

Maazimio hayo yaliungwa mkono na mataifa mengi sana duniani. Kila nchi wanachama Ililiweza kuona umuhimu wa maazimio hayo. Hii ilitokana na hali mbaya ambayo baadhi ya mataifa mengi yakiwemo ya Kiafrika ilikuwa nayo wakati huo. Kulikuwa na mtazamo mbaya kuhusu wanawake hasa katika masuala ya uongozi na utawala na kwamba wanawake walio wengi walikuwa hawapewi fursa kutokana na jinsi yao. Kwa upande wa Bara la Afrika, (JUUJIA) yaani Jumuiya ya Usawa wa Jinsia Afrika (2015) inayofafanua kuhusu Uwezeshwaji wa wanawake wa Afrika kwa matendo inalenga kuchunguza usawa wa kijinsia baina ya mwanamke na mwanamme kwa kuzingatia vipengele muhimu vifuatavyo:

> Mosi, Kuangalia fursa sawa katika taasisi za kijamii. Pili, Usawa wa kisheria kwa pande zote bila ya kujali jinsi, rangi, dini au kabila na kwamba kila mtu ana haki sawa mbele ya sheria. Tatu, Upatikanaji wa maendeleo na haki za binaadamu na kwamba hakuna mtu aliye juu ya sharia. Nne, Usawa katika mambo ya ajira na uchumi kwa wote.

Maelezo ya hapo juu yanaonyesha wazi jinsi harakati za kuwatetea wanawake kuondokana na mfumo uliopo sasa zimeongezeka kutoka siku hadi siku. Jumuiya nyingi za ndani na nje ya nchi zinazungumzia kuhusiana na mambo haya.

Tanzania nayo haiko nyuma katika kuunga mkono kwa dhati katika kuondoa kila aina ya ukandamizaji unaofanywa dhidi ya wanawake. Katika kuliunga mkono agizo hili taasisi mbalimbali zimeundwa ili kukemea hali hiyo. Mfano wa taasisi hizo ni pamoja na: ZLSC (2012) ZAFELA (2012) MKONO KWA MKONO (2013) TAMWA (1987), TAWLA (1989), TGNP (1993), WAMA (2006).

Jumuiya hizi zinaendesha shughuli zake kote nchini ikiwemo Unguja na Pemba na pia jumuiya hizo kwa sasa zimeanzisha taasisi ndogo ndogo ambapo zipo katika wilaya zote za Unguja na Pemba.

Kwa upande wa Zanzibar tunayo Wizara ya kazi, uwezeshaji, wazee, vijana, wanawake na watoto ambayo nayo inapiga vita dhidi ya udhalilishwaji na unyanyaswaji wa wanawake. Sambamba na hilo wizara hii inasimamia na kusaidia katika kuwatetea wanawake katika harakati na shughuli za maendeleo ya wanawake wote wa Zanzibar.

Mbali na matamko ya Umoja wa Mataifa duniani na mashirika mbalimbali ya umma ya Afrika yaliyozungumzia kuhusu nafasi ya mwanamke pia zipo tasnifu zilizoozungumzia nafasi ya mwanamke, Tasnifu hizo tunapenda kuzitaja kwa ufupi kama zifuatavyo:-

Yego, (2012) aliandika kuhusu “Kutathmini nafasi ya mwanamke jinsi ilivyotetewa katika nyimbo za taarab.” Katika tasnifu yake alimzungumzia

mwanamke kama mtu muaminifu, mpole na mkarimu, shujaa, mzalendo na mkombozi, mchapa kazi, mjasiri amali na mtafutaji rizki. n.k.

Githuci (2013) aliandika kuhusu *Ujagina wa mwanamke katika Pango*. Katika utafiti wake alishughulikia Ujagina wa mwanamke katika asasi za kijamii. Alishughulikia kwa kina kipengele cha usawiri wa mwanamke na kueleza jinsi mwanamke huyo alivyosawiriwa katika asasi hizo. Asasi alizozibainisha ni pamoja na asasi ya dini, ndoa, jamii na elimu.

Tasnifu ya Githuci na Yego (wameshatajwa) imemsaidia sana mtafiti wa kazi hii kwa kuwa kuwa asasi zilizojadiliwa na watafiti hao zinajitokeza hata katika riwaya ya *Mfadhili.* Hivyo basi tasnifu zao hizo zimekuwa ni dira na muongozo muhimu katika utafiti huu.

Caleb (2013) Katika tasnifu yake ya *Taswira ya mwanamke katika tamthiliya za Nguzo Mama na Mama Ee* aliangalia mambo ya msingi yafuatayo: **Moja:** Kubainisha jinsi changamoto zinazowakabili wanawake zinavyochangia kutokupata haki zao. **Mbili:** Majukumu na dhima alizopewa mwanamke kupitia asasi za kijamii yanavyochangia mwanamke kutokupata mafanikio katika harakati zake. **Tatu:** Kuonyesha jinsi waandishi walivyomsawiri mwanamke kama shujaa.

Caleb (ameshatajwa) katika kufanikisha malengo ya utafiti wake aliweza kumweleza mwanamke kuwa na majukumu mbalimbali kama alivyofafanua kupitia uchambuzi wa maudhui katika tamthiliya ya *Nguzo mama na Mama Ee.* Katika uchambuzi huo

alitaja nafasi mbalimbali kama ifuatavyo: Kwa mfano tamthiliya ya *Mama Ee* alifafanua, Matatizo ya unyumba, ubaguzi wa kijana wa jinsia ya kike, nafasi ya mila na desturi katika ndoa, nafasi ya dini katika mahusiano ya kinyumba, nafasi ya mahakama katika suala la ndoa na unyumba na mwisho umoja wa wanawake. Kwa upande wa *Nguzo mama* alifafanua suala la matabaka na wanawake, majukumu ya wanawake na nafasi yake katika jamii, wanawake na watoto wa kambo.

Kwa ujumla utafiti wa Caleb (ameshatajwa) umekuwa na thamani kwa mtafiti wa kazi hii kwa sababu umejitahidi kuangazia maeneo muhimu kuhusu mwanamke. Pamoja na kuwa mtafiti hachunguzi kazi za tamthiliya lakini utafiti huu umemsaidia sana katika kumsawiri mwanamke kupitia riwaya ya *Mfadhili* anayoichunguza.

Alie(2014), Katika mada yake ya *"Kutathmini nafasi ya mwanamke katika mashairi ya kiarudhi (kimapokeo)* alilinganisha na kulinganua usawiri wa mwanamke katika mashairi hayo katika maeneo mbalimbali ya nchi za Kiafrika na nchi nyengine duniani.

Katika tasnifu yake alimuangalia mwanamke alivyosawiriwa kwa mambo chanya kadhaa kama vile ulezi, uchapa kazi, ushujaa na uzalendo, pamoja na ujasiri na ukombozi n.k. Pia alitaja hali hasi na kutoa mifano kama vile chombo cha starehe, mkandamizwaji na mfumo dume, mtu asiye na mamlaka au maamuzi n.k.

Tasnifu ya Alie (ameshatajwa) imekuwa na thamani kubwa katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu tasnifu hiyo imejitahidi kufafanua tabia halisi za wanawake ambazo ziko

nzuri kwa upande mmoja na hata zile mbaya kwa upande wa pili. Pamoja na kwamba mtafiti hachunguzi utanzu wa ushairi lakini dhana inayojadiliwa kuhusu usawiri wa mwanamke ina umuhimu mkubwa katika utafiti huu tukihusisha na riwaya ya *Mfadhili.*

Kwa ujumla tunaona jinsi mtafiti alivyoweza kuhusisha mada za watafiti hao na mada yake ya usawiri wa mwanamke na kwamba zimemsaidia sana katika mada yake ya Kutathmini usawiri wa mwanamke katika riwaya teule ya *Mfadhili.*

## 1.3. Tatizo la Utafiti

Watafiti wengi wamejadili kwa kina kuhusu nafasi au usawiri wa mwanamke katika mitazamo tofauti tofauti. Wako waliomjadili mwanamke katika misingi hasi na misingi chanya pia, kutegemea na muonekano wa mwanamke huyo kuhusu ama tabia zake, changamoto zinazomkabili na kupendekeza namna ya kupambana nazo katika yale anayostahiki kuyafanya au kufanyiwa.

Mtafiti amebaini mada ya usawiri /nafasi ya mwanamke imefanyiwa utafiti na wataalamu na wanataaluma mbalimbali. Miongoni mwa wataalamu na wanataaluma hao ni pamoja na: Kituo cha Huduma za Sheria (ZLSC) 2014, Nung'o 1985, Chacha 1986, Lughano 1989, Momanyi 1998, Osoro 2003, Jilala 2000 na 2010/2011, Lyatuu 2011, Waruguru 2013, Ann 2013, Fakih 2017 na wengineo.

Kwa ujumla tunaweza kusema kuwa pamoja na mchango na msaada mkubwa kuhusu wanawake kupitia tafiti mbalimbali zilizofanywa na wataalamu hao, mtafiti

amebaini kuwa bado hakuna utafiti wowote uliofanywa kuhusu usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Mfadhili*. Kwa misingi hiyo, mtafiti amekusudia kutathmini usawiri wa mwanamke katika riwaya teule ya *Mfadhili* ili kuziba mwaya ulioachwa na watafiti wengine.

## 1.4. Malengo ya Utafiti

Malengo ya Utafiti huu yamegawanywa katika aina mbili: Lengo kuu na Malengo mahsusi.

### 1.4.1 Lengo Kuu

Kutathmini usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Mfadhili*.

### 1.4.2 Malengo Mahsusi

Utafiti huu una jumla ya malengo mahsusi mawili (2) yafuatayo:

- **i.** Kubainisha taswira mbalimbali za mwanamke alivyochorwa katika riwaya ya *Mfadhili*.
- **ii.** Kuelezea sababu zinazomfanya mwanamke huyo asawiriwe hivyo alivyosawiriwa katika riwaya teule ya *Mfadhili*.

## 1.5. Maswali ya Utafiti

Utafiti huu umeongozwa na maswali ya utafiti mawili (2) yafuatayo:

- **i.** Ni taswira zipi za mwanamke zilizobainishwa na kuchorwa katika riwaya ya *Mfadhili?*
- **ii.** Ni sababu zipi zinazomfanya mwanamke huyo asawiriwe hivyo alivyosawiriwa katika riwaya teule ya *Mfadhili?*

## 1.6. Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu una umuhimu mkubwa sana kwa mtafiti mwenyewe pia kwa watu wengine ambao watausoma kutokana na mambo muhimu yafuatayo:

**Moja;** Ni imani ya mtafiti kwamba utafiti huu umesaidia sana kudhihirisha usawiri wa mwanamke alivyochorwa na changamoto anazokabiliana nazo na jinsi ya kuzitatua katika maisha ya kila siku kwa kurejelea riwaya teule ya *Mfadhili*

**Mbili**; Utafiti huu utakuwa ni msingi imara kwa watafiti wengineo kuendeleza juhudi zakuchunguza usawiri wa mwanamke kwa kurejelea utanzu wa riwaya mbalimbali na hata tanzu nyenginezo katika Fasihi ya Kiswahili.

**Tatu;** Utafiti huu umekuwa ni nyongeza muhimu ya marejeleo ya kitaaluma na kinadharia katika ngazi mbalimbali za kielimu na fani nyenginezo stahiki kwa upande wa walimu na wanafunzi.

**Nne;** Utafiti huu umezidi kutoa mwanga na kupanua mawazo ya mtafiti kwa undani zaidi na kujiamini katika kuhaulisha uzoefu huo katika tanzu nyengine za fasihi.

## 1.7. Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umejikita katika mada isemayo**:** Kutathmini usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Mfadhili* Mtafiti anatambua vyema kuwa mwandishi wa riwaya hii Hussein Issa Tuwa ni gwiji na mashuhuri katika uandishi wa vitabu vingi hasa vya riwaya.

Kwa ujumla mwandishi Hussein Issa Tuwa amewahi kuandika vitabu kadhaa kama vile *Shangazi Kutoka Mjini* (2003), *Mfadhili* (2007), *Bondia* (2012), *Mdunguaji* (2012), *Miss Tanzania* (2013), *Utata wa 9/12* (2013), *Mkimbizi* (2015), *Mtafiti* (2015), *Mtuhumiwa* (2016) na *Wimbo wa Gaidi* (2017).

Kwa misingi hiyo, mtafiti amezingatia na kutathmini usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Mfadhili* ambayo amekusudia kujua na kutathmini maendeleo, mabadiliko, sababu, vikwazo na mapendekezo ya mtafiti kuhusu mwanamke kupitia riwaya hii. Mtafiti hakuhusika na riwaya nyengine za mwandishi huyu au riwaya za mwandishi mwengine kwa vile mada yake inahusiana na riwaya hii teule ya *Mfadhili*

Mtafiti amechagua riwaya hii kwa sababu hatachunguza na kutathmini riwaya nyenginezo au mada nyengine akiamini riwaya iliyoteuliwa itatosha kufanikisha malengo na kujibu maswali yake ya utafiti kwa kiwango kinachostahiki. Marejeleo mengine mbalimbali yakiwemo ya riwaya au mengine yoyote ya kifasihi yametumika ili kusaidia kufanikisha mada hii ya utafiti vyema.

### 1.8. Mpangilio wa Tasnifu

Utafiti huu umefuata mpangilio na umegawanywa katika sura kuu tano zifuatazo: **Sura ya kwanza**; **Utangulizi wa jumla:** Katika sura hii mtafiti ameangalia mambo muhimu yafuatayo:Utangulizi, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, mpangilio wa tasnifu na hitimisho.

**Sura ya pili; Mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia:** Katika sura hii mtafiti ameangalia mambo ya msingi yafuatayo: Utangulizi wa sura, Ufafanuzi wa Istilahi mbalimbali,Mapitio ya kazi zinazohusiana na mada inayofanyiwa utafiti, Mkabala wa Kinadharia na mwisho Hitimisho.

**Sura ya tatu; Mbinu za utafiti:** Katika sura hii tumeangalia mambo ya msingi yafuatayo: Utangulizi, Mbinu za Utafiti, Eneo la Utafiti, Usanifu wa Utafiti, Kundi lengwa, Sampuli na Usampulishaji, Aina za Data, Mbinu za Kukusanya Data, Uchambuzi wa Data, Usahihi wa Data za Utafiti, Maadili ya Utafiti na Hitimisho.

**Sura ya nne, Uwasilishaji, Uchambuzi wa data za utafiti:** Vipengele vilivyojadiliwa ni pamoja na: Utangulizi, Usuli wa mwandishi Hussein Issa Tuwa, Muhtasari wa riwaya ya *Mfadhili*, Uchambuzi wa usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Mfadhili* na sababu za usawiri wa mwanamke huyo. Mwisho ni Hitimisho.

**Sura ya tano; Muhtasari wa Utafiti, Hitimisho na Mapendekezo**: Vipengele vilivyojadiliwa ni pamoja na Muhtasari wa tasnifu (sura tano), Hitimisho la tasnifu, na Mapendekezo kitaaluma, kwa serekali, kwa watafiti wengine na jamii.

# SURA YA PILI

# 2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALAWA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sehemu hii imejikita kwa kuzungumzia juu ya mambo ya msingi yafuatayo: Ufafanuzi wa Istilahi muhimu katika mada ya utafiti, Mapitio ya kazi tangulizi, Mkabala wa kinadharia na Hitimisho. Kwa misingi hiyo sehemu hii itaimarishwa kwa kurejelea kazi mbalimbali tangulizi zenye uhusiano na mada husika ili kujenga ithibati na umakinifu wa kutimiza haja ya malengo na maswali ya utafiti huu.

## 2.2 Ufafanuzi wa Istilahi Mbalimbali

### 2.2.1 Dhana ya Riwaya

Wataalamu mbalimbali wameizungumzia dhana hii kwa miono tofauti. Maelezo yafuatayo yanaangazia baadhi ya wataalamu hao walivyoifafanua dhana hii. Muhando na Balisidya (1976) wanaeleza kuwa: Riwaya ni kazi ya kubuni, ni hadithi ambayo hutungwa kufuatana na uwezo wa fanani kuibusha mambo kutokana na mazoea au mazingira yake. Wanaendelea kusema kuwa riwaya yaweza kuanzia maneno 35000 hivi na kuendelea. Kwa mujibu wa fasili hiyo mtafiti ameona kwamba sio lazima riwaya kuwa iwe na idadi hiyo tu na sio vizuri kuweka idadi fulani ya maneno. Mtafiti anaona kwamba vile vigezo vya msingi sana viangaliwe na sio idadi ya maneno kwani riwaya zipo refu na nyengine fupi kutegemea mtunzi alivyoandika.

Senkoro (1982) anaeleza kuwa, Riwaya ni kisa ambacho ni kirefu vya kutosha chenye zaidi ya tukio moja ndani yake, ni kisa mchangamano ambacho huweza

kuchambuliwa na kupimwa kwa uzito na undani wa mambo mbalimbali. Riiwaya ni kisa ambacho urefu wake unakiruhusu kutamba mahali pengi na kuambaa vizingiti vingi kama apendavyo muandishi. Ndungo na Mwai (1991) wanaeleza kuwa, Riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni yenye mchangamano wa visa ambavyo huchambuliwa na kupimwa kwa mapana na marefu kimaudhui na kifani.

Kwa hakika mtafiti anaunga mkono tafsiri ya Senkoro, Ndungo na Mwai (wameshatajwa) kwa sababu tafsiri hizo zimezingatia vipengele vya kimsingi katika dhana muhimu ya riwaya. Vipengele hivyo muhimu ni pamoja na riwaya inahusu mchangamano wa visa na matukio, lugha yakubuni na kinathari, urefu wa kutosha, fani na maudhui iliyotimia.

Mulokozi (1996) anasema; Riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni yenye mawanda mapana, lugha ya kinathari, mchangamano wa visa na dhamira, wahusika kadhaa na matukio yaliyosukwa kimantiki, yenye kufungamana na wakati na kushabihiana na maisha halisi. Wamitila (2002) anafafanua kuwa; Riwaya ni kazi iliyoandikwa kwa mtindo wa kinathari ambayo ina urefu wa kiasi fulani, ni pana, ina uchangamano wa kimtindo na kidhamira na inashughulikia masuala kadha katika mtazamo mpana wa wakati.

Kwa mujibu wa wataalamu hao hapo juu Mulokozi na Wamitila (wameshatajwa) mtafiti anaendelea kuunga mkono maelezo ya fasili zao kuhusu dhana ya riwaya. Mtafiti anakubaliana na fasili hizi kwasababu wamegusa maeneo yote muhimu kama vile kinathari, urefu wa kutosha, wahusika wengi walioendelezwa kwa kina pamoja na dhamira.

Kwa ujumla tunaweza kusema: Riwaya ni aina ya utanzu wa fasihi andishi wa hadithi ndefu ya kubuni yenye kutumia lugha ya kinathari yenye fani na maudhui, yenye wahusika wa kutosha na yenye msuko wa matukio mbali mbali yanayogusa maisha halisi ya jamii. Kwa muhtasari, dhana hii ya riwaya imemsaidia sana mtafiti katika kazi yake kwa kuwa ndio msingi wa utanzu ambao ameushughulikia. Mtafiti kupitia mada ya utafiti tajwa amezingatia utanzu wa riwaya na sio utanzu mwengineo katika fasihi andishi ambao ni Ushairi na Tamthiliya. Jambo hili ndilo lililomsukuma kutumia riwaya ya *Mfadhili* ambapo pia imemsaidia kufanikisha dhana nzima ya kutathmini usawiri wa mwanamke kupitia riwaya hii na kufafanua mbinu za kisanaa alizotumia mwandishi Hussein Issa Tuwa ndani ya riwaya yake ya *Mfadhili.*

### 2.2.2 Dhana ya Usawiri

Msokile (1993) anafafanua: Sawiri ni fanya sura ya kitu kwa kutumia picha/kalamu au mashine za kutolea picha. Kusawiri maisha ni kuunda kazi ya sanaa inayosawiri, inayoiga maisha kwa kuzingatia misingi ya maisha ya jamii inayohusika. BAKIZA (2010) wanaeleza kuwa: Kusawiri ni kitendo cha kuchora sura ya kitu kwa kutumia vifaa kama vile kalamu, penseli au chaki. Au, sawiri ni kitendo cha kuunda sura ya mtu , kitu au jambo katika akili.

Kwa kuhitimishia tunaweza kusema kuwa: Usawiri katika kazi za fasihi ni kile kitendo cha kuwajenga, au kuwajengea dhima zao maaalum wahusika kwa mujibu wa matendo yao ambayo mwandishi amewajengea uwezo wahusika hao

kwa lengo la kufikisha ujumbe maalum kwa hadhira yake kwa yale aliyoyakusudia msanii au mwandishi katika kazi yake ya fasihi.

Wahusika hawa wanaweza kuwa binaadamu au viumbe vyengine visivyokuwa binaadamu. Wahusika huteuliwa na kubebeshwa majukumu na msanii kwa minajili ya matendo na maudhui ya kibinaadamu yanayohalisika na maisha ya jamii husika.

### 2.2.3 Dhana ya Wahusika

Katika uchambuzi/uhakiki wa kazi ya Fasihi, Fani na Maudhui ni misingi muhimu. Fani hujengwa na vipengele mbalimbali kama Muundo, Mtindo, Mandhari, Lugha na Wahusika. Wahusika ni mojawapo miongoni mwa vipengele muhimu katika kazi ya Fasihi. Wahusika ni dhana ambayo ndio msingi wa kujenga Maudhui ya msanii/ mwandishi katika kuiumba kazi yake na kwa lengo la kufikisha Maudhui/Malengo au Ujumbe kwa jamii alizozikusudia. Dhana hii ya "Wahusika" imefasiliwa na wataalamu kadhaa. Miongoni mwa wataalamu hao ni pamoja na hawa wafuatao:

Ndungo na Mwai (1991:160) wanasema kuwa, wahusika ni watu au hata viumbe viliochorwa na mwandishi kisanii ili kuwakilisha watu anaowafikiria katika kazi yake. Msokile, (1993:117) anaeleza kwamba, wahusika ni vitu, wanyama au watu katika kazi ya sanaa; mfano katika hadithi kuna wahusika wanyama, watu, mimea n.k. Njogu na Chimerah (1999) wanasema kuwa: Wahusika ni wale ambao wanatumiwa na mwandishi kubeba na kuwasilisha Maudhui katika kazi ya Fasihi, Riwaya ikiwemo. Wahusika hawa wanaweza kuwa wanaadamu, wanyama, wadudu, madubwana, majini, mashetani, mawe na vitu vyengine visivyokuwa na uhai.

Wahusika ni viumbe wanaopatikana katika hadithi yeyote ile. Viumbe hawa huwa sehemu ya kazi nzima. Pili, wahusika ni "binaadamu" wanaopatikana katika kazi ya kifasihi na ambao wana sifa za kimaadili, kitabia, kiitikadi, kifalsafa ambazo hutambulishwa na wanayoyasema (mazungumzo) na wanayoyatenda (matendo). Wahusika huweza kutambulishwa pia na maelezo ya mhusika au msimulizi. Msingi wa hisia, hali ya kimaadili, mazungumzo na matendo ya wahusika ndiyo kiini cha motisha au uhamasishaji wa wahusika (Wamitila, 2002:18).

Wamitila (2008) anaeleza kuwa, Mhusika ni mtendaji katika kazi ya kifasihi na huwa kielelezo cha viumbe wanaopatikana ulimwenguni ingawa si lazima sifa zote za mhusika zifungamane moja kwa moja na za wanaadamu. Senkoro (2011), Wahusika ni watu ama viumbe waliokusudiwa wawakilishe dhana, mawazo au tabia za watu katika kazi za Fasihi. Kwa kuhitimishia tunaweza kufasili: Wahusika kuwa ni watu (binaadamu) au viumbe vyenginevyo kama wanyama, au vitu vyengine vinavyowakilisha matendo ya kibinaadamu ambavyo msanii au mwandishi katika kazi ya Fasihi huviteua maalum kwa lengo la kuwasilisha Maudhui aliyoyakusudia kwa jamii husika. Wahusika ni kipengele muhimu katika kazi yeyote ya fasihi. Ndio rasilimali muhimu kwa msanii au mwandishi katika kuipa uhai kazi yake ya fasihi ili ionekane imelenga jamii iliyokusudiwa Kimaudhui. Msingi mmoja muhimu wa wahusika ni kupima tabia, nyenendo, hisia, uwezo, utendaji, fursa, uwajibikaji, maadili, nidhamu, malezi, pamoja na wema au/na uovu wa wahusika, matendo ambayo hutendwa na wanajamii au watu (binaadamu) katika jamii husika.

## 2.3 Uainishaji wa Wahusika

Uainishaji wa Wahusika sio jambo jepesi. Wataalamu mbalimbali wameainisha aina mbalimbali za wahusika. Baadhi ya wataalamu hao ni: Ndungo na Mwai (1991) Msokile (1993), Njogu na Chimerah (1999), Ntarangwi (2004), Wamitila (2008), Madumulla (2009) na wengineo. Wataalamu wote hao wametoa mchango mkubwa katika kuainisha aina kadhaa za wahusika. Ufafanuzi wa aina hizo ni kama ifuatavyo:

### 2.3.1 Wahusika Wakuu

Mhusika mkuu hasa ni yule anayehusishwa katika kazi nzima tangu mwanzo hadi mwisho. Ukuu wa mhusika unatambulikana kuambatana na dhima aliyopewa na msanii. Pia mhusika huyu huwa na Maudhui ya kazi ile kuliko mhusika mwengine yeyote. Hata mara nyingine mhusika mkuu hutumiwa na msanii kama kinywa chake. Yeye ndiye husema na kutenda msani anayoyapendelea yatekeleke katika jamii. Wahusika wakuu wana umuhimu mkubwa katika kazi ya Fasihi na wao huwa ndio watendaji wakuu wakufikisha maudhui ya kazi ya mwandishi. Kawaida katika kazi ya Fasihi muhusika mkuu huwa mmoja ingawaje wakati mwengine msanii anaweza kuchora jamii au kundi la watu kama wahusika wake wakuu. Wakati mwingine, baadhi ya wahakiki wamewaona wahusika hawa kuwa ni "midomo" ya wasanii.

### 2.3.2 Wahusika Wadogo

Hawa ni wahusika wanaomzingira mhusika mkuu na wanaomsukuma aamue au asiamue jambo kinyume chake wahusika hawa hujitokeza hapa na pale katika kazi ya fasihi wakiwa na lengo la kufikisha ujumbe. Wahusika wadogo pia husaidia kuijenga

dhamira fulani inayojadiliwa katika kazi ya fasihi. Hawa wanaweza kuchorwa sambamba na mhusika / wahusika wakuu ili kuisaidia hadhira kumwelewa mhusika mkuu /wakuu hao. Pia wahusika wa aina hii husaidia au kuyajenga maudhui fulani katika kazi ya fasihi. Lakini mradi tu wao wametumiwa kusaidia kuyajenga Maudhui yale wao wangali wasaidizi tu. Mtafiti amebaini kuwa amewatumia wahusika wote wa aina mbili katika utafiti huu ambao wameweza kusawiriwa kwa matendo tofauti tofauti katika riwaya yake ya *Mfadhili.*

## 2.4 Mapitio ya Kazi Tangulizi

Mapitio ya kazi tangulizi ni usomaji wa kina wa maandishi ya watafiti watangulizi, unaofanywa na mtafiti kwa ajili ya uchambuzi kuhusu suala la utafiti. Mapitio ya kazi tangulizi lazima yaonyeshe uhusiano wa maandishi hayo na mada ya utafiti. Katika mapitio ya kazi tangulizi huoneshwa pia nadharia zilizotumika katika uchambuzi wa data. Aidha, mapitio ya kazi tangulizi ni maarifa yanayopatikana kwa kuzamia mbizi maandishi ya huko nyuma ambayo hufananishwa na taarifa hai zilizopatikana ndani ya utafiti wa sasa (Enon, 1998). Buliba na wenzake (2014), wanasema kwamba sababu kuu ya kuyatalii yale yote yaliyoandikwa awali kuhusu somo la utafiti ni kuhakikisha kuwa swali lililotafitiwa awali halirudiwi tena kwa kutojua. Kwa kufanya hivyo, sehemu hii itamsaidia mtafiti kumridhisha mdhamini wake kuwa kazi yake ikikamilika itakuwa mchango mpya katika nyanja ya taaluma anayoishughulikia.

Kwa ujumla mtafiti amepitia kazi mbalimbali tangulizi ambazo zimemsaidia sana kufanikisha mada husika ya utafiti. Pamoja na kwamba mtafiti mada yake inalenga

riwaya lakini kazi mbalimbali tangulizi zimesaidia kwa kiwango cha hali ya juu zikiwemo za fasihi simulizi, riwaya mbalimbali, tamthiliya, ushairi, tasnifu, makala, na tafiti nyenginezo ambazo zimetoa msukumo mkubwa wa mada ya mtafiti ambayo ni: Kutathmini usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Mfadhili.* Kwa upeo mkubwa. Mapitio ya kazi tangulizi zilizotumika katika utafiti huu ni kama zifuatazo:

### 2.4.1 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Mwanamke

Katika sehemu hii, mtafiti amepitia kazi tangulizi mbalimbali zikiwemo tasnifu, marejeleo ya vitabu vya riwaya, tamthiliya na hata ushairi, makala na ripoti nyenginezo. Kazi tangulizi alizozipitia zaidi ni zile ambazzo zimejikita kujadili juu ya mwanamke. Lengo la kufanya hivyo ni kuweza kubaini michango, mawazo na juhudi za watafiti waliotangulia katika kumuelezea mwanamke. Mtafiti anaamini michango na mawazo hayo yamesaidia sana kufanikisha utafiti wake alioufanya. Juma (2008) amefanya utafiti kuhusu *Kiswahili cha Asili cha kinamama wa visiwani Zanzibari;* Katika utafiti wake amefanikiwa kueleza usawiri wa mwanamke unaojitokeza kama ifuatavyo: Lugha ya upole, nasaha na radhi, urembo na utanashati, malezi na mafunzo, mapenzi na mahaba, lugha ya ushawishi, majina ya kanga, sanaa na nyimbo, lugha ya mipasho n.k.

Utafiti wa Juma (keshatajwa) umetoa muelekeo mzuri wa matumizi ya lugha hususan kwa wanawake kupitia nafasi zao, uwezo na changamoto zake. Mwandishi wa mada hiyo amejitahidi sana kufafanua uwezo wa wanawake katika matumizi ya lugha kupitia nafasi zao visiwani Zanzibar. Dhana hii imemsaidia sana mtafiti kutambua

mchango wa wanawake katika kukiimarisha Kiswahili kupitia nafasi na usawiri wao katika maisha yao ya kila siku. Jambo hili halikudhihirika kwa wanawake wa Zanzibar na Tanzania tu bali Afrika na hata duniani kwa ujumla. Juhudi zao hizo zimehusishwa na mada ya mtafiti kupitia riwaya hii teule ya *Mfadhili.*

Sengo (2009) ame mchunguza mwanamke na kubaini ya kwamba mwanamke ana vyeo vinane (8) katika familia. Vyeo hivyo amevitaja kuwa ni ni mama, shemegi, mke, dada, nyanya, shangazi, mamkwe, binti. Dondoo hii imemsaidia mtafiti katika mada yake ambayo inalenga usawiri wa mwanamke. Mwanamke ameweza kukwezwa au kudunishwa kulingana na uhusiano alionao kati yake na watu wengine alionao katika jamii au familia kwa ujumla. Kipyegon (2013) katika tasnifu yake alichunguza mada isemayo: "Nafasi na Utambulisho wa Mwanamke katika *Natala* na *Kifo Kisimani"* Katika utafiti huo, mtafiti alibainisha uwepo wa pande mbili kubwa zjnazomuhusu mwanamke. Upande wa nafasi hasi (mbaya) na upande wa nafasi chanya (nzuri).

Kwa upande wa nafasi hasi, mtafiti amebainisha kwamba, Mwanamke ni kama chombo cha kumfurahisha mwanamume, Mwanamke kama mmbeya, Mwanamke kama kiumbe duni asiyestahili heshima, Mwanamke kama mtu mwenye hasira na chuki na mwanamke kama mtu anayedanganyika kwa haraka. Kwa upande wa nafasi chanya yaani nzuri na zenye kufaa; mtafiti amemchora mwanamke katika nafasi kadhaa kama vile, Mwanamke ni kama mtu mwenye bidii, Mwanamke kama mtu mwenye mapenzi ya dhati, Mwanamke kama mtu mwerevu na mwenye akili tambuzi, Mwanamke kama mzalendo, Mwanamke kama shujaa na jasiri. Pamoja

na hayo yaliyoelezwa na Kipyegon (keshatajwa) katika kazi yake, mtafiti wa kazi hii amebaini kuwa bado zipo changamoto kadhaa ambazo zimemkabili mwanamke na zinahitaji kupigwa vita. Mifano ya changamoto hizo ni pamoja na Mfumo mbaya wa kiuchumi, ukosefu wa mashirikiano, kutoshirikishwa katika maamuzi kama vile ndoa, kuendelea kubanwa na mfumo dume nk.

Dondoo ya Sengo na Kipyegon zimemsaidia na kumdhihirisha mtafiti jinsi mwanamke kama binaadamu anavyoweza kutenda matendo mbalimbali ambayo huweza kuwa mazuri (mema) na hata yakawa mabaya (maovu). Hata hivyo jambo la msingi mkubwa na la matarajio makubwa ni kutenda matendo mema na kuacha maovu. Pamoja na kwamba mtafiti hachunguzi tamthiliya lakini kupitia utafiti wa Kipyegon mtafiti ameweza kutambua dhima mbalimbali za mwanamke katika maisha ya kila siku. Mambo haya huweza kujitokeza hata katika triwaya ambako ndiko kwenye uwanja anaoogelea mtafiti wa kazi hii yaani riwaya ya *Mfadhili.*

Pauline (2013) katika tasnifu yake alichunguza mada isemayo: Uhakiki wa Kimaudhui na Kifani wa *Kidagaa Kimemwozea.* Katika riwaya hiyo, mtafiti alibaini nafasi mbalimbali za mwanamke zikiwemo hizi zifuatazo: Mwanamke kama mtu mwenye huruma, Mwanamke kama mtu mvumilivu, mwanamke ni mtu mzalendo, mwanamke kama mkombozi na mwanamke kama chombo cha starehe. Utafiti wa Pauline (ameshatajwa) umekuwa na umuhimu mkubwa kwa mtafiti wa kazi hii. Umekuwa ni wa umuhimu kwake, kwa sababu umemsaidia kutambua nafasi mbalimbali za wanawake na matendo yao katika maisha yao ya kila siku. Jambo hili

limemsaidia mtafiti kutathmini nafasi au usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Mfadhili.*

Ramadhan (2013) ameandika kuhusu: Usawiri wa Mwanamke katika Taarab ya Mipasho: Mfano kutoka nyimbo za Mzee Yussuf Mzee. Katika utafiti wake aligundua nafasi kadhaa za mwanamke kama vile: Mwana mke kuwa ni Mvumilivu na mwaminifu, mtu mwenye heshima, chombo cha starehe, mpole na mnyenyekevu, mshauri na mlezi wa familiya, mwenye msimamo, mtumishi wa mwanamume. Mwanamke kama chombo cha starehe. Maelezo ya Ramadhan (keshatajwa), yamemsaidia sana mtafiti wa kazi hii kutambua tabia za wanawake katika maisha yao ya kila siku. Pia amebaini kwamba kwa hakika baadhi ya mambo yao yanaridhisha (mema) na mengine yanakirihisha na kuchukiza (maovu). Kwa kuwa mtafiti alijikita katika nyimbo za taarabu, tabia hizo zitampa mwamko mtafiti wa kazi hii kutahmini usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Mfadhili.*

Salem (2013) alifanya utafiti wenye mada: "Usawiri wa Jinsia katika Lugha ya Mashairi: Mifano kutoka Mashairi ya Shaaban Robert*"*. Katika utafiti huo, (Salem) alibaini uwezo wa mwanamke katika kutenda matendo mbalimbali na kubeba nafasi nyingi za msing. Miongoni mwa nafasi hizo ni Mwanamke kama kiumbe muhimu katika jamii, Mwanamke katika Mapenzi, Mwanamke katika maamuzi, Mwanamke katika asasi ya ndoa, Mwanamke katika elimu, Mwanamke katika uzazi na malezi, Mwanamke katika utamduni, mwanamke katika dini.

Kwa haki, dondoo hii ina umuhimu mkubwa kwa mtafiti. Pamoja na kwamba mtafiti alitafiti upande wa utanzu wa Ushairi lakini tasnifu hiyo imekuwa ni msaada

mkubwa kwa mtafiti kuweza kuona mwanamke na juhudi zake katika msingi wa kujiimarisha katika sekta mbalimbali zikiwemo za Kisiasa, kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni. Hivyo basi utafiti wa Salem(keshatajwa) umeleta tija kubwa kwa upande wa mtafiti wa kazi hii kwa kuweza kulinganisha matokeo ya Salem (keshatajwa) na mada yake ya utafiti katika wa riwaya ya *Mfadhili*.

Ali (2014) alifanyia utafiti mada iliyohusu: *"Kutathmini Nafasi na Mwanamke katika Mashairi ya Mnyampala" Kiswahili: Uchunguzi na Mashairi ya Shaaban Robert na Mathias*. katika utafiti wake alibaini kwamba mwanamke anajitokeza katika sura kadhaa zikiwemo, Mwanamke kama Chombo cha starehe, Mwanamke ni Mpole, Mnyenyekevu kwa Mwanaume, Mama na Malezi katika jamii, Mwanamke na suala la Uaminifu, Suala la Uasherati na Umalaya katika jamii.

Matokeo ya utafiti wa Ali (keshatajwa) yamemsaidia sana mtafiti kuibua dhana nzima ya uwepo wa pande mbili kuhusu wanawake katika maisha ya kila siku yaani matendo mema (chanya) na matendo maovu (hasi). Ingawa hii ni hali ya kawaida kwa wanadamu lakini imemfanya mtafiti kuzidi kutathmini usawiri wa mwanamke katika riwaya teule ya *Mfadhili* kwa lengo la kubaini vipi mwandishi amemsawiri mwanamke katika riwaya hiyo.

Mapunjo (2014) alifanya utafiti kuhusu mada ya"Usawiri wa Mwanamke kama Kiongozi katika Tamthiliya: Uchunguzi wa *Kivuli Kinaishi na Nguzo Mama"* Katika utafiti huo, Manjo (keshatajwa) kwa ujumla alibaini nafasi kadhaa za muhusika mwanamke katika tamthiliya hizo. Katika tamthiliya ya *Nguzo Mama* kwa mfano

alibaini nafasi kadha zinazomuhusu mwanamke. Miongoni mwa nafasi hizo ni Mwanamke Kama Kiongozi Mwenye Maamuzi, Mwanamke Kama Mfuata Sheria, Mwanamke Kama Kiongozi wa Familia, Mwanamke Kama Mtetezi wa Wanawake na Mwanamke Kama Kiongozi Mwenye Bidii. Katika tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* mtafiti alibainisha nafsi za mwanamke ambazo ni: Mwanamke kama Kiongozi Anayependa Elimu, Mwanamke kama Kiongozi mwenye Maamuzi ya Mwisho, Mwanamke Kama Kiongozi Mwenye Huruma kwa Wenzake na Mwanamke kama Kiongozi Mwenye Ndoto ya Kuona Mbali.

Kwa kweli utafiti kuhusu tamthiliya hizi mbili una umuhimu mkubwa kwa mtafiti wa kazi hii kwa sababu imekuwa kama tochi ing'arayo katika uhalisia wake. Katika utafiti huu, mtafiti ameibua uwezo mkubwa wa mwanamke hususan katika upande wa uongozi ingawaje mwanamke huyo bado anakabiliwa na changamoto kadhaa kama zilivyotambulishwa na kuchambuliwa na mtafiti katika mada yake inayohusu tamthiliya zake za *Kivuli Kinaishi na Nguzo Mama* na mwishowe kutoa mapendekezo na njia ya kupambana na changamoto hizo. Kwa upande wa utafiti huu, mtafiti amethmini mchango wa wanawake hao ambapo anaamini kwamba mchango umesaidia kwa kikubwa katika kutathmini usawiri wa mwanamke katika riwaya teule ya *Mfadhili.*

Mtafiti kupitia dondoo hizo mbili zilizotangulia zimemsaidia na zimedhihirisha jinsi mwanamke kama binaadamu huweza kutenda matendo mbalimbali ambayo huweza kuwa mazuri (mema) na hata yale mabaya (maovu) lakini msingi mkubwa ni kutenda matendo mema na kuacha maovu.

Fakih, (2017) katika tasnifu yake “Kutathmini mabadiliko ya usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Utengano* na *Kamwe si mbali tena*: Utafiti linganishi. Katika tasnifu yake hii mtafiti alimuangalia mwanamke katika nyanja kadhaa kama ifuatavyo: Mwanamke kama mshauri mwema, Mwanamke kama muwajibikaji, Mwanamke kama mtu jasiri, Mwanamke kama mlezi wa familia, Mwanamke kama mtu mwenye mapenzi ya dhati, Mwanamke kama chombo cha starehe, Mwanamke kama msomi n.k

Mtafiti alifafanua mwanamke huyo kama alivyosawiriwa, na jinsi alivyobebeshwa dhima mbalimbali katika riwaya husika. Mtafiti pia aliweza kulinganisha na kulinganua jinsi mwanamke huyo alivyosawiriwa katika njanja zote kama nilivyokwisha kuzitaja hapo awali lakini pia changamoto mbalimbali zilivyojitokeza katika riwaya ya *Utengano* na *Kamwe si mbali tena* .

Mtafiti anaona kwamba kazi hii tangulizi imemsaidia sana katika kazi yake ya usawiri wa mwanamke kwani ameweza kuhusisha kazi yake hii katika kuangalia vipengele muhimu atakavyoweza kuvitumia katika mada yake ya usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Mfadhili.*

Kwa kuhitimishia tunaweza kusema kuwa, sehemu hii ya Mapitio ya kazi tangulizi kuhusu usawiri wa mwanamke katika yametoa mwanga mkubwa na wenye mafanikio katika utafiti huu kwa sababu yameangazia uwepo wa pande mbili juu ya matendo ya mwanamke, yaani matendo hasi (maovu) na matendo chanya ( mema).

Hali hii imemsaidia sana na kumpa nguvu mtafiti ya kufikia mada yake kwani ameweza kwa kina kuyafikia malengo yake na hata kuweza kujibu maswali yake ya utafiti katika mada isemayo: Kutathmini usawiri wa mwanamke katika riwaya yake ya *Mfadhili*.

**2.4.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Mwandishi Hussein Issa Tuwa**

Mwandishi Hussein Issa Tuwa ameandika vitabu vingi vya riwaya. Baadhi ya vitabu vyake ni pamoja na*: Shangazi Kutoka Mjini (2003), Mfadhili (2007), Mkimbizi (2007) Mdunguaji (2012) Bondia (2012) Miss Tanzania (2013), Utata wa 9/12 (2013), (2015) Wimbo wa Gaidi (2017) Mtafiti (2015), Mtuhumiwa (2015) na Wimbo wa Gaidi* .

Venance, (2012) aliandika makala kuhusu riwaya ya *Mfadhili*. Katika makala yake alizungumzia mtiririko wa fani na maudhui katika riwaya ya *Mfadhili*. Baadhi ya vipengele vya fani alivyovitaja ni pamoja na muundo, mtindo, lugha na pia aligusia baadhi ya vipengele vya maudhui kama vile mapenzi, usaliti, uwajibikaji, umoja na mshikamano, migogoro nk.

Baada ya kusoma makala hii mtafiti aligundua kwamba pamoja na kuwa mwandishi hakugusia usawiri wa mwanamke lakini vipengele vya mapenzi, usaliti, uwajibikaji vimemgusa mwanamke na kwa hivyo vimemsaidia sana mtafiti katika mada yake ya usawiri wa mwanamke katika riwaya teule ya *Mfadhili*.

Casuits ( 2014 ) yeye kwa upande wake aliandika makala sehemu ya kwanza hadi ya kumi (1- 10) katika riwaya ya *Bondia.* Katika makala yake hiyo alizungumzia maisha ya Inspekta Fatma na Roman aliyefungwa jela. Makala hiyo ilizungumzia mambo kadhaa kama vile urafiki, mapenzi, msiba, maisha ya gereza, biashara, mahusiano, mechi za ngumi za kitaifa nk.Katika makala hii Casuits (ameshatajwa) alizungumzia mapenzi ya kweli na uongo na athari zake.

Mtafiti ameisoma kwa kina makala hii na kugundua kwamba pamoja na kuwa haikuzungumzia usawiri wa mwanamke lakini iligusia vipengele vya mapenzi na mahusiano ambapo mtafiti aliweza kuona kwamba vipengele hivyo vimemgusa pia mwanamke na kwa hivyo vimemsaidia sana mtafiti katika mada yake ya usawiri wa mwanamke katika riwaya teule ya *Mfadhili*. Masatu (2015) pia nae aliandika makala kuhusu riwaya ya *Mfadhili.* Katika makala yake hiyo Mastu(keshatajwa) aliandika kuhusu fani na maudhui katika riwaya ya *Mfadhili.* Baadhi ya vipengele alivyovitaja ni pamoja na lugha, mundo, mtindo, wahusika na mandhari. Pia aliandika baadhi ya vipengele vya maudhui kama vile usaliti, mapenzi, uwajibikaji, umuhimu wa elimu na nyenginezo.

Baada ya kusoma makala hii mtafiti aligundua kwamba pamoja na kuwa mwandishi hakugusia usawiri wa mwanamke lakini vipengele vya mapenzi, usaliti, uwajibikaji umuhimu wa elimu vimemgusa pia mwanamke na kwa hivyo vimemsaidia sana mtafiti katika mada yake ya usawiri wa mwanamke katika riwaya teule ya *Mfadhili.*

## 2.5 Pengo la Maarifa

**M**paka sasa tafiti mbalimbali zimefanyika kuhusu usawiri wa mwanamke katika kazi za fasihi. Pamoja na ukweli huu lakini mtafiti hajaona kazi ambayo imefanyika kwa kina kwa nia ya kutathmini usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Mfadhili* ya Hussein Issa Tuwa. Hata hivyo, baada ya utalii wa kina uliofanywa na mtafiti kuhusiana na maandishi tangulizi inaonesha kuwa bado hakujafanyika utafiti wenye kuchambua kwa kina kazi ya mwaandishi huyu teule kwa kutumia nadharia ya ufeministi. Hivyo, inaonesha kuwa kuna pengo kubwa ambalo linapaswa kuzibwa katika taaluma ya fasihi ya Kiswahili. Utafiti huu basi, utajaribu kuziba pengo hilo kwa kutathmini usawiri wa mwanamke katika riwaya hiyo teule ya *Mfadhili* na kuweza kuona ni kwa jinsi gani mwanamke huyo amesawiriwa katika nyanja zote za kijamii, kiuchumi, kielimu na katika mazingira tofauti.

## 2.6 Mkabala wa Kinadharia

"Nadharia" ni dhana yenye mawanda mapana. Wataalamu wengi wamejadili dhana hii kwa mapana na marefu kwa mujibu wa mitazamo yao. Miongoni mwa wataalamu hao ni pamoja na hawa wafuatao:

Msokile, (1993) anafafanua kwamba: Nadharia ni mawazo, mpango, mwongozo, maelezo, yaliyowekwa ili kusaidia kutatua au kutekeleza jambo fulani. Wamitila (2002) yeye kwa upande wake anaeleza kwamba: Nadharia za uhakiki ni muongozo unaomuelekeza msomaji na mhakiki kwenye vipengele vya msingi vya nadharia anayoitumia. Wafula na Njogu (2007) wanasema kwamba: Nadharia ni jumla ya

maelekezo yanayomsaidia msomaji au mhakiki kuifahamu kazi ya fasihi kwa kufuata utaratibu maalum.

Wamitila (2008) anafafanua kuwa: Nadharia ni maarifa ya kitaaluma ambayo msomaji au mhakiki anapaswa kuyajua na kuyafahamu kabla ya kuianza kazi yake. Haya ni maarifa ambayo inatupasa kuwa nayo kabla ya kujihusisha na kazi ya uhakiki. Ni maarifa ambayo yatamwezesha msomaji pia kuyaelewa mambo muhimu na kwa njia hiyo, kuuboresha usomaji wake na uwezo wake wa kuifurahia fasihi. Maarifa haya yote ni sehemu ya *Nadharia ya Fasihi.*

Kwa ujumla tunaweza kusema kwamba: Nadharia ni jumla ya maelekezo, taratibu, kanuni, misingi, mwongozo na mpango unaotumiwa na msanii au mhakiki/ mtafti ili kumsaidia kuifanikisha au kutekeleza kazi yake ya fasihi katika kiwango cha ubora au ufanisi zaidi.

Kwa hakika kila nadharia huwa ni muhimu na yenye ubora na upungufu wake. Uteuzi wa nadharia bora unaitategemea a mtafiti mwenyewe. Mtafiti anapaswa kuteuwa nadharia inayomfaa kwa mujibu wa mada, malengo na maswali ya utafiti wake. Kutokana na hali hiyo mtafiti amekusudia kutumia nadharia ya ufeministi. Msingi mkubwa wa kuchagua nadharia hii ni imani ya mtafiti ya kwamba nadharia hii itaweza kufanikisha vyema na kwa kiwango cha juu malengo na maswali ya utafiti huu ambayo ndio roho kuu ya utafiti huu. Nadharia hiyo imechambuliwa vyema ikihusishwa na misingi/mihimili yake kama ifuatavyo:

### 2.6.1 Nadharia ya Ufeministi

Wamitila (2002) anasema, uhakiki wa kifeministi una sifa sawa na nadharia za mwitikio wa msomaji. Sifa hii ina ugumu uliopo wa kubainisha ni kipi hasa kinachorejelewa na dhana yenyewe. Tatizo hili linatokana na uhalisi kuwa, nadharia hii inaifumbata pamoja mikabala na mitazamo kadhaa. Yote kwa ujumla inajulikana kama Ufeministi.

Wafula na Njogu (2007) wanaeleza kuwa: Nadharia ya Ufeministi ni nadharia inayoyaangalia na kujaribu kutatua matatizo yanayowakabili wanawake katika jamii inayotawaliwa na wanaume. Matatizo ya wanawake yanahusiana na yanasababishwa na jinsia. Hii ina maana kwamba shida nyingi zinazowakumba wanawake zimejengeka kwenye misingi ya jinsia yao. Kwa sababu ya jinsia, mwanamke amewekwa katika kitengo maalum cha jamii. Nadharia inayohusu masuala ya wanawake inajaribu kufichua matatizo yawapatayo wanawake kama tabaka la kiuchumi na pia kama wanawake.

Ufeministi ni dhana inayojumlisha mikabala mbalimbali ya kiuhakiki ambayo licha ya tofauti zake, inaelekea kukubaliana na kuafikiana kwenye masuala kadha na malengo yake ya kimsingi. Kimsingi, hii ni nadharia ambayo imewekewa msingi na msukumo mkubwa pamoja na nia ya kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kiutamaduni, kidini, kijamii, kisiasa na kiuchumi – pingu ambazo zimejengeka kwenye misimamo na itikadi za kiume. Kwa mujibu wa wahakiki wa kifeministi kama Birke (1986) na Lovenduski na Randall (1993), Ufeministi ni dhana inayoelezea hali na tendo la wanawake wanaodai kujieleza katika jamii mbali na

wanaume wanaounga mkono jitihada za wanawake hao. Ni dhana inayopinga mfumo dume.

Nadharia ya Ufeministi iliasisiwa na Mary Wollstonecraft katika makala yake ya *A Vindication of the rights of women* iliyochapishwa katika mwaka wa 1792 huko Uingereza. Katika makala yake ya kwanza kabla ya kushughulikia masuala ya wanawake alikuwa ameshughulikia haki za mwanamume. Makala yake yaliyotetea haki za mwanamke *A Vindication of the rights of women* yalikuwa na athari katika kumuwaza mwanamke huko Uingereza na Amerikani. Malengo ya mwandishi huyu yalikuwa kuonesha dhahiri anayoyapitia mwanamke katika jamii. Ufeministi uliendelea na huku ukipata kuungwa mkono na wengi. Wanawake wamekuwa wakipigania haki zao katika kipindi chote ambacho binaadamu ameitawala sayari hii. Kinadharia, masuala ya kifeministi yalianza kuzungumziwa karne ya kumi na tisa (19) na kutia fora katika miaka ya 60 na 70 ya karne iliyopita ambapo wanawake, hasa wa Kimagharibi walianza kuzungumza juu ya matatizo yao kwa utaratibu, yaani katika machapisho.

#### 2.6.1.1 Matapo Mbalimbali ya Ufeministi

Wafula na Njogu (wameshatajwa) wameainisha matapo ya aina mbili kuu kuhusu Ufeministi.

##### 2.6.1.1.1 Ufeministi wa Kimaeneo

Katika tapo hili wanawake kutoka sehemu mbalimbali za ulimwengu wanasisitiza masuala tofautitofauti yanayowakabili. Wahakiki waliojizatiti kuuainisha Ufeministi

katika makundi tofauti tofauti ni Mary Eagleton (1991) na Ross Murfin (1991). Kuna sehemu nne za ulimwengu zilizohusishwa na tapo hili: (i) Kifaransa (ii) Kimarekani (iii) Kiingereza (iv) Kiafrika.

**Wafaransa**: Wanawake wa Kifaransa wanatilia mkazo Lugha. Utafiti wao unalenga katika kufafanua namna lugha inavyomtolea maana mtumiaji wake. Wanadai kwamba lugha kama inavyotumika ni zao la taasubi ya kiume. Inampendelea mwanaume zaidi kuliko mwanamke. Jazanda zenye kuelezea uwezo, nguvu na mamlaka ni za kiume na ilhali zile zenye kusawiria ulegevu na kutoweza ni za kike.

**Wamarekani:** Wanakubaliana na Wafaransa kuhusu lugha. Wanaongezea kwamba wanawake wana namna yao ya kipekee ya kuandika na kujieleza. Pia wanasema kwamba kuna dhamira zinazorudiwarudiwa katika tungo za wanawake. Wanashughulikia kazi za fasihi zilizotumgwa na wanawake na hata zile zilizotungwa na wanaume wanaume maadamu zinaongea juu ya wanawake.

**Waingereza:** Wanaiona dhima yao kuwa ya kisiasa. Wanafikiria kwamba wenzao wa Kimarekani wanazungumzia zaidi masuala ya kihisia na kisanaa na kusahau historia na siasa. Kwao, mambo ya historia na siasa ndiyo huathiri matendo ya wanawake.

**Waafrika:** Wanawake wa Kiafrika wanasisitiza zaidi upinzani dhidi ya utamaduni unaomnyima mwanamke nafasi ya kutekeleza malengo yake. Miongoni mwa vitengo vya utamaduni huu ni: Kukosa uwezo wa kuchagua kuwa mke au mzazi wa mwanajamii, Tohara na ukeketwaji wa wanawake, Kimya cha kulazimishwa na

desturi na mila zinazomdhalilisha. Miongoni mwa mambo ni kama vile kuonewa kwa mwanamke asiyezaa au kuzaa wasichana watupu bila ya wavulana.

#### 2.6.1.1.2 Ufeministi wa Kiitikadi

Adamson, Briskin na McPhail (1988) wanabainisha mitazamo mitatu ya Kifeministi:

**Ufeministi Huru:** Hutetea usawa kati ya wanawake na wanaume katika ngazi zote za maisha. Wakati mwingine Ufeministi huu huitwa Ufeministi wa Kibepari. Mkondo huu hushikilia kwamba maadamu wanaadamu wameumbwa kuwa viumbe sawa, wote wake kwa waume wanapaswa kuwa huru kutekeleza majukumu na malengo yao.

**Ufeministi wa Kiharakati:** Huu humchukua mwanamume kama adui mkubwa wa mwanamke. Waitifaki wa mkondo huu wanaamini kuwa uwezo wa mwanamke wa kuzaa ndio ambao hutumiwa na mwanaume kumdhalilisha na kumtawala mwili wake. Kwa hivyo, ili wanawake waweze kujitawala katika nyanja zote za maisha wanahimizwa wasiolewe na wanaume. Kinyume na haya wanahimizwa kushirikiana wao kwa wao hata kimapenzi.

**Ufeministi wa Kijamaa:** Ufeministi wa kijamaa hulenga kukosoa ujamaa wa kimapokeo ambao licha ya kudai kwamba msingi wa unyonyaji ni jamii ya kitabaka inayompa uwezo mwenye kumiliki njia kuu za kuzalisha mali kutumia mali hiyo kadiri ya uwezo wake, huendeleza utabaka na unyonyaji katika misingi ya kijinsia .Ufeministi wa kijamaa unawahimiza wanaume kushiriki katika malezi ya watoto na kadhia nyengine ambazo kimapokeo zimechukuliwa kuwa kazi za wanawake.

#### 2.6.1.2 Mihimili ya Nadharia ya Ufeminist

Wafula na Njogu (wameshatajwa) kwa kuzingatia matapo ya Kimaeneo na Kiitikadi wanafafanua mihimili ya nadharia ya Ufeministi kwa ujumla kama ifuatavyo:

i. Ni nadharia inayotumia Fasihi kama jukwaa la kuelezea kwa uyakinifu hali aliyonayo mwanamke ili kumsaidia mtu yeyote kuielewa hali hiyo.
ii. Nadharia hii inanuia kuwasawazisha wanadamu kwa upande wa utamaduni na uana. Inapigania jamii mpya yenye msingi katika amali za kibinaadamu: Baadhi ya amali ni za kike na za kijadi na ambazo zinadharauliwa katika jamii ya sasa.
iii. Mtazamo huu vilevile unajaribu kuhamasisha utungaji wa kazi za sanaa zenye wahusika wa kike wanaoweza kuigwa, wanawake ambao hawawategemei wanaume ili wajitambulishe.
iv. Ni nadharia inayokuza na kuendeleza hisia za umoja wa wanawake kama kundi linalodhulumiwa.
v. Nadharia hii hunuia kuzindua mwamko kwa upande wa wanawake jinsi wanavyojiona, na uhusiano wao na wa watu wengine.
vi. Hatimaye, lengo muhimu la nadharia hii ni kuvumbua na kuziweka wazi kazi za fasihi zilizotungwa na wanawake na ambazo zimepuuzwa kwa sababu ya utamaduni unaompendelea mwanamume.

Ntarangwi (2004) anaeleza kwamba: Nadharia hii hudhamiria kuonyesha kwamba uana na uhusiano kati ya mwanaume na mwanamke ni mambo ya kati kabisa katika fasihi. Uhakiki huu pia hupiga hatua mbele na kuonyesha uhafifu wa hali ilivyo hasa katika nadharia nyingi za uhakiki. Wahakiki wanaozingatia nadharia hii hudai

kwamba tahakiki za kijadi zimekandamiza mjadala kuhusu uana jambo ambalo yaelekea ni kwa manufaa yao. Kwa hivyo azma kuu ya Ufeministi ni `kusoma upya' kazi za fasihi ili kusisitiza umuhimu wa vipengele vilivyopuuzwa na wahakiki wengi au ambavyo hawangeviona kwa sababu walikuwa wanafanya kazi katika nadharia za kijadi zinazomtukuza mwanaume.

Ama kwa hakika Ufeministi ni siasa. Siasa kwa sababu mfumo huu wa uhakiki unaelekezwa katika kubadilisha uhusiano uliopo sasa kati ya wanaume na wanawake. Uhusiano huu, ambao umejaa mivutano, hugubika miundo yote ya maisha. Miundo inayohusu maswali ya familia, elimu, kazi na siasa, utamaduni na hata mambo ya starehe na anasa. Hivyo basi, kwa kifupi ni kwamba uhusiano huu huongoza jinsi wanajamii wanavyoishi, wanachotenda, wanayemtendea, na jinsi watakavyokuwa siku za usoni.

**2.6.1.3 Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika**

Nadharia ya ufeministi wa Kiafrika iliibuka mwanzoni mwa karne ya ishirini. Nadharia hii iliasisiwa kwa mtazamo wa mwanamke wa kiafrika. Waasisi wake ni pamoja na Filomena Steady (1981), Olufemi Taiwo, Ayesha Imam na Okeke (1996). Waasisi wa nadharia hii waliweza kuwa na mtizamo sawa juu ya masuala ya wanawake barani Afrika.

Steady (1981) anasema: Ufeministi wa Kiafrika umejikita katika mwelekeo wa kuangalia majukumu tofauti ya kijinsia kama yanayoegemeana na kukamilishana. Anaendelea kusema kwamba majukumu haya yanaenda sambamba na jinsia na hata

kusababisha hali ya usawa. Maswala ya ubaguzi, uana, utabaka na mielekeo ya utamaduni huletwa pamoja ili kuanzisha ufeministi unaomwangalia mwanamke kama kiumbe wala sio kwa msingi wa kijinsia. Ufeministi unachunguza utamaduni unaomlemaza mwanamke. Hili ni muhimu katika utafiti huu ikizingatiwa kwamba katika tamaduni nyingi za Kiafrika dhana ya ukuu wa mwanamume dhidi ya mwanamke si swala geni. Dhana hizi za ubaguzi, uana na utabaka hazikuwepo katika utamaduni wa kiasili wa Kiafrika lakini ziliingia kupitia kwa athari za kikoloni na kibepari. Mabepari walitoa mchango mkubwa kupitia kazi ambazo zilitengewa wanaume na wanawake.

Millett (1977) anasema: Ufeministi wa Kiafrika umetokana na utamaduni katika jamii iliyojikita katika kilimo na ushiriakiano wa kijamii. Umejengeka katika misingi thabiti ya kumhusisha mwanamke katika shughuli tofauti za jamii bila kuangalia asasi zinazotawaliwa na mwanamume. Kulingana na Millett, Ufeministi wa Kiafrika husisitiza usawa katika shughuli za jamii na utoaji uamuzi kwa wanawake na wanaume.

Strobel (1980) anauona Ufeministi wa Kiafrika kama uliokumbana na changamoto nyingi kutokana na asasi tofauti kwa sababu huwa unataka kujua chanzo cha ubaguzi katika maswala ya kiutawala. Mwelekeo pinzani unasisitiza uongozi wa jinsia ya kiume ambao umeupa changamoto nyingi sana mwelekeo wa Ufeministi wa Kiafrika.

Mwasisi wa Ufeministi huu wa Kiafrika Filomena Steady (1981) aanafafanua matarajio ya nadharia yenyewe. Kwake, nadharia inafaa kuchunguza hali za kijamii

na kiutamaduni zinazorutubisha unyanyasaji wa wanawake katika jamii. Nadharia yenyewe ina nyanja zifuatazo: **Mosi:** Inadhihirisha nia na malengo mahsusi yanayotokana na hali halisi katika jamii za Kiafrika. **Pili:** Inatambua historia ya jamii za Kiafrika, zilizokuwa na watawala na mashujaa wanawake. **Tatu:** Inachunguza hali ya mwanamke katika jamii ambazo zimekuwa na harakati za ukombozi na ujenzi wa jamii mpya. Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza mihimili ya kimsingi ya nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Wanasema Ufeministi wa Kiafrika ni kama jukwaa la kuelezea kwa uyakinifu hali aliyomo mwanamke wa Kiafrika ili kumsaidia mtu yeyote kuielewa hali hiyo. Mtazamo wa Ufeministi wa Kiafrika, vilevile hujaribu kuhamasisha utungaji wa kazi za sanaa zenye wahusika wa kike wanaoweza kuigwa na ambao hawawategemei wanaume ili kujitambulisha. Aidha, kisaikolojia wawe ni wanawake wanaojielewa na kujiamini wala wasiwe wanahisi kama wana udhaifu kwa ajili ya uwanauke wao.

Kuibuka kwa nadharia ya ufeminsti wa Kiafrika ni kutokana na mielekeo mikali iliyotoka Umarekani, iliyochukulia kwamba mwanamume ni adui ya mwanamke na kamwe mwanamume hawezi kushiriki katika ukombozi wa mwanamke. Pia mielekeo hii huunga mkono ndoa za jinsia moja. Nadharia ya mtazamo kike yenye msingi wa ufeministi wa Kiamerikani ndiyo yenye misimamo hii mikali. Wafuasi wake hudai kuwa ushirikiano mzuri ni wa baina ya wanawake tu. Kwa kuwa na baadhi ya arki au elementi ambazo haziwiani vyema na masuala ya mwanamke hasa wa Kiafrika. Pia waasisi wake walikuwa wanawake wa kimagharibi na kuandika kwao kulitegemea kuhadithiwa yanayofanyika. Kwa sababu hiyo maoni na msimamo yao ikawa na athari ya kupotosha na kukengeusha.

Ili kujikita katika masuala halisi ya mwanamke wa kiafrika, nadharia ya ufeministi wa Kiafrika ilijitokeza na kupata hadhi ya kushughulikia masuala ya wanawake baada ya mijadala mikali na kuwa faafu mno. Sifa zake zinaakisi tajriba na hali halisi ya mwanamke wa Kiafrika. Aidha utamaduni wa Mwafrika ni tofauti sana na wa mwanamke wa kimagharibi. Mathalani inawezekana sana yanayomkera na kumfinyilia mwanamke wa Kiafrika huenda si kero ama dhuluma kwa mwanamke wa kimagharibi.

Bara la Afrika kwa mtazamo wao ni kwamba, mwanamke wa kiafrika huwa hana uwezo ila kudhulumiwa chini ya himaya ya ubabedume uliotiliwa nguvu na tamaduni na mila za jamii na ukawa umekita mizizi barani Afrika. Kutokana na hayo wanaharakati wa masuala ya mtazamo kike barani Afrika wamekuwa katika harakati za kuwasilisha matatizo yanayowakumba wanawake wa bara la Afrika pamoja na ukombozi wao.

Wito wa kutaka kupigania haki na usawa ilitokana na misimamo ya baadhi ya wanasaikolojia waliomchanganua mwanamke na kumpa nembo mbalimbali kulingana na mtazamo wao. Kwa mfano Mwanasaikolojia Freud (1927) alichangia pakubwa kuweka wazi suala la jinsia kupitia Nadharia ya Jinsia. Wanaharakati wa mtazamo kike na waliochangia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ni kama vile Betty Friedan na Kate Millet walipinga vikali maoni ya Freud maana waliona yalidhalilisha na kumtweza mwanamke na kumtwaza mwanamume.

Wamitila (2002) katika *Uhakiki wa Fasihi* alimnukuu Freud Sigmund akisema kuwa mtoto wa kike huanza kujidunisha na kujidharau punde tu anapotambua kuwa hana kiungo cha kiume. Freud aliita hali hii 'Wivu wa Zubu'. Millet yeye kwa upande wake alipinga dhana hii kwa kusema "wivu" uliopo ni wa mwanamume kuwa na uwezo kutokana na muundo wa jamii kwa kuwa na 'zubu' inayoashiria au kuonesha nguvu fulani lakini si kuwa na kiungo chenyewe. Uana ni dhana inayodhihirisha majukumu ambayo ni ya kike na kiume. Hili lilizua mushkili mkubwa. Hii ni kwa sababu majukumu aliyopewa mwanamke yalishabihiana na maumbile yake kama vile kuzaa, kulea, kupika na kadhalika. Majukumu haya yaliunda nafasi nzuri ya kumdhulumu na kumdunisha mwanamke. Simon de Beavoir (1974) katika makala iitwayo *The Second Sex* kama alivyonukuliwa na Wamitila katika *Uhakiki wa Fasihi* ni kuwa ulikuwa wa kuushambulia uana ambao ni dhana ya kitamaduni inayomwangalia mwanamke kama kitu hasi na duni na huku ikimchukulia mwanamume kama binadamu kielelezo. Pia alisisitiza kuwa utamaduni anamokulia mwanamke unachangia kumdidimiza na kuwa mnyonge. Utamaduni huo unamfanya na kumlazimisha mwanamke akubali kuwa ni kiumbe duni. Mwanamke amekubali kufanywa na jamii yake kama chombo cha kuendeleza utamaduni hasi.

Hivyo nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika haina budi kuzama katika mila, desturi na kaida za kijamii ili ibainishe nafasi ya mwanamke na uwezo wake katika utendakazi sambamba na anavyofanya mwanamume. Pia nadharia ya ufeminist inadhima ya kuangalia dhuluma atendewazo mwanamke katika ufanisi wake kulingana na ulimwengu ulivyo. Yanayoangaziwa na nadharia hii ni mahusiano ya jamii baina ya mwanamume na mwanamke, asasi za jamii zilizojengwa na kuhimiliwa kwa misingi

ya uana, utamaduni wa kigeni na athari zake na maonevu mengine kama ukeketwaji, ndoa zisizo za hiari, ukewenza na udunishwaji. Yote haya hutiliwa nguvu na taasubi ya mwanamume.

Nadharia hii aidha hujishughulisha na masuala ya kuyamudu maisha ndani ya mfumo wa ugandamizwaji. Wanawake wa Afrika wanapigania haki zao kama vile kuweza kumiliki ardhi na mali, kuwa na uhuru wa kujiamulia bila dhuluma, suala la usalama wao katika utekelezaji wa kazi zao, kuthibiti ajira na ugawaji wa chakula. Masuala yote yanayorejelewa na nadharia hii juu ya dhuluma yamesawiriwa vyema katika fasihi ya Kiswahili. Mfano kupitia riwaya, waandishi wengi wamewasawiri wanawake katika hali mbili kubwa (hasi na chanya). Kwa upande wa hali hasi (matendo maovu) kama dhuluma katika mirathi, umiliki wa mali, ukatili na ukeketwaji. Mambo mengine hasi yanayomkabili mwanamke ni ndoa za kulazimishwa, ukosefu wa elimu, ubakwaji, kufanywa masuria, kugeuzwa au kujigeuza kuwa makahaba, chombo cha kuwastarehesha wanaume.

Kwa upande wa hali chanya (matendo mema), Fasihi ya Kiswahili imeweza kuwasawiri wanawake kama viumbe wenye umahiri mkubwa katika kufanya maamuzi bora. Pia waandishi hao wamewahi kuwasawiri wanawake kuwa mashujaa wa kujitoa mhanga kupigania haki zao na za wengine na kuipiga vita mifumo ya udhalimu. Wanawake pia wamewahi kusawiriwa kama wasomi waliobobea, washauri wema, walezi wazuri wa familiya na mengineyo. Mfano mzuri wa kazi za Fasihi ya Kiswahili zinazodhihirisha kauli hii pamoja na kuipa nguvu nadharia ya ufeministi wa Kiafrika ni riwaya ya *Nyota ya Rehema* ya Muhamed S.Muhamed

(1976), *Utengano (1980), Nyuso za Mwanamke (2010), Kamwe si mbali tena (2014) zote za Said Ahmed, Wasifu wa Siti bint Saad ya Shaaban Robert* na nyingi nyenginezo.

Utafiti huu umejikita kutumia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kutathmini usawiri wa mwanamke katika riwaya teule ya *Mfadhili. Nadharia hii imechaguliwa* kwa sababu ni moja kati ya nadharia adhimu inayoakisi kusawiri mwanamke katika matendo yake mbalimbali yanayodhihirisha usawiri wake katika riwaya yetu teule ya *Mfadhili.*

## 2.7 Hitimisho

Sura hii inahusu kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Mtafiti ameelezea kwa kina mambo yote muhimu yanayohusu sura hii. Ameanza kuifafanua sura hii kwa kuanzia na utangulizi, Baadae mtafiti alizungumzia maana ya kazi tangulizi, ambapo alitoa mifano ya waandishi mbalimbali wa tasnifu. Baada ya hapo mtafiti ametoa ufafanuzi wa istilahi mbalimbali. Mtafiti alizungumzia kuhusu pengo la maarifa. Kuhusu mkabala wa kinadharia mtafiti aligusia kuhusu dhana ya nadharia huku alijikita zaidi katika nadharia ya ufeministi na mwisho akatoa hitimisho la sura.

# SURA YA TATU

# 3.0 MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti ameangalia mambo ya msingi yafuatayo: Mbinu za Utafiti, Eneo la Utafiti, Usanifu wa Utafiti, Kundi Lengwa, Sampuli na Usampulishaji, Aina za Data, Data za Msingi, Data za Upili, Mbinu za Kukusanya Data kwa ujumla huku akibainisha Mbinu za Kukusanyia Data za Msingi na zile za Kukusanyia Data za Upili. Vipengele vyengine alivyoangazia ni Upitiaji wa Nyaraka, Uchambuzi wa Data, Mkabala wa Kimaelezo, Usahihi wa Data za Utafiti, na mwisho akamalizia kipengele cha hitimisho.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Enon (1998) anaeleza kuwa: Eneo la utafiti la kijiografia ni pahala mahsusi ambapo mtafiti amekwenda au amekutumia kukusanya data za utafiti wake. Eneo la utafiti ni mahali ambapo utafiti umefanyika au umekusudiwa kufanyika. Katika eneo la utafiti ndipo data za utafiti hupatikana kwa mtafiti kufanya usaili, mahojiano, kushuhudia au kushiriki shughuli au tukio fulani pamoja na watafitiwa (Babbie, 1992).

Kwa kuzingatia umbo la mada ya mtafiti: *Kutathmini Usawiri wa mwanamke katika riwaya ya Mfadhili,* mtafiti amekusanya data kwa kutumia mbinu ya maktabani: Mtafiti ametumia maktaba za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA). Maktaba nyengine alizotumia ni Maktaba Kuu Zanzibar, na Maktaba ya Wilaya ya Wete. Mbali na hayo wavu pepe na

vyanzo vinginevyo vimetumika kwa lengo la kupata taarifa nyenginezo zilizohusiana na mada ya utafiti.

### 3.2.1 Sababu za Uteuzi wa Eneo la Utafiti

**Mosi, Urahisi wa upatikanaji wa data husika:** Mtafiti kwa makusudi ameamua kuteua maeneo hayo kwa sababu imekuwa ni rahisi kwake kuweza kuyafikia na kuyatumia katika utafiti. Kwa sababu ya urahisi huo mtafitiamepata fursa nzuri ya kufanya marejeleo yanayohusu kazi yake.

**Pili: Uteuzi wa Maktaba tajwa:** Mtafiti ametumia maktaba mbalimbali zilizotajwa; Maktaba ya Chuo Kikuu Huria Tanzania, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Maktaba kuu Zanzibar, (zote tawi la Pemba). Sababu kubwa ya mtafiti kuchagua maktaba hizo ni kuwa zote zinapatikana kisiwani Pemba ambapo mtafiti anaishi. Hivyo mtafiti ameweza kufika maeneo husika kwa lengo la kukusanya taarifa anazozihitaji. Pia taarifa alizozihitaji mtafiti amezipata katika maktaba hizo lakini katika kiwango tofauti. Kiwango hicho kimesaidia sana kufanikisha kazi ya mtafiti ipasavyo hususan ile inayomuhusu mwanamke.

**Tatu: Matumizi ya Wavupepe (Internet)**: Matumizi ya wavu pepe yalikuwa na umuhimu mkubwa katika kuongezea maarifa mbalimbali kuhusu mada ya utafiti. Mtafiti ametumia wavu pepe kwa lengo la kupata taarifa za ziada kutoka vyanzo vyenginevyo kulingana na mada ya utafiti. Hivyo basi wavu pepe zina umuhimu mkubwa kwa mtafiti katika kufanikisha mada ya utafiti wakati wa kurejelea.

Kwa muhtasari eneo la utafiti lina mchango mkubwa katika kujenga uhalali wa taarifa zitazokusanywa na mtafiti wakati wa uchambuzi wa taarifa (data) na kuifanya kazi ya utafiti iwe na uhai na yenye kuaminika na kuleta tija kwa umma wote.

## 3.3 Kundi Lengwa

Enon (1998) anaeleza kwamba: Uteuzi wa kundi lengwa ni ule wa mtafiti kwenda moja kwa moja kwenye chanzo cha data atakazozihitaji ili kupata data za utafiti wake. Mtafiti atatumia uteuzi wa kundi lengwa katika mada husika. Uteuzi lengwa ni uteuzi ambao huteuliwa na mtafiti kwa makusudi akifahamu kuwa uteuzi huo utampatia data sahihi ambazo zimejibu maswali yake ya utafiti (Babbie,1999). Kundi lengwa ni jumla ya watu wote ambao huhusishwa katika utafiti (Kothari, 2004). Walengwa waliohusishwa katika utafiti huu ni riwaya teule ya *Mfadhili.* Msingi wa uteuzi lengwa umetokana na sababu kuu zifuatazo:

**Mosi,** Riwaya teule ya *Mfadhili.* Msingi mkubwa wa kuteua riwaya hii ni kwamba mtafiti anaamini bado riwaya hii haijawahi kufanyiwa utafiti jambo lililomchochea mtafiti kufanya utafiti huu.

**Pili,** Riwaya hii imefanikisha vyema malengo na maswali ya utafiti kupitia mada husika ambayo ni: *Kutathmini Usawiri wa mwanamke katika riwaya ya Mfadhili.* Kwa msingi huo mtafiti anaamini kwamba kitabu teule cha *Mfadhili* kimefanikisha vyema kiu ya mtafiti kwa mujibu wa mada yake kwa kiwango kikubwa kinachostahiki.

### 3.4 Sampuli na Usampulishaji

Kwa mujibu wa Kothari (1990, 2004) Sampuli ya watafitiwa ni kundi dogo la watafitiwa lililochaguliwa kuwakilisha sifa na tabia za kundi zima ambalo humsaidia mtafiti kupata taarifa kutoka sampuli hiyo ili kutoa majumuisho ya utafiti wake. Bryman (2004),amekuja na maoni yasemayo kwamba, Uteuzi wa Sampuli ni mchakato wa kuchagua kikundi cha vitu au watu ili kitumike katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi lolote linalotafitiwa. Ni muhimu kuteuwa kundi lengwa kwani sio rahisi kutafiti kundi zima linalohusiana na utafiti.

Hornby (2005), anaeleza kwamba: Sampuli ni kundi la watu au vitu vlivyoteuliwa kutoka kundi kubwa na ambavyo hutumika kwa lengo la kutoa taarifa kuhusu kundi kubwa. Pia tunaweza kusema pia Sampuli ni kundi dogo teuliwa litakalotumika kwa lengo la kutoa taarifa kuhusiana na jambo au mada fulani. Sampuli ni nyenzo muhimu katika kufikia hatua ya ukusanyaji wa taarifa zinazohitajika na mtafiti katika utafiti wake kulingana na mada.

**Usampulishaji** ni mchakato unaohusisha mbinu mbalimbali za uteuzi wa watafitiwa kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ambalo mtafiti hulifanya kwa lengo la kupata kundi maalum atakalolitumia katika ukusanyaji wa data zinazohusiana na mada ya utafiti. Kwa ujumla sampuli ni kipengele muhimu katika utafiti kwa sababu ni njia muhimu ya kufikia hatua ya kukusanya data. Kwa hiyo mtafiti ameamua kuchagua sampuli maalum kwa kuwa ni vigumu kutafiti kundi kubwa la watafitiwa. Sampuli aliyochaguwa mtafiti ni Sampuli lengwa.

### 3.4.1 Sampuli Lengwa

Yin (1994), anaeleza kwamba: Sampuli Lengwa ni aina ya sampuli ambayo mtafiti anateua watafitiwa ama vitafitiwa akiwa amejiridhisha kwamba watafitiwa hao watampatia data zitakazoweza kutimiza malengo ya utafiti wake. Babbie (1999) anaeleza kuwa: Usampulishaji lengwa ni mbinu ya uteuzi wa sampuli ya utafiti ambapo mtafiti huteua sampuli fulani ya watafitiwa wake akiamini kuwa sampuli hiyo ni sahihi na ndiyo itakayompa data sahihi za kuweza kutimiza malengo ya utafiti kwa wepesi na haraka.

Mbinu hii ya Usampulishaji lengwa imetumika katika kuteua riwaya ya *Mfadhili* ya mwandishi Hussein Issa Tuwa. Kwa kweli mbinu hii ndiyo msingi mkuu ambapo mtafiti amejiridhisha kwamba umekuwa toshelevu kiasi cha kutosha kuweza kumpata data za uhakika za utafiti wake ili kufanikisha vyema malengo na maswali ya utafiti ipasavyo. Mbinu ya Usampulishaji lengwa imempa manufaa makubwa mtafiti kwasababu imemuwezesha kupata ata za uhakika tena kwa muda mfupi. Vilevile mbinu hii imemfanya mtafiti kutokutumia muda mwingi kwenda kufanya utafiti kwa kundi ambalo halihusiki. Mtafiti amefanya utafiti wake kutokana na sampuli lengwa tu kulingana na malengo na maswali ya utafiti.

## 3.5 Ukusanyaji wa Data

Enon (1998) anaeleza kwamba: Ukusanyaji wa data, ni zoezi la awali katika utafiti. Zoezi hili, humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kumfikisha katika lengo lake la utafiti. Kothari (2004) anafafanua kwamba: Ukusanyaji wa data ndio zoezi la awali katika utafiti ambalo humuwezesha mtafiti kupata taarifa

alizozikusudia ili kumfikisha katika malengo yake ya utafiti. Aidha, hatua ya uwasilishaji na uchambuzi wa data haiwezi kufanyika kabla ya hatua ya ukusanyaji wa data. Kiudhati, katika utafiti wowote hususan wa kitaaluma ukusanyaji wa data huwa unajitokeza katika aina kuu mbili: Data za Awali (Msingi) na Data za Upili (Fuatizi).

### 3.5.1 Data za Awali (Msingi)

Adam na Kamuzora (2008) wanaeleza kwamba: Data za Awali ni aina ya data zilizokusanywa na mtafiti mwenyewe au msaidizi wa mtafiti kutoka katika eneo halisi kwa lengo la kujibu maswali yanayohusiana na mada ya utafiti. Kothari (2004) anaeleza kwamba: Data za msingi ni zile zinazokusanywa kwa mara ya kwanza na hivyo ni data halisi. Data hizi za msingi zinakuwa hazijapata kukusanywa na mtafiti mwingine kwa minajili ya utafiti kama huu ambao ulikusudiwa kufanywa kwa mara ya kwanza.

Kwa kuhitimisha, mtafiti anasema Data za awali ni aina ya data halisi na thabiti ambazo mtafiti huzikusanya kwa mara ya kwanza kutoka katika eneo alilolichagua kwa mujibu wa mada ya utafiti. Data za msingi katika utafiti huu zimetokana na riwaya ya *Mfadhili.*

### 3.5.2 Data za Upili (Fuatizi)

Kothari (2004), amekuja na maelezo yasemayo kwamba: Data za Upili ni data zote ambazo tayari zimekwishakusanywa na watafiti wengine na ambazo zimepitia katika hatua zote stahiki za ukusanyaji wa data. Kamuzora na Adam (2008) wanasema:

Data za Upili ni data zote zinazopatikana kutoka vyanzo tangulizi au data zilizokusanywa na watu wengineo kwa malengo maalum. Katika utafiti huu, mtafiti ametumia data za upili kwa lengo maalumu la kukazia, kushadidia na kutilia mkazo taarifa alizozipata kutoka katika data za awali (msingi). Katika kufanikisha dhamira hiyo, mtafiti amesoma kwa umakini kazi tangulizi zikiwemo, tasnifu, vitabu, makala, majarida, magazeti, ripoti na wavuti mbalimbali ambavyo kwa kiasi kikubwa vinahusiana na mada ya utafiti.

## 3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Mbinu za ukusanyaji data ni njia anazochagua mtafiti kuzitumia kukusanya data kwa ajili ya utafiti wake (Kothari, 1990). Kwa udhati kabisa utafiti wowote hauwezi kufanyika bila ya kuwepo mbinu za kukusanyia data. Mbinu za utafiti huu ni Usomaji makini kupitia Maktaba.

### 3.6.1 Mbinu ya Maktabani

Mbinu hii inalenga kutoa fursa kupitia kwa kina kazi mbalimbali zilizoko katika maktaba. Katika mbinu hii mtafiti ametumia mbinu ya Usomaji makini wa vitabu husika na kazi nyenginezo zinazoendana na mada akiwa na imani kubwa ya kupata taarifa zenye uhakika katika utafiti huo.

### 3.6.2 Usomaji Makini

. Enon (1998) kwa upande wake anasema kwamba: Mbinu ya usomaji makini ni mbinu inayomtaka mtafiti kukusanya taarifa kwa umakini baada ya kusoma kwa kina kazi husika kuanzia mwanzo hadi mwisho. Kothari (2004) anaeleza kwamba:

Usomaji makini ni mbinu inayolenga kusoma na kuchambua kwa undani (kwa kina) maudhui yanayojitokeza katika kazi husika kama vile vitabu, majarida pamoja na magazeti yanayoendana na mada inayohusika.

Katika utafiti huu, mtafiti kupitia njia ya maktabani ametumia mbinu ya Usomaji makini kwa kupitia kwa kina na hatua kwa hatua kuanzia mwanzo hadi mwisho riwaya teule ya *Mfadhili* na kunukuu sentensi pamoja na aya mbalimbali zinazohusiana na dhana nzima ya mwanamke na usawiri wake kwenye daftari (shajara) maalum aliloliandaa na kwa kuzingatia malengo na maswali ya utafiti. Kazi hiyo imefanyika kwa lengo la kupata data mbazo amezikusanya na baadae akaweza kuzichambua ipasavyo.

### 3.7 Mbinu za Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data ni kitendo kilichorasmi ambacho mtafiti hukifanya mara baada ya kukusanya data za utafiti kutoka katika vyanzo husika. Lengo la kuzichambua data hizo ni kupima uhalali wa taarifa zilizopatikana kwa mujibu wa mada ya utafiti. Katika utafiti huu, mtafiti ametumia mbinu ya mkabala wa kimaelezo katika uchambuzi wa data ili kufanikisha malengo ya utafiti na kupata matokeo sahihi.

#### 3.7.1 Mkabala wa Kimaelezo

Mkabala wa Kimaelezo ni mbinu ya uchambuzi wa data ambapo mtafiti huzichambua data zake kwa kuzitolea maelezo yanayohusiana na madhumuni ya utafiti wake (Kothari, 1990). Mtafiti amechagua mbinu hii katika uchambuzi wa data akiamini kwamba hii ni mbinu muwafaka hususan katika uchambuzi wa kazi za

Fasihi kwa ujumla. Dhana hii haina maana kuwa mbinu ya Kitakwimu haifai katika uchambuzi wa data. Mtafiti anatambua ubora wa mbinu zote (mbinu ya kitakwimu na kimaelezo) ila mtafiti ameona ya kuwa mbinu hii imetoa fursa kubwa na itakuwa ni nyepesi kuweza kuitumia kuchambua data kwa uwazi na kwa urahisi zaidi. Vilevile katika uchambuzi wa data, mtafiti amezingatia matumizi ya nadharia husika katika kuhusisha na mada ya utafiti, malengo na maswali ya utafiti. Nadharia ambazo zimetumika katika uchambuzi wa utafiti huu ni Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ambapo kwa ujumla zimeenda sambamba na mada ya utafiti isemayo: *Kutathmini Usawiri wa mwanamke katika riwaya ya Mfadhili.*

## 3.8 Usahihi wa Data za Utafiti

Mtafiti anaamini kwamba data zilizokusanywa ni sahihi kwa sababu zifuatazo: Mtafiti amepitia na kusoma kazi nyingi tangulizi ambazo zimepitiwa na kusahihishwa na walimu wabobezi wa fasihi na isimu wa vyuo husika na kukubalika.

i. Mtafitia amepitia na kusoma kwa kutumia mbinu ya usomaji makini na kukusanya data za uhakika kutoka katika vitabu vya riwaya , tamthiliya, majarida na mada mbalimbali ambazo mtafiti anaamini zimemsaidia vya kutosha katika kutoa majibu sahihi ya malengo na mswali yake ya utafiti.

ii. Mtafiti pia ametumia mitandao mbalimbali kama vile wavu pepe na mengineyo ambapo amepata maelezo ya kutosha yaliyomsaidia katika mada yake.

iii. Mtafiti amewasiliana hatua baaada ya hatua na baadhi ya walimu wake ambapo alipata maelekezo ya kutosha na kuifanya kazi yake kuwa rahisi na ya uhakika.

Katika utafiti huu mtafiti ametumia mbinu ya usomaji makini ili kuleta ufanisi zaidi. Mtafiti anaamini kwamba mbinu aliyoitumia inafaa zaidi kwa mujibu wa mada yake. Mbinu hii imemsaidia mtafiti kiasi cha kutosha na kwa hivyo kukamilisha malego na maswali ya utafiti.

## 3.9 Hitimisho

Sura hii nayo ina umuhimu mkubwa sana kwani imekuwa kama ni dira inayomuongoza mtafiti kufikia katika malengo aliyoyakusudia. Mtafiti amejikita katika mambo muhimu na ya msingi katika utafiti huu.

Vipengele vilivyozingatiwa ni Utangulizi wa sura, Mbinu za Utafiti, Eneo la Utafiti, Usanifu wa Utafiti, Kundi lengwa, Sampuli na Usampulishaji. Vipengele vyenine ni Aina za Data, (Data za Msingi na Data za Upili), Mbinu za Kukusanya Data, (Mbinu za Kukusanyia Data za Msingi, Mbinu za Kukusanyia Data za Upili), Upitiaji wa Nyaraka, Uchambuzi wa Data, Mkabala wa Kimaelezo, Usahihi wa Data za Utafiti, Maadili ya Utafiti, na mwisho Hitimisho. Kwa ujumla kila kipengele kina umuhimu wake katika kukamilisha kazi nzima ya utafiti huu kwa kiwango bora.

# SURA YA NNE

# 4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Kwa ujumla sura hii imezingatia msingi muhimu wa utafiti huu. Vipengele vya msingi vifuatavyo vitajadiliwa kwa kina: Usuli wa Mwandishi wa riwaya teule, Muhutasari wa riwaya teule ya *Mfadhili,* Usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Mfadhili* na sababu za usawiri huo kwa kutumia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika na mwisho hitimisho.

## 4.2 Usuli wa Mwandishi: Hussein Issa Tuwa

Hussein Issa Tuwa ni miongoni mwa waandishi wabobezi wa riwaya za Kiswahili. Mwandishi huyu amechipukia kuwa na kasi kubwa ya uandishi. Tuwa alizaliwa Novemba 1970 jijini Dar es Salaam Wilaya ya Ilala kata ya Mchikichini. Tuwa ni mtoto wa kwanza katika watoto watatu wa tumbo moja, ingawa wapo ndugu wengine amabo wamechangaya nae mama na wengine baba. Mwandishi huyu alioa mwaka 1997. Hivi sasa bwana huyu ana mke na mtoto mmoja. Hussein Issa Tuwa alipata elimu ya msingi katika shule ya msingi Osterbay kati ya mwaka 1977 na1984. Elimu ya sekondari ya awali (O level) alisoma katika shule ya Kiislamu ya Seminari Masjid Qubar kati ya mwaka 1985na 1989. Elimu ya sekondari ya juu (A. level) aliisoma katika shule ya sekondari ya kiislamu ya Al- Haramain kati ya mwaka 1990 na1991. Bwana Tuwa pia ni muhitimu wa shahada ya kwanza ya Utawala na Uongozi (Bachelor of Arts-Public Administration) Chuo Kikuu Dar es Salaam. Ni program

ya miaka mitatu kati ya mwaka 1993 na1996. Tuwa pia alipata taaluma ya Shahada ya Pili (Masters) ya Uongozi wa makampuni (MBA-cooperate Management) Chuo Kikuu cha Mzumbe Kituo cha Dar es Salaam, kati ya mwaka 2010 na 2011.

Hussein Issa Tuwa ameandika riwaya zifuatazo: *Shangazi Kutoka Mjini (2003), Mkimbizi (2004), Mfadhili* (2007), *Mdunguaji* (2012), *Bondia* (2012), *Miss Tanzania* (2013), *Utata wa 9/12* (2013), *Mtafiti* (2015), *Wimbo wa Gaidi* (2017). Mwandishi huyu alianza uandishi wake 1992 na amepata tunzo ya BURT Award for African Literature kwa kuandika riwaya ya *Temporary Orphan.* Tuwa ana upekee uliojichomoza katika kazi zake kwani riwaya zake huwa zinataja wadhifa / nafasi ya muhusika wa kisa husika mfano *Mfadhili, Mkimbizi, Mdunguaji, Mtuhumiwa,* nk. Hata hivyo Tuwa anazo riwaya nyengine ambazo hazikuwa na majina ya aina hiyo. Kwa sasa Mwandishi Hussein Issa Tuwa ni afisa wa Shirika la Kimataifa nchini (Human Resource Mananger) akiwa kama mtaalamu wa Ujasiriamali watu.

### 4.3 Muhutasari wa Riwaya ya Mfadhili

Riwaya ya *Mfadhili* ni miongoni mwa riwaya nzuri na ya kusisimua sana. Riwaya hii imewagusa moja kwa moja wasomaji na wanajamii kutokana na dhamira zake na jinsi zinavyoakisi uhalisia wa maisha ya kileo. Mwandishi Hussein Issa Tuwa amewaacha hoi wasomaji baada ya tanzia kubwa aliyoionyesha kwa nguli (Gaddi Bullah) kufariki mwisho ambapo kila msomaji ataacha mdomo wazi kwa tukio hilo. Sababu kubwa ya kufariki kwa Gaddi Bullah ni ufadhili wake wa kutoa ini lake ili kuokoa maisha ya Dania aliyeathirika na pombe

kali sana. Kwa hatua ya mwanzo Dania alimpenda Gaddi na wakapendana lakini baadae alimsaliti na kurudiana na mpenzi wake wa zamani anayeitwa Jerry ambaye hakuwa na mapenzi ya dhati kwake.

Katika kusawiri kazi yake hiyo mwandishi katuonyesha baadhi ya dhamira mbalimbali na jinsi dhamira hizo zilivyoigusa jamii yetu na kuiacha jamii hiyo ikijiuliza maswali kadhaa. Miongoni mwa dhamira hizo ni pamoja na Mapenzi na ndoa, Suala la uongozi, Usaliti, Bidii katika kazi, Dharau na chuki , Migogoro, Nafasi ya Mwanamke katika jamii na nyingi nyenginezo.

Mwandishi Hussein Tuwa ametuonyesha dhamira zake hizo kupitia muhusika mkuu wake Gaddi Bullah, pamoja na wahusika wengine kama vile, Dania, Nunu, mama Mlole, Bi Hanuna, Nyambuja, Jerry, Dkt. Viran na Junior.

Mwandishi Hussein Tuwa katuonyesha ufadhili wa aina tofauti katika riwaya yake miongoni mwa ufadhili huo ni pamoja na ;

i. Ufadhili wa Gaddi Bullah kwa Dania .
ii. Ufadhili wa Mama Mlole kwa Gaddi Bullah na Dania.
iii. Ufadhili wa Gaddi Bullah kwa Juniour.
iv. Ufadhili wa Mama Mlole kwa wafanyakazi wake
v. Ufadhili wa Nuru na Boaz kwa Dania.
vi. Ufadhili wa daktari Virani kwa wateja wake.
vii. Ufadhili wa Gaddi Bullah kwa wazazi wa Dania.

Kwa ujumla riwaya ya *Mfadhili* ni riwaya ambayo inazungumzia umuhimu wa utendaji wema na kwamba mtu anaekufadhili basi anajenga imani na wema

kwako nae siku moja atatarajia kulipwa shukurani badala ya maovu. Pia mwandishi ametuoyesha mapenzi ya aina tofauti ndani ya riwaya yake hii. Riwaya ya *Mfadhili* imesheheni ufadhili kuanzia kiongozi wa kampuni Mama Mlole, Gaddi Bullah na wahusika wengine wengi. Kila muhusika alilitekeleza hili kutokana na umuhimu wake kwa jamii ya Tanzania. Kwa jumla tunasema kwamba Hussein Issa Tuwa amefanikiwa sana kuiakisi jamii ya kiafrika ikiwemo Tanzania katika riwaya yake hii.

## 4.4 Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya ya Mfadhili

Riwaya ya *Mfadhili* ni riwaya iliyosheheni wahusika wengi. Wahusika hawa wapo wahusika wanawake na pia wapo wahusika wanaume ambao wameshirikishwa vyema na mwandishi katika kufikisha maudhui aliyoyakusudia kwa jamii. Wahusika wanaume ni pamoja na Gaddi Bullah, Jerry, Boaz , Juniour na Daktari Virani. Wahusika wanawake ni pamoja na Dania, Mama Mlole, Nunu, Bi Hanuna, Nyambuja na wengineo.

Mtafiti kwa mujibu wa mada husika hajajihusisha na uchambuzi wa wahusika wanaume. Amejikita zaidi katika kujadili wahusika wanawake ingawa baadhi ya matendo ya wahusika wanaume yamehusishwa kwa kiasi katika uchambuzi. Mtafiti amebaini kuwa usawiri wa mwanamke umejitokeza katika hali mbili tofauti; hali chanya (njema / nzuri) kwa upande mmoja na hasi (mbaya) kwa upande wa pili. Mtafiti akihusisha nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika amebainisha taswira mbalimbali alizosawiriwa (alivyochorwa) mwanamke katika riwaya ya *Mfadhili*. Ili kukamilisha azima hii mtafiti aliongozwa na swali la kwanza la

msingi linalosema: Ni taswira zipi za mwanamke zilizobainishwa na kuchorwa katika riwaya ya *Mfadhili?* Kwa hakika swali hilo la msingi la kwanza limekwenda sambamba na lengo mahsusi la kwanza la utafiti lisemalo: Kubainisha taswira mbalimbali za mwanamke alivyochorwa katika riwaya ya *Mfadhili*.

Kwa kuzingatia lengo na swali la msingi la kwanza la utafiti huu, mtafiti amefafanua taswira mbalimbali za mwanamke zilivyobainishwa na kuchorwa katika riwaya ya *Mfadhili* kama ifuatavyo:-

### 4.4.1 Mwanamke kama Mshauri Mwema

Suala la kushauri ni zuri kwa kila binaadamu. Ushauri una umuhimu mkubwa katika maisha ya kila siku. Ushauri humjenga mtu, familia na hata taifa. Mara nyingi ushauri mzuri huweza kuijenga nafsi ya mtu na hata kusaidia katika maendeleo ya jamii yoyote. Katika riwaya hii mtafiti amebaini kwamba mwanamke ana uwezo mkubwa wa kushauri katika maisha, afya, mahusiano, kazi ,uwajibikaji, na hata maendeleo ya mtu mwengine. Utafiti huu umebaini jinsi kiongozi wa kampuni ya kutengeneza magari Bi Fausta (Mama Mlole) alivyotoa ushauri kwa Gaddi Bullah. Mama Mlole alitoa ushauri wake baada ya kupokea barua kali ya mashtaka na onyo aliyoiandika Gaddi Bullah dhidi ya Dania kutokana na kitendo chake cha kutokuwajibika na kumdharau bosi wake. Mwandishi ametuonyesha Mama Mlole akitoa ushauri mwema kwa Gaddi baada ya kupokea barua hiyo kama ifuatavyo:

> “Gaddi Bullah … Hali hii haitowafikisha wala kuwasaidia lolote. Kwa madhila mliyopitia wewe na Dania, ni nyinyi pekee ndio

> mtakaoweza kusaidiana. Mkiendelea hivi mtaharibu kazi. Kitengo chenu kitashindwa kutimiza malengo na majukumu yake na nyote mtaonekana hamfai hapa…“Mama Mlole alimshauri, kisha akaioneshea kidole ile barua iliyokuwa mezani mbele ya Gaddi, …Nikiiweka hii barua kenye faili binafsi la Dania kama nitakavyotakiwa kufanya, hili sula litabaki kwenye kumbukumbu kwa muda wote wa ajira yake, lakini mngelizungumza na kulimaliza hata kwa kumpa onyo la mdomo suala lote lingeisha hapo hapo, (uk. 92)

Vile vile suala la ushauri mwema pia limejitokeza tena kupitia rafiki wa karibu wa Dania yaani Nunu. Hali hii imejitokeza baada ya Dania kusalitiwa na Jerry alipoahidi kurudi kutoka Marekani ili kuja kufunga ndoa na Dania. Siku ilipowadia Jerry hakuonekana jambo ambalo lilimfanya Dania achanganyikiwe. Kuchanganyikiwa kwake kulifanya ajinyime hata kula. Tuangalie ushauri ambao aliutoa Nunu kwa Dania:

> Nunu alimwambia “Dania rafiki yangu…’ nakushauri umsahau kabisa Jerry. Angalia maisha yako na mwanao; huyo si wa kurudi tena .We mwenyewe unajua jinsi vijana wa hapa wanavyobadilika na kusahau nyumbani pindi wakifika nchi za nje hasa huko Marekani . Jerry amekufanyia unyama tu rafiki yangu. Mfute kabisa akilini mwako ! Nunu alimshauri rafiki yake kwa huzuni.” (uk, 87)

Dondoo hizi zimeonesha ni kwa kiasi gani mwanamke alivyoweza kuona mbele zaidi katika sula zima la kujenga maisha yaliyo bora zaidi . Ushauri huu ulifanyika kwa lengo la kumuokoa Dania katika janga la mapenzi ya uongo ya mpenzi wake Jerry. Dania alikuwa amejisahau na kuzidi kutumbukia katika giza nene na lenye hatari kubwa kwake.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, kupitia mihimili yake imetilia mkazo zaidi katika kumpa nafasi mwanamke kwa kuzingatia uwezo wake. Uwezo huo ni

pamoja kipawa kikubwa alichonacho cha kutowa ushauri juu ya mambo ya maisha na mipango ambayo inaweza kuleta mafanikio katika jamii zetu za kiafrika ikwemo jamii ya Tanzania. Mtafiti anaona kwamba suala la utoaji wa ushauri mwema lina nafasi yake na umuhimu wake. Kwa kweli ni jambo jema linalofaa kuendelezwa na wanawake kwa ajili ya maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

### 4.4.2 Mwanamke kama Muhusika Muwajibikaji Kazini (Bidii katika Kazi)

Katika kujenga jamii imara na yenye mafanikio, jambo muhimu kabisa ni uwajibikaji. Wanajamii wanapowajibika kupitia kazi mbalimbali husaidia sana kuchangia maendeleo ya taifa. Kupitia utafiti huu, mtafiti amebaini juhudi za Agnes akiwa kazini. Agnes alionyesha juhudi kubwa katika kuwakaribisha wageni wanaokuja na kusikiliza shida zao ili aweze kuwasaidia akiwa mapokezi ili kampuni yao isipate sifa mbaya ya watendaji wake. Agnes katika kumkaribisha mgeni wake ambae alikuwa ni Nunu wakati anamtafuta Gaddi ili ampe barua inayotoka kwa Dania anasema:-

> Karibu dada….nikusaidie tafadhali!’’Emmm, ndiyo! Habari yako ‘Yule binti alimjibu haraka huku akijiweka vizuri mbele ya lile dawati .”Nzuri tu dada mambo Safi ‘Nikusaidie nini dada yangu? Agnes alimuuliza kwa upole huku akiendelea kutabasamu! Eeem … Aaamm….Naomba kuonana na Bwana Bullah… Samahani sana lakini Gaddi si mfanyakazi tena wa kampuni hii. Ameacha kazi. ( uk 4 na 5)

Mtafiti kwa ujumla amebaini kuwa uwajibikaji katika sehemu za kazi ni jambo zuri na linaleta faraja kwa wageni na pia linalitangaza eneo husika., Sambamba na hilo mtafiti amebaini kwamba mwanamke ana nafasi kubwa katika kujiletea

maendeleo yake binafsi na hata taifa. Mwanamke pia ana mchango mkubwa wa kimawazo na kivitendo.

Vilevile mtafiti anaamini kuwa mashirikiano mazuri baina ya mwanamke na mwanamme ni jambo zuri katika kumuhamasisha mwanamke na mwanamme huyo kufanya kazi kwa pamoja. Hili tunaliona wakati Gaddi na Nunu walipoamua kushirikiana pamoja na kusahau tafauti zao baada ya Dania kusamehewa makosa yake na bosi wake Gaddi kama tulivyoona ushauri wa mama Mlole alioutoa kwa Gaddi na kuanzia hapo maendeleo makubwa yakajitokeza.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika na kwa kuzingatia mihimili yake kwa kina tumeona kwamba mwanamke ana mchango mkubwa katika maendeleo ya mataifa ya kiafrika na duniani kwa ujumla. Mtafiti amebaini kuwa uwajibikaji wa mwanamke umempa nafasi kuonekana na kutambulika kuwa anaweza kushika nafasi mbalimbali serikalini na hata katika taasisi za kimataifa. Mfano nchini Liberia uwajibikaji wa mwanamke umesaidia na kumpa hadhi kiongozi mkuu (raisi) wa serikali Mheshimiwa Helen Johnson Salef ambae aliitumikia nafasi yake vyema.

Kwa upande wa Tanzania tunao mfano wa viongozi hao wanawake ambao wameweza kushika nafasi kubwa duniani mfano Mh. Asha Rose Migiro aliwahi kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN). Pia amewahi kuwa Waziri wa Katiba na Sheria., Sambamba na hilo amewahi pia kuwa Mkuu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Halikadhalika Mheshimiwa Anna Makinda amewahi kuwa Spika wa Bunge la Tanzania na kwa sasa Mheshimiwa Makamo wa raisi wa Tanzania ni Mh. Samia Suluhu Hassan, pamoja na mawaziri, wabunge, wawakilishi na madiwani wengineo wanawake kwa Tanzania. Kutokana na hayo tunaweza kusema kwamba mwanamke anawajibika na anao uwezo mkubwa sana wa kushika nafasi za uongozi ndani na nje ya jamii yake.

### 4.4.3 Mwanamke kama Muhusika mwenye Mapenzi ya Dhati

Mapenzi ya dhati ni kitu adimu sana. Suala hili limo ndani ya nafsi ya mtu na halionekani. Misingi mikubwa inayobainisha mapenzi hayo ya dhati ni wanajamii wenyewe kuimarisha masikilizano, uaminifu, mashirikiano, heshima, matunzo, imani, kuvumiliana, kushibana, kusameheana, uwazi na ukweli, usawa wa haki na mengineyo. Kwa wanaopendana au hata katika ndoa mara nyingi usaliti huwa sumu na adui mkubwa wa mapenzi ya kweli. Mwandishi Hussein Issa Tuwa amelizungumzia suala hili katika riwaya hii ya *Mfadhili* kwa kutuonyesha wahusika mbalimbali ingawa wapo baadhi ya wahusika ambao mwandishi kawachora kuonyesha kinyume chake. Mtafiti amebaini mapenzi ya dhati yakijitokeza katika sehemu mbalimbali ndani ya riwaya hii mfano; (uk 7, 17, 55, 86, 98, 99, 123, 125, 144, 145, 146).

Katika mifano ya kurasa hizo hapo juu mtafiti amewabaini wanawake kadhaa wakionyesha mapenzi ya dhati., Miongoni mwa wana wanawake hao ni mama Mlole aliyeonesha mapenzi ya dhati kwa wafanyakazi wake, bi Hanuna kwa ndugu yake Gaddi, Nunu kwa Boaz, Nunu kwa rafiki yake Dania, Dania kwa Jerry.

Wanawake wengine waliioonesha mapenzi ya dhati ni Mama Dania kwa mtoto wake Dania, bi Hanuna kwa Dania, Dania kwa Juniour na wengineo. Tuangalie uhusiano wa Bi Hanuna kwa Dania na mapenzi ya dhati kwa wote kabla mapenzi hayo hayajaingiliwa na Jerry ambae alichafua kila kitu baadae. Mwandishi anasema:

> … Bi Hanuna alimfuata Dania jikoni alipokuwa akiosha vyombo na kumwita " Dania…'' Dania aligeuka na kumtazama kwa macho ya kuuliza huku akiwa ameshika sahani mkono mmoja na sabuni mkono mwengine.'Ahsante wifi yangu..''Bi Hanuna alimwambia huku akimsogelea taratibu pale alipokuwa amesimama…na huku akitabasamu…Kwa kunirudishia kaka yangu ninayemjuwa, Dania. Kwani kwa hakika Gaddi alibadilika kabisa lakini baada ya kukutana na wewe amerudia uchangamfu amejitokeza….Bi Hanuna… ni mimi ndiye natakiwa nimshukuru Gaddi kwa kunifikisha hapa ….. ni mimi ndiye niliyerudishiwa utu na heshima yangu kwa kuwa na Gaddi, na hata kitokee nini, sitomuacha Gaddi nakuahidi hilo…Bi Hanuna alimtazama yule binti kwa tabasamu pana. " Sina shaka kabisa na hilo wifi……sina shaka kabisa.(uk . 98)

Mtafiti amebaini mapenzi mengine ya dhati kabisa ya Bi Hanuna kwa mdogo wake Gaddi. Mapenzi hayo aliyaonesha pale Gaddi Bullah aliposalitiwa tena mara ya pili ambapo mara hii alionana na Jerry ana kwa ana chumbani kwa Dania jambo ambalo lilisabisha purukushani kubwa kati yao. baada ya hapo Gaddi alirudi nyumbani na kumuhadithia dada yake kisa na mikasa yote iliyomfika. Mtafiti aliona hisia za wazi za mapenzi yaliyojaa huruma ya Bi Hanuna kwa mdogo wake. , Mwandishi anasema:

> Bi Hanuna nae alilia na mdogo wake. Ulikuwa ni msiba mkubwa kwake. Huyu ni ndugu yake pekee hapa duniani na ni mtu mkarimu sana. Sasa kwa nini anapatwa na mabaya tu hapa duniani? "Nyamaza mdogo wangu nyamaza! Wala usilie … hao wote waliokufanyia hivi ni watu dhalili sana kwako na hawastahili machozi yako. Ni vile tu hawakuwa stahili yako ndio maana imekuwa hivyo….naamini utapata tu mwanamke

> mwengine atakaye…” Hapana Da Hanuna! Hapana. Mimi tena… Sina haja ya mwanamke tena! Haya…. yananitosha.” (uk. 125)

Kwa hakika mapenzi ya dhati yanahitaji wale wanaopendana wawe wakweli kwani hakuna mkamilifu na inapotokea kukosana basi watu wavumiliane na kusahau yaliyopita. Mtafiti ameyabaini haya kupitia Mama Mlole kwa wafanyakazi wake, pia Dania kwa Gaddi.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kupitia mihimili yake inatetea umuhimu wa kuwa na mapenzi ya dhati ili kuweza kujenga jamii iliyo bora na kuepukana na ubaguzi na aina zote za udhalilishaji. Nadharia hii ya Ufeministi wa Kiafrika inatilia mkazo mwanamke na mwanamme kuwa na haki na usawa katika masuala mbalimbali ya kijamii yakiwemo mapenzi ya dhati baina yao. Mtafiti anaunga mkono kuwa mapenzi ya dhati yanajenga familia bora yenye umoja na mashirikiano yaliyo imara ambayo yanaleta tija katika jamii zetu. Jamii zote za Kiafrika ikwemo jamii ya Watanzania husisitizwa kulizingatia hilo kwa kuwa ni miongoni mwa misingi muhimu ya maisha ya kila siku. Jambo hili ni la lazima kwa kila binaadamu anayehitaji kutambuliwa na kuthamiwa utu wake.

### 4.4.4 Mwanamke kama Chombo cha Starehe kwa Mwanamme

Wanawake wengi katika jamii zetu wamekuwa wakifanya ngono na kutumika kama chombo cha starehe kwa wanaume. Jambo hili sio geni tena. Limekuwa ni mashururi sana mijini na limeenea hata vijijini. Uhusiano baina ya mwanamke na mwanamme limekuwa jambo la kawaida sana katika jamii zetu. Baadhi ya

wanawake huitoa miili yao bure au kwa ujira hafifu kwa lengo la kuwastarehesha wanaume. Vijana wengi wanadai kwamba kabla ya ndoa ni vyema kuishi na mpenzi kwanza ili kujenga mazoea na kupimana tabia. Mambo kama haya si halali kwa dini zote na yanavunja maadili katika jamii zetu. Mambo kama haya yanafanyika katika nchi nyingi duniani Afrika na hata Tanzania . Jambo hili linaweza kupelekea maambukizo ya maradhi yakiwemo ya UKIMWI.

Mwandishi amelifafanua hilo kupitia uhusiano wa kimapenzi baina ya Dania na Jerry ambapo Jerry alimtumilia Dania katika starehe tu bila malengo yoyote na Dania kwa maksudi liamua kumstarehesha Jerry kimwili kila alipomuhitaji. Mwandishi anayafafanua maelezo ya Mama Mlole ambayo alikuwa anamueleza Gaddi Bullah kuhusu uhusiano wa Dania na Jerry kama ifuatavyo:

> " Naamini hiki kilikuwa kipindi kilichojaa furaha sana kwao . Mimi binafsi nilishakutana nao mara kadhaa mjini katika siku za mwisho wa wiki wakiwa katika furaha ya ujana. Mara mbili walinialika kwa chakula cha jioni kwenye sehemu nzuri za vyakula hapa jijini, kutokana na ukaribu uliokuwapo baina yangu na Dania. Walikuwa wakitoka kila mwisho wa wiki kwenda kwenye kumbi kadhaa za starehe na rafiki zao mbalimbali, wakati mwengine walienda pwani na kurudi nyumbani kwa mmoja kati yao… Mwaka huo huo Dania akabeba mimba." (uk 82)

Pia Dania hakuishia hapo tu katika mahusiano yake na Jerry lakini aliona bora atafute mwanamme mwengine ambae atamtoa majonzi baada ya kusalitiwa na Jerry na ndipo alipoanza mahusiano na Gaddi. Dania alimstarehesha Gaddi wakawa wapenzi:

> " Gaddi itakuwaje iwapo.. iwapo…yatanikuta tena yaliyonikuta kwa Jerry? Dania aliuliza kwa wasiwasi mkubwa huku akilengwa

> na machozi. " Hayawezi kukukuta tena mambo kama yale kwa sababu mimi sio Jerry mimi nakupenda kwa dhati"
> "Oh Gaddi! Najua mpenzi, lakini .. ah! Naona kama nina mkosi na ndoa …Naogopa!
> "Hapana. Usiogope Dania naamini huu ni uamuzi wa busara kwetu sote…Alimkumbatia kwa upendo yule mwanamme aliyetokea kumpenda kwa moyo wake wote.
> "Oooh, Gaddi! Nakupenda sana Gaddi Bullah! Na nashukuru……… kwa kunipa nafasi nyengine ya kupenda katika maisha yangu…Dania, Dania, Dania,..Ahsante wewe mpenzi wangu …Gaddi alimjibu kwa huba huku akimpapasa kwa upendo mkubwa..." ( uk. 99).

Mtafiti pia amebaini kuwa bado mwandishi kawachora wanawake wengine katika riwaya hii kama chombo cha starehe, hili limejitokeza kati ya Nunu na Boaz ( uk. 17) Pia katika mahusiano ya Nyambuja (mke wa Gaddi) (uk. 66) Kutokana na dondoo hizo hapo juu imeonesha wazi ni kwa jinsi gani mwanamke ametumika kama chombo cha starehe katika mapenzi. Mtafiti amegundua bado tabia ya kumtumia mwanamke kama chombo cha starehe ipo katika jamii zetu. Ukweli ni kwamba tabia hii sio njema kwa mwanamke na hata mwanamme, ni vyema tukaachana na tabia hii ya kumuona mwanamke kama bidhaa. Kumfanya mwanamke kama bidhaa ni kumvunjia hadhi na kumpunguzia thamani yake.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kupitia mihimili yake imesisitiza na kuwakumbusha wanawake kuwa wao sio bidhaa au chombo tu cha kumfurahisha mwanamme. Wanawake ni binaadamu na wana haki stahiki kwa kuzingatia hali zao. Mtafiti anawataka wanawake waachane na tabia ya kujiuza kama bidhaa ya kumstarehesha mwanamme pasipo stahiki. Pia wanawake waachane

na tabia ya kujidhalilisha kwa matashi binafsi isipokuwa haki ya kustarehe kihalali ambayo iko kwa waume zao tu na kwa wakati muwafaka.

### 4.4.5 Mwanamke kama Muhusika Mlevi

Ulevi bado ni miongoni mwa tabia mbaya ambayo baadhi ya watu hawajali kabisa. Ulevi katika jamii yoyote ile una athari kubwa na huchangia katika kurejesha nyuma hali ya mtu mwenyewe, familia na hata taifa kwa ujumla. Hii ni kutokana na wale wanaoendeleza ulevi hushindwa kutimiza majukumu yao ya kikazi ipasavyo. Pia ufanisi katika kazi hukosekana kwa sababu watendaji ni walevi, na hii hutokea kwa sababu akili zao huwa haziko timamu. Utafiti huu umebaini baadhi ya wahusika wakiwemo wanawake wakijiingiza moja kwa moja katika ulevi. Wamefanya hivyo huku wakiamini kuwa hilo ndilo suluhisho la matatizo bila kujua kuwa ulevi wa pombe una athari kubwa katika mwili wa mwanaadamu. Hali hii imejitokeza kupita muhusika Dania ambae amekuwa akinywa pombe kali kupindukia akiamini kuwa pombe itamtuliza akili kwa hali aliyonayo. Ili kushadidia hoja hii mwandishi ametuonesha ukweli wa madai haya kupitia mama Mlole akimsimulia Gaddi kama ifuatavyo;

> “ Jerry alimchanganya sana akili yake na aliuumiza sana moyo wake .Alianza kunywa pombe kali tena kwa wingi!”….Akawa mlevi kupindukia, hatuna tulichoweza kufanya kumzuia kunywa pombe kali., Si wazazi wake. si rafiki zake, wala si wa sisi hapa ofisini..Dania alishindikana!(uk. 87na 88 ).

Mwandishi pia ametuonesha athari hiyo ya pombe kali aliyokuwa akitumia Dania iliyothibitishwa na daktari Verani ikiwa ni pamoja na kuharibika ini (uk. 105)

Mtafiti kupita dondoo hiyo anatoa tahadhari kubwa kwa wale wenye tabia ya kutumia ulevi. Mtafiti anawasihi watu wote wenye tabia ya kutumia ulevi kwamba ni vyema waache tabia hiyo kwani madhara yake ni makubwa. Nadharia ya Ufeministi ya Kiafrika kupitia mihimili yake inaliangalia suala la ulevi kuwa miongoni mwa matendo maovu ambapo wanawake wa kiafrika ni miongoni mwa waathirika. Kwa muktadha huu na kupitia mihimili ya nadharia hii mtafiti anawashauri wanawake na hata wanaume waachane na tabia ya ulevi. Anatoa ushauri huu kuku akiamini kwamba ulevi sio suluhisho la kuondoa matatizo yetu. Kwa kubaki na tabia ya ulevis tutaliingiza taifa katika hasara kubwa. Taifa linapoteza nguvu kazi ya vijana wengi wakiwemo wanawake. Tuelewe kwamba ulevi huchangia kwa asilimia kubwa kuathiri uchumi na kipato cha wanajamii wenyewe.

### 4.4.6 Mwanamke kama Mtu mwenye Busara na Hekima

Busara na hekima ni vitu muhimu kwa binaadamu. Mara nyingi nyenzo hizi hutumika katika kutatua migongano baina ya mtu au watu. Pia busara na hekima hutumiwa na husaidia sana katika kutatua matatizo pale yanapotokea ndani ya jamii zetu. Vitu hivi ni adimu sana na si watu wote waliojaaliwa kuwa navyo. Tunu hizi kwa nadra huweza kujitokeza katika baadhi ya mioyo ya wanawake na hata wanaume.

Katika kulitafiti hilo mtafiti amebaini usawiri wa mwanamke katika suala zima la kumuhusisha kuwa na busara na hekima kwa wanaadamu wenzake. Mtafiti amelibaini hili kupitia muhusika Mama Mlole ambae alijitahidi sana

kutumia busara na hekima kwa wafanyakazi wake. Mama huyu alitumia hekima na busara zake katika kujitahidi uwaunganisha pamoja Gaddi na Dania napale walipokuwa katika mgogoro wa kikazi. Tuangalie hekima na busara aliyoitumia Mama Mlole kwa Dania wakati Dania alipojiingiza katika ulevi na kutohudhuria kazini:

> “ Ndio … kwa hatua aliyofikia ilibidi aachishwe kazi, lakini kwa kumsaidia, nikiwa kama Afisa wa Utumishiwa kampuni nilipendekeza apewe likizo bila malipo kwa muda wote aliotakiwa nje ya nchi kwenye matibabu. Nilifanya kazi ya ziada kuushawishi uongozi wa kampuni juu ya hili, kama jinsi nilivyofanya kazi ya ziada kulishawishi lile jopo la wakaguzi kule Arusha kukupa wewe nafasi nyengine katika kampuni badala ya kukufukuza kazi…. lakini nilifanikiwa Mama Mlole alisema kwa msisitizo huku akimtazama usoni Gaddi” (uk 88).

Vilevile mwandishi amezionesha busara na hekima kupitia muhusika Nunu alipokuwa akimnasihi Bi Hanuna ili aipokee barua ya Gaddi Bullah ( uk 27 na 29) pia busara na hekima zimejitokeza tena katika (uk. 32, 70, 89 , 129)

Kwa upande wa Nadharia ya Ufeministi wa `Kiafrika, mtafiti amekuwa akisisitiza na kuunga mkono busara kubwa na hekima aliyonayo mwanamke kazini na hata katika jamii. Busara na hekima ya mwanamke inajenga mapenzi, umoja na mshikamano. Kwa kuzingatia hilo mtafiti anaamini kwamba wanawake wenye busara ni nguzo na ni mfano wa kuigwa kwa wenzao ambao hasira, chuki, hamaki, ugomvi, unachukua nafasi katika maisha yao.

### 4.4.7 Mwanamke kama Msaliti

Usaliti ni hali ambayo inajitokeza pale ambapo mmoja baina ya watu walokubaliana kitu au jambo anamgeuka mwenzake. Mmoja huvunja ahadi

waliyoipanga na kufanya kinyume chake. Usaliti ni kitu kibaya na unaweza ukamuathiri mtu yoyote kimwili na hata kisaikolojia. Wakati mwengine usaliti unaweza kusababisha hata kifo miongoni mwa wanajamii.

Katika kulithibitisha hilo mtafiti amebaini makosa makubwa ambayo yamefanywa na wahusika wanawake na kusababisha migogoro ndani ya jamii zetu. Katika hali hiyo mtafiti amegundua tatizo hilo kupitia wahusika mbalimbali. Mwandishi alitoa mfano wa Nyambuja alivyomsaliti Gaddi wakati bado Gaddi Bullah yupo katika penzi zito kwake. Katika kulithbitisha hilo mwandishi anasema kupitia barua ambayo Nyambuja alimpelekea mumewe:

> Kwako Gaddi, Samahani sana kwa yote yaliyotokea, na pia kwa huu uamuzi wangu niloamua kuuchukua. Naomba usinichukie na usinielewe vibaya. Mimi nimeamua kuondoka na kutoka kabisa katika maisha yako… nimefanya hivi ili kutoendelea kuwa mke mwenye upendo kwako. Gaddi nimependana na mtu mwengine, na nimekuwa nikisaliti ndoa yetu kwa muda mrefu….. nimeamua kuondoka.
> Naomba uelewe kwamba huu ni uamuzi wangu mwenyewe kwa hivyo niko tayari kwa lolote ambalo wewe unaona linafaa ili kila mmoja aendelee na maisha yake kwa amani. ….. Nakutakia maisha mema katika siku zako zilizobakia ukiwa mbali nami.
>
> Aliyekupenda kwa dhati,
>
> Nyambuja. (uk. 65)

Vile vile usaliti mwengine ambao mtafiti ameubaini ni ule alioufaya Dania kwa Gaddi. Hii ilitokea wakati Jerry alipojitokeza kwa mara nyengine kumpenda Dania pamoja na ahadi kali alizoziweka Dania kwamba hatomsaliti Giddi na hatorejea trna kwa Jerry. Dania alijikuta akirudiana na Jerry, huku akimsaliti Giddi. Mwandishi anasema:

> “ ..Ndiyo mimi na Dania tumekaa na kuamua kwamba pamoja na matatizo yote yaliyotokea tuliona ni vyema tukawa pamoja

> kwa manufaa ya mwenetu…Tumeamua ndoa kwa ndoa mwenetu.. kwa hivyo bwana wee kaa pembeni sasa muda kwa Dania umekwisha!..akimgeukia Dania, .. Dania hivi ndivyo ulivyoamua kunijulisha juu ya jambo hili? Yaani baaada ya yote umeshindwa hata kunijulisha kistaarabu na kuamua kunisaliti namna hii? Yaani nasalitiwa kwa mara ya pili mimi? Dania macho yalimtoka … lakini wewe ndo ulokuja nyumbani saa hizi lakini nilipanga kukueleza.”( uk 120 na 121).

Dondoo hizi zinaonyesha wazi jinsi baadhi ya wanawake wanavyoweza kuwasaliti wapenzi wao. Baadhi yao huzisaliti hata ndoa zao bila ya kufikiri nini athari ya usaliti waufanyao. Mtafiti anaamini kwamba hali hii ni aibu kubwa na inaweza kuleta migogoro mikubwa miongoni mwa wanajamii.

Kwa kutumia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kupitia mihimili yake ambayo inamjali na kmtetea mwanamke, mtafiti anaona kwamba suala la usaliti ni jambo baya na linaweza kuleta athari kwa wanajamii. Sambamba na hilo nadharia hii inazingatia usawa miongoni mwa wanajamii. Kitendo cha usaliti kwa mwanamke kinamvua hadhi mwanamke na kuonekana mtu asiye na maadili na mafunzo mema. Hivyo nadharia ya ufeministi wa kiafrika inapingana na hali na tabia hiyo kuwa haina budi ipigwe vita kabisa na kwamba haifai kuigwa.

### 4.4.8 Mwanamke kama Kiongozi Bora

Kwa hakika uongozi sio kitu cha mchezo. Mtu anaeongoza watu anatakiwa awe mvumilivu na awe tayari kuwaongoza wenzake kwa hali yoyote. Pia kama kiongozi anatakiwa ujuwe kwamba anawaongoza watu wenye tabia tafauti hivyo awe tayari kukabiliana na matokeo yoyote. Mtafiti amebaini kuwa suala la uongozi linaweza kujitokeza kwa jinsi zote mwanamke na mwanamme pia.

Jambo hili limejitokeza katika riwaya ya *Mfadhili* pale mwandishi alipomsawiri Mama Mlole kama Afisa wa Utumishi wa Kampuni moja Dar es Salaam. Mama Mlole alikuwa ni mtu hodari asiyeyumba na aliyejali zaidi ubinaadamu kuliko kazi. Mama huyu ndie aliyewaunganisha Dania na Gaddi wakiwa katika ugomvi mkubwa. Sambamba na hilo Mama Mlole ndiye aliyeishawishi bodi kule Arusha na pia kuushauri uongozi Dar es Salaam kuwarudisha kazini Gaddi na Dania badala ya kufukuzwa kazi. Tuangalie Mama Mlole alivyotumia nafasi yake ya Uongozi kukasimu madaraka. Mwandishi anasema:

> Sasa mwenyewe nimerudi "Dania alidakia kwa hasira. Gaddi alizidi kumshangaa. Mama Mlole alimgeukia Dania. "Hakuna mwenyewe kwenye vyeo vya kampuni, Dania wewe ndio leo unaripoti baada ya kuwa nje ya kazi kwa muda mrefu, ilitakiwa uripoti kwangu kwanza kabla kwenda huko ulikodhani ndiko kwenye ofisi yako…..Gaddi amepewa uhamisho kutoka Arusha kuja hapa, …"Wewe utaendelea kufanya kazi kwenye kitengo hicho hicho, ila sasa utakuwa chini ya Gaddi Bullah. Yeye ndie mkuu mpya wa kitengo na wewe utakuwa msaidizi wake." Hivyo ndivyo tulivyoamua kama uongozi wa kampuni." Mama Mlole alimjibu na kwa jibu lile ilkuwa wazi kuwa ule mjadala ulikuwa umekwisha." ( uk .73 na 74).

Ukurasa mwengine pia unaozungumzia mwanamke kama kiongozi bora ni (uk. 79 na 88). Suala la uongozi kwa wanawake sasa si suala geni. Wapo viongozi wengi sasa duniani ambao ni wanawake. Mfano mzuri wa viongozi wanawake duniani ni Malkia Elizabeth wa Uengereza. Katika bara la Afrika pia wapo viongozi wengi wakuu wanawake. Tanzania pia tunao viongozi wakuu wanawake. Mfano mzuri wawanawake hao ni Mh. Samia Suluhu Hassan ambae ni Makamo wa Rais wa Tanzania wa awamu ya tano. Tunao pia mawaziri wanawake katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Kiongozi wa Bunge la kumi, bi Anna Makinda

alikuwa mwanamke. Pia wapo wajumbe wa baraza la, wawakilishi, wabunge, wakuu wa Wilaya, wakuu wa Mikoa ambao ni wanawake.

Kwa kutumia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kupitia muhimili wake wa usawa kwa wote na kuondoa mfume dume mtafiti anaunga mkono kwamba ule wakati wa mwanamme kumdhalilisha mwanamke kwa kumuweka ndani tu na kuona mwanamke hawezi kufanya kazi ila kazi za ndani umekwisha. Sasa wanawake wanaweza kufanya mengi wanapowezeshwa na mara nyengine bila kuwezeshwa. Inatubidi tuondokane na mawazo potofu ya ule mfumo dume kwamba wanawake ni watu wa kukaa ndani tu na kuwastarehesha mabwana. Kitendo cha wanawake kufanya kazi ni hatua moja ya wanawake hao kujikomboa.

### 4.4.9 Mwanamke kama Rafiki wa kweli na Mwenye kutimiza Ahadi

Rafiki mzuri huonekana katika kipindi cha shida. mtafiti amebaini kwamba ili urafiki wa kweli ushamiri baina ya watu basi ni vyema .watu wajenge makubaliano baina yao, washibane na kila mmoja awe tayari kujitoa muhanga kwa ajili ya mwenzake. Katika utafiti huu tumeona marafiki wengi lakini urafiki hasa wa kushibana ni ule aliouonyesha mwadishi ambao ulikuwa baina ya wanawake wawili ambao ni kati ya Nunu na Dania.

Nunu kama mwandishi alivyomsawiri, alionekana kumpenda Dania na alikuwa tayari muda wote kumsaidia na kumshauri katika kipindi ama cha furaha au cha shida. Tatizo la Dania lilikuwa tatizo la Nunu. Nunu alimuahidi Dania

kumsaidia kupelekea barua ya kuomba msamaha kwa Gaddi. Dania wakati huo alikuwa katika hali mbaya sana kiafya. Alikuwa karibu sana na kukata roho baada ya kukosa mtu wa kumfadhili ini. Kuingizwa ini jipya ilikuwa ndio njia pekee ya kuponya maisha yake. Nunu alijitahidi kwa uwezo wake wote kuhakikisha barua ile inamfika Gaddi kabla Dania hajakata roho. Tuangalie Nunu anavyolalamika baada ya kukosa barua ile kufika kwa Gaddi.

> “ Eeeh, jamani sasa hili balaa gani hili! Nilimuahidi kuwa nitahakikisha kuwa Gaddi anapatikana na sasa nimeshidwa kutimiza ahadi hii muhimu sana kwa rafiki yangu!” Nunu alilalama na kuanza kulia tena”(uk.19).

Tuangalie pia ushauri mzuri alioutoa Nunu kwa rafiki yake Dania wakati Dania alipoamua kumsaliti Gaddi na kurudiana na Jerry ambae hakuwa mtu mzuri kwake. Mwandishi amemsawiri rafiki huyu kuwa si rafiki tu bali mshauri na ndugu mwema. Dania alikuwa mkaidi, hakuwa hakufuata ushauri wa rafiki yake. Aliendelea kushikilia msimamo wake. Mwandishi anasimulia malumbano ya Nunu kwa rafikiye Dania kama ifuatavyo:

> “Una wazimu wewe! Tena huna akili kabisa,! Nunu alimwambia huku akitupa mikono yake hewani kwa hasira .. Lakini Nunu..“Huwezi kurudiana na Jerry, Dania! Hivi umesahau mambo aliyokufanyia? Umesahau jinsi alivyotuhangaisha sisi wakati yeye anaponda maraha huko? Leo unanambia unarudiana naye? Haya Gaddi utampeleka wapi?...Gaddi nilimpenda.. Ulimpenda… yaani kama past tense? Sasa Nunu rafiki yangu mbona hutaki kunisikiliza lakini? Nisikilize upuuzi huu? Hebu amka mwanadada Gaddi anakupenda kwa dhati Gaddi amekuwa na wewe kwenye matatizo na raha. Hivi Gaddi unafikiri anastahiki kufanyiwa hivi kweli? ( uk. 114).

Tukiiangalia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kupitia mihimili yake inahimiza umoja na mshikamano pamoja na upendo wa kweli miongoni mwa wanajamii.

Mtafiti amebaini kwamba kwa udhati kabisa Nunu ni miongoni mwa wanawake wenye urafiki wa kweli. Nunu pamoja na kutofautiana kimawazo na rafiki yake Dania bado hakuacha kumpa nasaha na ushauri mwema. Nadharia hii inawaongoza na kuwatanabahisha wanajamii na hasa wanawake ambao hawana ukweli kwamba kufanya hivyo ni kujiondolea hadhi. Wanawake wa aina hoyo wanatakiwa wabadilike ili waweze kujenga jamii yenye ubora kwa faida ya wanajamii na taifa kwa ujumla.

### 4.4.10 Mwanamke kama Mtu Msuluhishi

Amani na upendo ni kitu muhimu sana katika jamii zetu. Suluhu inahitajika pale watu wanapotofautiana kimawazo na hii inaweza kutokea baina ya mtu na mtu au mtu na kundi la watu wengine. Katika riwaya hii mwandishi amewasawiri Mama Mlole na Nunu kama wasuluhishi katika riwaya hii. Kwanza tumeona juhudi za Mama Mlole alipojitahidi kuwaunganisha Gaddi na Dania pale walipokosana kutoka na Dania kufanya uzembe na kukataa amri za bosi wake Gaddi. Jambo hili Mama Mlole kuliingilia kati kumnusuru Dania na kumbukumbu mbaya katika faili lake. Kwa hivyo Mama Mlole kama kiongozi alifafaya suluhu hiyo. Tuangalie dondoo ifuatayo:

> Gaddi Bullah … Hali hii haitowafikisha wala kuwasaidia lolote. Kwa madhila mliyopitia wewe na Dania, ni nyinyi pekee ndio mtakaoweza kusaidiana. Mkiendelea hivi mtaharibu kazi. Kitengo chenu kitashindwa kutimiza malengo na majukumu yake na nyote mtaonekana hamfai hapa.. “Mama Mlole alimshauri,kisha akaioneshea kidole ile barua iliyokuwa mezani mbele ya Gaddi, ..Nikiiweka hii barua kenye faili binafsi la Dania kama nitakavyotakiwa kufanya, hili suala litabaki kwenye kumbukumbu kwa muda wote wa ajira yake, lakini mngelizungumza na kulimaliza hata kwa kumpa onyo la mdomo suala lote lingeisha hapo hapo uk. 92).Baada ya maelezo hayo ya Mama Mlole siku

> ya pili tu Gaddi alimuita Dania pale ofisini na kumaliza tofauti zao. Mwandishi anasema:
> Kwa mshangao mkubwa alimshuhudia Gadi akiichukua ile barua yake ya maelezo, ile barua kali aliyo mwandikia hapo awali na nakala ya barua ile iliyokwenda kwa Mama Mlole na kuzipanga pamoja. Kisha alitoa kiberiti cha gesi na kuzitia moto zote palepale ofisini. Macho yalimtoka Dania na kumtazama kwa mshangao mkubwa kabisa. Hilo suala limeisha kama barua hizi zinavyomalizwa na huu moto! .. Oooh, Bosi! Ahsante sana bosi!" Dania alisema kwa hamasa huku akiinuka na kumpa mkono Gaddi ambaye nae aliinuka na kuupokea ule mkono huku akicheka (uk 94 na 95).

Vilevile Mwandishi kwa upande mwengine amemsawiri Nuru kuwa msuluhishi kutokana na ugomvi uliokuwepo kati ya Dania na Bi Hanuna, ugomvi hapo awali na Bi Hanuna hakuwa tayari kuonana na Dania lakini Nunu na Boaz walimteka nyara kwenye gari na kumpeleka kwa Dania kwa nguvu kwenda kujionea mwenyewe hali ya Dania ambae aliomba radhi katika ile barua. Dania alikuwa hali mbaya sana pale kitandani, Bi Hanuna alibaki akimtazama yule mwanamke ambae hapo awali alikuwa mrembo na wa kuvutia sana leo anaonekana mzee aliyechakaa.

> " … Hakujuwa iwapo aendelee kumchukia au la au yeye alie….. Bi Hanuna alimtazama yule kiumbe na chozi la huruma likamdondoka na badala ya hasira ikaja imani" ( uk.53 na 54).

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inasisitiza maelewano na mshikamano miongoni mwa wanawake na wanajamii na inakataza fitna na ugomvi. Mtafiti anaamini kwamba endapo jamii itaepukana na ugomvi usio wa lazima basi maendeleo ndani ya jamii hiyo yatapatikana. Pia hapa tunapata angalizo kwamba chuki za mtu mmoja dhidi ya mwengine sio kitu kizuri. Kwa hivyo wanajamii wanatakiwa wawe waangalifu sana na endapo itatokea kutokuwepo maelewano baina ya watu njia pekee ya kuondosha suitafahamu hiyo ni kfanya suluhu.

### 4.4.11 Mwanamke Kama Mtu asiyetaka Ushauri

Ushauri mwema ni jambo zuri katika maisha ya kila siku ya mwanadamu. Ushauri unaleta mabadiliko na maendeleo. Ushauri unajenga heshima na nidhamu. Ushauri huleta upendo baina ya mtoaji na mpokeaji. Ushauri mwema unapokataliwa athari zake zinakuwa kubwa na kumfikisha pabaya sana mshauriwa. Mwandishi hakulifumbia macho suala hili. Mwandishi ametuonyesha jinsi alivyomsawiri Dania kupata mashaka na kufikia pabaya baada ya kukataa ushauri aliopewa na rafiki yake wa karibu; Nunu. Nunu alimtaka Dania aachane na kufanya tena uhusiano wa kimapenzi na Jerry. Kukataa ushauri kilimfanya Dania amalizie vibaya sana. Mtafiti amebaini kwamba mara nyingi mtu anayekataa ushauri mzuri hana mwisho mwema. Tuangalie mfano mzuri wa Dania aliekataa ushauri wa Nunu kuhusu mahusiano yake na Jerry. Mwandishi anafafanua kwa kusema:

> Wakati mwengine ni salama zaidi kudharau jinsi moyo wako unavyotaka,…..kusikilizaushauri wa wanaokupenda! Hivi kwa nini huwezi kuelewa jambo hilo wewe? …. Umenasa sio ? .. Dania wewe ni rafiki yangu. Lakini kwa hili, nakuambia waziwazi kuwa siko na wewe. Kama hutasikia ushauri wangu basi kaa ukijua kuwa mimi siko upande wako!Naomba uondoke!”.. Unanifukuza Nunu? ( uk.116).

Pamoja na maelezo makali ya Nunu lakini Dania aliendelea kushikilia msimamo wake. Nunu kwa upande wake hakusita kumshauri Dania kwenda kumtaka msamaha Gaddi ili ili aweze kurejeana nae baada ya kumfumania akiwa na Jerry. Hata hivyo Dania aliendelea kukataa ushauri wa rafiki yake Nunu. Mwandishi anatuelezea ushauri alioutoa Nunu kwa Dania kama ifuatavyo:

> “Lakini bado hujachelewa Dania! Bado una nafasi ya kurudi kwa Gaddi sasa na kumtaka radhi … naamini atakusamehe. Ni bora nusu ya shari kuliko shari kamili!”
> “Hapana Nunu nimeshaharibu kwa Gaddi sasa sina budi ila kumng’ang’ania Jerry tu vinginevyo nitakosa kote”( uk. 127).

Pia katika hali hiyo hiyo Dania alishauriwa na Nunu, Wazazi wake, na hata watu wa ofisni mwake akiwemo bosi wake Mama Mlole aachane na pombe kali. wakati ule aliposalitiwa na Jerry kutokuja katika ndoa yao lakini Dania hakukubali akiamini pombe ndio suluhisho la matatizo yake lakini mwisho hali ilikuwa mbaya na wazazi wake wakalazimika kumpeleka Afrika ya Kusini kwa matibabu zaidi (uk. 88).

Kwa kutumia nadharia ya Ufeministi ya Kiafrika, mtafiti anaunga mkono nadharia hii kwamba ushauri na maelekezo ambayo watu wanapewa wanawake marafiki, wazee, au watu wa karibu wakati mtu / watu wakitokewa na matatizo basi ni vyema mtu aangalie ukweli huo kabla ya kutoa maamuzi na kwamba kukataa ushauri wa wenzake mtu mwisho wake ni mbaya, ushauri unafanyika ndani ya familia, kazini, katika jamii, na haijalishi ushauri huo umetolewa na jinsi gani. Mtafiti amebaini kwamba ushauri mwema husaidia katika maendeleo na tusiwadharau wanawake tukaona kwamba wao ni watu duni na hawana ushauri wowote dhana hiyo ni potofu kwani ushauri wao ni mzuri na unasaidia katika maendeleo.

### 4.4.12 Mwanamke kama Mtu mwenye Huruma na Imani

Kuwa na huruma na imani ni jambo linalihitajika kwa kila binaadamu na kwa kila kiumbe. Kuwa na tabia ya unafiki, chuki, choyo, tamaa na mfano wa hayo

si katika tabia njema. Tabia kama hizo inakuwa ni vikwazo katika ujenzi wa jamii imara na yenye mafanikio. Katika kulijadili hilo mtafiti amebaini usawiri wa mwanamke katika suala zima la kumuhusisha na tabia njema ya huruma na imani kwa wanaadamu wenzake na viumbe vyenginevyo. Mtafiti kupitia data alizozikusanya amebaini tabia njema na huruma kupitia kwa Bi Hanuna. Bibi huyu alionesha huruma na imani kubwa baada ya kuiona hali ya Dania imekuwa mbaya sana. Wakati huo Dania alikuwa anasubiri kufa tu. Mwanndishi anafafanua:

> Bi Hanuna alilia! Alilia kwa uchungu na simanzi huku akimtazama yule mwanamke aliyekuwa kwenye kizingiti cha mauti Dania ….! Dania ….. Nime …. Nime ….. lolote alilokusudia kulisema lilikwama kooni ni ajabu sana kwani sasa Bi Hanuna alimlia mtu aliyekuwa akimchukia sana… Huku akilia kwa uchungu Bi Hanuna alimuinamia yule mwanamke aliyeitwa Dania pale kitandani na kumkumbatia kwa muda kisha akainuka na kubaki akimtazama huku akilia kwa uchungu ( uk 54 na 55).

Bila shaka mtafiti ameweka wazi usawiri wa huruma na imani ya Bi Hanuna kwa Dania. Kabla ya hapo kulikuwa na ugomvi mkubwa baina Hanuna na Dania. Huruma na imani pia imejitokeza kwa Bi Hanuna, Nunu, Dania ambao wote wlikuwa wanamlilia na kumuonea huruma Gaddi ambae alikuwa hali mbaya sana ya kukata roho pale kitandani.

Huruma na Imani walioionesha wanawake hawa juu hali mbaya walizokuwa nazo Dania na Gaddi zinaenda sambamba mkono imani kubwa aliyonayo mwanamke mapenzi umoja na mshikamano. Sambamba na hilo mwanamke anatakiwa kuwa mstari wa mbele katika kujenga imani ambayo itasaidia kuondoa chuki

miongoni mwa wanajamii. Nadharia inawahamasisha wanawake wote kuacha tabia ya kiburi na kwamba huruma na imani inajenga upendo kwa wanajamii wote.

### 4.4.13 Mwanamke kama Mroho wa Madaraka

Cheo ni dhamana. Mtu yoyote anaweza kuongoza kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa kufuatana na majukumu ya kazi yaliyopangwa. Hakuna mtu ambae anaondoka duniani na cheo na cheo. Kitu cha msingi kwa kila mtu ni kujua wajibu wake. Mtafiti katika ukusanyaji wake wa data amegundua baadhi ya wanawake ambao wamesawiriwa katika hali ya kuwania madaraka na vyeo. Kung'ang'ania madaraka sio jambo zuri. Kitu muhimu ambacho kinaonyesha kipimo cha utu ni utendaji wake wa kazi na jinsi anavyotekeleza majukumu ya kazi aliyopangiwa. Mtafiti amegundua udhaifu huo kwa kuangalia pale mwandishi alivyomsawiri Dania katika ofisi aliyokuwa akiifanyia kazi. Mwandishi anasema:

> ….. Alikutana na macho yenye hasira yaliyokuwa yakimchungulia kutokea nyuma ya vioo vya miwani ya macho aliyokuwa amevaa yule dada na hapo alihisi moyo wake ukimuenda mbio na kumpiga kwa nguvu. “ Ni vipi, vipi?” Alimuuliza yule dada taratibu huku akiushangaa moyo wake kwa kufanya vile ulivyofanya. “ Khah we vipi , vipi….? Hii ni ofisi yangu bwana! Sasa sijuwi wewe ni nani na kwa nini uko humu ….! Yule dada alimjia juu, na Gaddi alizidi kushangaa .
> Mimi ni Gaddi Bullah … Na hii ni ofisi yangu ….”Mi naona we Gaidi Bullah! Hebu toa hiyo miguu yako kwenye meza yangu na utoke humu ndani haraka ..!” “ We binti hebu kamata adabu yako wewe, umesikia? …alimwambia kwa hasira hakupenda jina lake kumwita gaidi. Nijuavyo mimi hii ofisi ni yangu na nimekuwa nikifanya kazi humu ndani kwa zaidi ya wiki tatu sasa! Sijuwi wewe ni nani mpaka uje …” Mimi ni Dania Theobald! Na ndiye mkuu wa kitengo hiki na mwenye ofisi hii!” Ghadhabu ilimpanda yule dada akabaki kusonya...!Akiwaacha wafanyakazi

> wengine wakitumbua macho kwa mshangao. " Kwenda mwana kwenda." Gaddi alisema kwa hasira … (uk 71 na 72 ).

Mtafiti baada ya dondoo hiyo amebaini chanzo cha chuki kubwa iliyojengeka miongoni mwao. Chuki hii ilisababisha mgogoro mkubwa kiasi cha Mama Mlole bosi wao kuingilia kati mgogoro huo na kutoa maamuzi yanayostahiki.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inahimiza demokrasia miongoni mwa wanajamii wakiwemo wanawake. Kwa vyoyote vile kama busara ingetumika yasingetokea matatizo kama hayo. Chuki na uhasama ndani ya jamii inabomoa badala ya kujenga. Ufeministi wa kiafrika unapinga udhalilishaji wa kijinsia. Wanaume hawapaswi kuwadhalilisha wanawake na wanawake hawapaswi kuwadhalilisha wanaume. Wote wawili; Dania na Gaddi walifanya udhalilishaji wa kijinsia. Mtafiti anaona kwamba kinachotakiwa kwa wafanya kazi ni kutunza demokrasia na nidhamu makazini ili tukuze uchumi wa taasisi zetu na taifa kwa ujumla.

### 4.4.14 Mwanamke kama Mtu aliyedhalilishwa

Udhalilishaji ni kitendo chochote anbacho mtu mmoja anamfanyia mtu mwengine bila ya ridhaa yake. Uadhalilishaji uko wa namna nyingi. Mifano ya udhalilisha unakuwa wa kimwili, kisaikoljia, kimaneno, kivitendo na aina nyenginezo. Kwa vyovyote vile udhalilishaji haupendezi na unapigwa vita ndani ya jamii zote.

Mtafiti katika ukusanyaji wake wa data amebaini udhalilishaji ukifanyika ofisini. Matokeo ya udhalilishaji huo ilikuwa ni kusababisha mgogoro mkubwa.

Jambo hili liliwaacha baadhi ya wafanyakazi wakitumbua macho kwa mshangao mkubwa. Hili lilifanyika katika ofisi ambayo alipangiwa Gaddi na Mama Mlole mara tu baada ya kutoka uhamishoni Arusha. Kabla ya hapo ofisi hiyo alikuwa akiifanyia kazi Dania. Wawili hawa walipokutana ofisini kila mmoja alimdhalilisha na kumdharau mwenziwe. Kila mmoja aliamini kuwa yeye ndie anayestahiki kuwa mkuu wa kitengo hicho. Mwandishi anasema :

> Mimi ni Gaddi Bullah …. Na hii ni ofisi yangu ….” Mi naona we Gaidi Bullah! Hebu toa hiyo miguu yako kwenye meza yangu na utoke humu ndani haraka ….!” “ We binti hebu kamata adabu yako wewe, umesikia? …alimwambia kwa hasira hakupenda jina lake kumwita gaidi. Nijuavyo mimi hii ofisi ni yangu na nimekuwa nikifanya kazi humu ndani kwa zaidi ya wiki tatu sasa! Sijuwi wewe ni nani mpaka uje …” …Mimi ni Dania Theobald! Na ndiye mkuu wa kitengo hiki na mwenye ofisi hii!” Mhmm! Ant … mimi naona we ni Damien The Omen, mana’ke …..” Gaddi naye alimgeuzia jina yule dada, akimaanisha kuwa alikuwa ni Damien badala ya Dania ) The Omen (badala ya Theobald ) mtoto wa kishetani, kutokana na filamu maarufu ya kizungu ya kutisha, Damien The Omen (uk .72).

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kupitia mihimili yake inapingana kabisa na udhalilishaji wa aina yoyote. Kitendo cha udhalilishaji hakina budi kupigwa vita kwa nguvu zote. Mtafiti amebaini kwamba bado vitendo kama hivi vinaendelea kufanyika ndani ya ofisi zetu. Vitendo hivyo vinafanywa na watendaji wetu makazini hususan wanawake. Ppia matendo kama haya yanafanyika ndani ya jamii zetu barabarani, masokoni, majumbani pamoja na sehemu nyenginezo. Mtafiti analaani hali hiyo na anatoa wito kwa wanajamii wote kuachana na vitendo hivyo. Vitendo vya aina hiyo, licha ya kuathiri kisaikolojia lakini pia vianathiri maendeleo kwa ujumla.

### 4.4.15 Mwanamke kama Mtu mwenye Kusababisha Mgogoro

Mgogoro ni kutokuelewana baina ya mtu mmoja na mwengine. Mgogoro husababisha chuki, fitna miongoni mwa wanajamii. Wakati mwengine migogoro hupelekea hata vita baina ya upande mmoja na mwengineKwa muktadha huo suala la migogoro sio zuri hata kidogo. Pindi patatokea mgogoro ni vyema pafanyike kufanyike suluhu ya haraka ili kuepusha mambo mabaya yasitokee. Mtafiti baada ya kukusanya data zake amebaini kwamba mwanamke amesawiriwa kama msababishaji wa mgogoro katika maeneo tofauti na kwa watu tofauti. Mwandishi ametuonesha migogoe mingi katika riwaya yake hii. Miongoni mwa migogoro hiyo ni mgogoro baina ya Dania na Mama Mlole, mgogoro baina ya Dania na Gaddi, mgogoro baina ya Nunu na Bi Hanuna, mgogoro baina ya Nunu na Dania, mgogoro baina ya Nyambuja na Gaddi. Mtafiti baada ya kuchambua data zake amebaini kwamba migogoro mingi ilifanywa na wanawake japokuwa chanzo ni wanaume. Mwandishi anatueleza mfano wa ugomvi baina ya Bi Hanuna na Dania hali hii ilitokea kutokana na Bi Hanuna kusalitiwa mdogo wake Gaddi sambamba na kupigwa nyumbani mwa Dania. Mwandishi anasema:

> "Alikwenda moja kwa moja hadi nyumbani kwa Dania . Huko alimpakia maneno makali juu ya mambo aliyomfanyia Gaddi. Dania alijitahidi kuhalalisha uamuzi wake huo lakini Bi Hanuna hakutaka kumsikiliza. " Wewe ni malaya usiye na haya ……baradhuli na hayawani! Hukumstahi mdogo wangu hata kidogo" ( uk. 126).

Vilevile hali ya mgogoro imejitokeza baina ya Dania na Gaddi katika kitengo chao ambapo kila mmoja aliamini kwamba yeye ndie anayestahiki kuwa mkuu wa kitengo. Mwandishi anasema:

> Mimi ni Gaddi Bullah …. Na hii ni ofisi yangu ….” Mi naona we Gaidi Bullah! Hebu toa hiyo miguu yako kwenye meza yangu na utoke humu ndani haraka ….!” “ We binti hebu kamata adabu yako wewe, umesikia? ….. alimwambia kwa hasira hakupenda jina lake kumwita gaidi. Nijuavyo mimi hii ofisi ni yangu na nimekuwa nikifanya kazi humu ndani kwa zaidi ya wiki tatu sasa! Sijuwi wewe ni nani mpaka uje …”
> Mimi ni Dania Theobald! Na ndiye mkuu wa kitengo hiki na mwenye ofisi hii!” Mhmm! Ant …… mimi naona we ni Damien The Omen, mana’ke …..” Gaddi naye alimgeuzia jina yule dada, akimaanisha kuwa alikuwa ni Damien ( badala ya Dania ) The Omen (badala ya Theobald ) mtoto wa kishetani , kutokana na filamu maarufu ya kizungu ya kutisha, Damien the Omen. (uk .72).

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika katika muhimili yake inahimiza utu wa mtu, usawa, demokrasia na inapinga vikali migogoro ambayo mwisho wake ni vita na uhasama mkubwa ndani ya jamii zetu. Kupitia nadharia hiyo, mtafiti anaendelea kuwataka wanawake na hata wanaume wasiwe chanzo cha migogoro katika jamii. Bado Ingawa bado ndani ya jamii migogoro ipo ila jambo la msingi ni ibakie hapana budi tu. Jambo hili ni lazima lipigwe vita kwa nguvu zote kwani migogoro hudhoofisha hata uchumi wa mtu.

### 4.4.16 Mwanamke kama Mtu asiyekata Tamaa

Binaadamu anatakiwa kuwa na juhudi ya kutafuta anapokuwa na shida ya jambo. Mafanikio ya kupata kitu yanatokea kutokana na bidii ya mtu na juhudi ya mtafutaji. Juhudi siku zote huzaa mafanikio. Waswahili wanasema “Mtaka chamvunguni sharti ainame”. Methali hii inatufundisha kuwa mtu hatakiwi kukata tama anapotafuta jambo lake. Anachotakiwa ni kuonesha jitihada kubwa mpaka apate mafanikio. Mtafiti baada ya kukusanya data mbalimbali amebaini kwamba mwanamke amesawiriwa kama mtu asiyekata tamaa. Hili limejitokeza

kwa Nunu ambae ni rafiki kipenzi cha Dania. , mwandishi amemsawiri mwanamke huyu kuwa kiumbe mweye bidii kubwa na mtu asiyekata tama haraka. Hali hii imejitokeza pale Nunu alipoonyesha uungwana wake kwa kumtafuta Gaddi kutoka nyumba hadi nyumba na kutoka mtaa hadi mtaa iliaweze kutimiza ahadi yake ya kumpa barua aliyopewa na Nunu. Hata hivyo juhudi ya Nunu ilipita bila mafanikio. Mwandishi ametuthibitishia hilo katika riwaya hii katika (uk 8, 9, 16, 51) Kwa mfano:

> "Nina shida ya Gaddi Bullah sijuwi nimemkuta?"Alimuuliza yule kijana baada ya kusalimiana naye. Yule kijana alikunja uso na kumtazama Nunu kama kwamba alikuwa mwehu" " Gaddi Bullah na huyo ndio nani bibie? Mbona simjuwi mtu huyo ? Alimuuliza kwa mshangao na moyo wa Nunu ukaingia baridi…..sauti kutoka nje vipi….. "Eee…. kuna dada hapa amepotea nyumba! Anamtafuta mwenyeji wake ….."( uk. 8)

Mtafiti baada ya kukusanya data zake amebaini kuwa bado Nunu hakukata tamaa aliendelea tena kumtafuta Gaddi tuangalie dondoo hii :

> Samahani anti. Mimi naitwa Nunu na nilikuwa na shida na mwenye nyumba…Nina ujumbe wake muhimu sana…"Yule dada alimtazama kwa muda, huku akionesha wazi kuwa hakupenda alivyoingia mle ndani….Mwenye nyumba ameenda kazini lakini mimi ndiye mkewe. Mkewe? …wewe ni mke wa Gaddi?...Khah!Wewe umekosea nyumba anti…Mimi ni mke wa mwenye nyumba hii, lakini mume wangu sio huyo unayemsema wewe. Mume wangu ni Uwesu.Uwesu Hamdani (uk. 9).

Hali hiyo hiyo aliendelea nayo Nunu kumsaka Gaddi kama mbwa mkali anaemsaka tumbili katika kichaka. Nunu hakufanikiwa na ndipo alipoamua kwenda kumteka nyara Bi Hanuna kama njia pekee ya kufanikisha lengo lake.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inaunga mkono na inahimiza juhudi za wanajamii katika kutafuta mafaniko ya jambo. Mtafiti amebaini kwamba katika kupata mafanikio ya jambo basi mtu anatakiwa asikate tamaa kwani raha au mafanikio yanakuja baada ya shida kubwa. Nadharia hii inahimiza juhudi, maarifa, hekima, na busara kama nyenzo za kumfikisha mwanaadamu hususan wanawake katika malengo yake. na kwamba Siku zote juhudi hujenga maarifa, na maarifa huzaa tunda la mafanikio kwa mtu na hata taifa kwa ujumla.

### 4.4.17 Mwanamke kama Mtu aliyekwepa Majukumu na asiye na Maadili ya Kazi

Kazi ni msingi wa maendeleo. Uwajibikaji kazini ndio mafanikio ya taasisi kampuni, wizara na serikali kwa ujumla. Moja katika jambo baya kazini ni mfanyakazi wa sekta yoyote iwe ya serikali au binafsi kukwepa majukumu ya kazi. Kufanya hivyo ni kurudisha nyuma maendeleo ya sehemu husika na jambo hilo linaweza kuingiza hasara kubwa katika taasisi husika. Mtafiti baada ya kukusanya data zake za utafiti amebaini kuwa mwanamke amesawiriwa katika suala zima la kukwepa majukumu. Pia mwanamke amesawiriwa kuwa mtu aliyekosa maadili ya kazi. mtafiti anaona hili si jambo jema na halifai kujaribiwa makazini. Kwa kulithibitisha hilo mwandishi nae amelionesha hilo pale alipomsawiri muhusika Dania kutenda makosa kama hayo. Aliyafanya hayo pale alipopangiwa kazi na bosi wake Gaddi na kuonesha jeuri na ufedhuli wa kutokumjali bosi wake. Alikwepa majukumu ya kazi aliyopangiwa na akaacha kuyatekeleza. Mwandishi analithibitisha hilo kama ifuatavyo:

> "Dania … unaendeleaje na taarifa yako.?" Alimuuliza huku kwa mara nyengine akiuhisi moyo wake ukimpiga kwa nguvu."Naendelea nayo bosi …muda sibado?" Dania alijibu bila kumtazama akionyesha wazi kuwa hakuwa akijali iwapo atamaliza kwa wakati au vinginevyo. Gaddi alikunja uso kwa ghadhabu (uk. 77).

Mwandishi katuonesha tena hali hiyo pale Dania kwa makusudi alipoiningia ofisini hadi muda wa kikao kuanza saa mbili na nusu asubuhi akimuacha Gaddi akiwa na ripoti isiyo kamili., Gaddi hakuridhika na tabia yake ile ndipo alipoamua kumuandikia barua na nakala kumpelekea Mama Mlole. Aliamua kumuandikia barua akimlaumu juu ya utendaji wake mbovu wa kazi. Gaddi anamsimulia bosi wake Mama Mlole kuhusu Dania: Mwandishi anasema:

> "Tabia yake chafu! Hana maadili ya kazi, jeuri .. Sijuwi ana matatizo gani yule dada! Hiyo barua ndicho anachostahili.Labda maelezo yakeyatahalalisha tabia yake hiyo, lakini mimi siwezi kuendelea kuvumilia uzembe wa makusudi." Gaddi alijibu kwa jazba (uk. 79).

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inahimiza uwajibikaji kazini na kupinga kabisa suala la ujeuri. Nadharia hii inazingatia usawa miongoni mwa wanajamii. Pia nadharia hii inahimiza nidhamu na heshima si kwa wanawake tu bali watu wote., Kitendo cha ufedhuli na jeuri hakifai na kinahitaji kupigwa vita kwa nguvu zote kwani matokeo yake ni kuleta mfarakano ndani ya wanajamii wenyewe.

### 4.4.18 Mwanamke kama Mtu aliyekata Tamaa ya Uhai

Uhai ni kitu muhimu sana katika maisha ya mwanaadamu. Bila uhai mwanadamu hawezi kufanya kitu chochote. Thamani ya mtu inatokana uhai anaoumiliki mtu huyo.. Kwa hivyo mwanadamu hana budi kuutumia uhai wake kwa kufanya mambo

mema. Binaadamu anapofanya mabaya ni lazima yatakujia majuto mwishoni. Majuto hayo yatakuwa makubwa hasa ubaya kama utakuwa umefanywa dhidi ya mtu mwengine.

Mtafiti katika ukusanyaji wake wa data amegundua ubaya mkubwa alioufanya Dania dhidi ya Gaddi. Pia mtafiti amebaini hali ya kukata tamaa kwa muhusika Dania katika vipindi tofauti. Mwandishi amemsawiri Dania akimfanyia ubaya mkubwa Gaddi. Hata hivyo Dania baada ya kukata tamaa ya uhai alibaini makosa yake. Wakati huo aliamua kumtaka radhi. Alifanya hivyo kwa kumpa barua Nunu ya kutaka msamaha na kumuomba radhi kwa Gaddi kutokana na makosa aliyomfanyia. Hali hii imejitokeza katika sehemu kadhaa katika riwaya hii. Baadhi ya maeneo ambayo hali hii imejitokeza ni (uk. 53,134,135, 141). Kurasa hizo zinamzungumzia Dania akiwa katika hali mbaya sana. Hali ya kukata tamaa na uhai. Mwandishi anasema:

> Dania alikuwa amelala hapa akisubiri kufa tu Bi Hanuna! Hakuna matumaini tena. Unadhani anapenda kuwa hapa katika hali hii? (uk. 53)

Vilevile mwandishi amelionyesha tena tendo la kukata tamaa kwa Dania kama ifuatavyo:

> Mwezi ulikatika, Dania alizidi kudhoofu, mwezi wa pili pia ulikatika, bado hakukuwa na mfadhili aliyepatikana na Dania alidhoofu zaidi…. Na mwezi wa tatu ulipoingia bila ya mfadhili kupatikana hali yake ilizidi kuwa mbaya zaidi,” …“Dania alijuwa kuwa anasubiri kifo tu sasa, “Nunu rafiki yangu .. mimi nakufa sasa! Nilifanya kosa kubwa la maisha yangu na sasa ninalipa kutokana na kosa hilo…Nilimuona Jerry bora kuliko Gaddi nawe ukaniambia najidanganya sikukusikia sasa nimedhihirisha mwenyewe …Hii ndio ile mkaidi hafaidi ila siku ya iddi…Najuta…Nakuomba umtafute Gaddi Nunu nakuomba umsihi

> aje anione japo kidogo. Nipate kumtaka radhi kwa mambo niliyomfanyia…Kitu pekee kitakachonifanya niende mbele ya haki kwa amani ni kujuwa kuwa Gaddi Bullah amenisamehe."(uk. 134 na 135)

Nadharia ya ufeministi wa kiafrika kupitia mihimili yake inahimiza wanajamii na wanawake kutendeana mema miongoni mwao Binaadamu ni kiumbe wa Mungu. Wakati wowote Mungu huyo anaweza kumpandisha daraja huyu na kumshusha huyu sasa Ni jambo jema kwa kiumbe mwanaadamu kutumia wakati wake vizuri. Hatakiwi kusubiri tusisubiri mpaka hali inapokuwa mbaya ndiyo akatafuta kosa ni lipi. Nadharia hii inatoa mafunzo kwamba mtu lazima awe makini katika maisha yake na ajuwe mazingira ya kuishi na watu katika hali ya amani na upendo.

### 4.4.19 Mwanamke kama Mtu Mwenye Msimamo

Msimamo ni kuwa na msisitizo wa jambo au kushikilia kitu kwa kauli ile ile ama chanya au hasi. Kwa kawaida msimamo mzuri (chanya) ndio unaofaa kuigwa na wanajamii katika kuleta maendeleo ya kweli. Mtafiti katika ukusanyaji wa data zake amegundua misimamo ya aina zote mbili (chanya na hasi). Mtafiti amejaribu kuichambua na kuifanyia kazi misimamo yote ya aina mbili. Hali hii imemsaidia sana mtafiti kuweza kugundua kuwa kwamba kumbe baadhi ya watu hawataki kushauriwa na wanaendelea kushikilia misimamo yao bila kuangalia athari ya baadae. Mtafiti amebaini hili kupitia usawiri wa wanawake kadhaa kama ilivyojitokeza katika riwaya ya mfadhili. Mfano mzuri wa kushikilia misimamo ni pale Bi Hanuna aliposhikilia msimamo wake wa kuikataa barua aliyopewa na Nunu iliyotoka kwa Dania ili imfikie Gaddi ( uk 32 na 33 ). Mwandishi anasema:

> “ Ah jamani sasa …? Nakuomba Bi Hanuna …mfikishie Gaddi hii barua ….‘Nunu alimwambia huku akimwekea ile barua mikononi mwake. Bi Hanuna aliiachia ile barua ikaanguka sakafuni, hakutaka kabisa kuipokea. “ Hebu ondoka kabisa na takataka yako hii” Bi Hanuna alimkemea huku akionyesha iliyokuwa na barua iliyolala sakafuni. (uk 33)

Mfano mwengine wa kung’ang’ani msimamo ni ule aliouonyesha Nunu ambae pamoja na majibu mabaya ya Bi Hanuna bado alishikilia msimamo wa kumbembeleza ili akubali kuichukua barua na kuipeleka kwa Gaddi. Bi Hanuna aliendelea na msimamo wake wa kuendelea kuipokea barua (uk.33):

> “Ah, Bi Hanuna! Yaani mi nimekuwa takataka kweli.? “Tokaaa.”
> “Sawa Bi Hanuna… Sawa …lakini kaa ukijuwa iko siku utakuja kujuta sana kwa hili ulilofanya leo.. wewe na Gaddi Bullah. …”(uk 33).

Mfano wa msimamo mwengine ni ule wa Dania kuendelea kumng’ang’ania Jerry. Aliendelea kubaki na Jerry licha ya ushauri mzuri aliopewa na Nunu ( uk. 127). Mwandishi analithibitisha hilo:

> “Lakini bado hujachelewa Dania! Bado una nafasi ya kurudi kwa Gaddi sasa na kumtaka radhi … naamini atakusamehe. Ni bora nusu ya shari kuliko shari kamili!”
> “Hapana Nunu nimeshaharibu kwa Gaddi sasa sinabudi ila kumng’ang’ania Jerry tu vinginevyo nitakosa kote”(uk. 127).

Nadharia ya ufeministi inaangalia haki na usawa miongoni mwa wanajamii. Pia nadharia hii inakemea vikali wanajamii wakiwemo wanawake wasiotaka mabadiliko na wasiokuwa na ubinaadamu. Inapaswa mtu ajuwe kwamba anapokosea katika jambo lolte suala la msingi ni kutafuta njia bora ya kukosoana ili kujenga umoja udugu na urafiki. Nadhari hii inawakosoa wale

wasiotaka ushauri mwema. Ushauri ni njia moja ya kuleta mabadiliko na maendeleo katika taifa.

### 4.4.20 Mwanamke kama Mtu Msomi (Mwenye Elimu )

Elimu ni ufunguo wa maisha. Elimu ni kitu muhimu sana katika maisha ya mwanaadamu. Maendeleo ya jamii au taifa lolote duniani linatgemea upeo wa elimu wa raia zake. Elimu ni msingi wa kwanza katika kujenga jamii yenye wataalamu na mafanikio makubwa. Elimu ndio msingi imara wa kujenga jamii au taifa lolote duniani. Elimu humuongoza mwanaadamu kuwa mwema kwa kutenda yanayofaa na kuacha yasiyofaa. Dini zote zinahimiza masuala ya kielimu ili mtu aweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Misingi ya ufeministi wa kiafrika inaosisitiza kuhusu mwanamke kujikomboa kielimu Data zilizokusanywa na mtafiti katika kitabu cha mfadhili zinaonesha kumsawiri mwanamke kuwa ni msomi mzuri. Usomi huo umedhihirika kutokana na juhudi kubwa iliyofanyika katika masomo na katika kuitumia vyema elimu iliyopatikana. Miongoni mwa wahusika wasomi walioweza kuitumia elimu yao vyema ni pamoja na Mama Mlole. Mama mlolealikuwa ni Afisa wa Utumishi katika kampuni yake jijini Dar es Salaam .

Mwandishi ametuonesha kwamba mama Mlole ni mwanamke asiyeyumba na mwenye kujiamini sana katika kazi zake. Aidha mwandishi ametuonesha jinsi gani mama Mlole alivyoweza kutumia elimu na busara zake katika kutatua matatizo mbalimbali. Mama Mlole aliweza kutumia hekima na elimu yake kwa kumtetea

Gaddi katika jopo la viongozi wenzake. Kutokana na utetezi huoGaddi akahamishwa jijini Arusha na kuletwa Dar es Salaam baada ya kufukuzwakazi (uk 73).

Kitu chengine kikubwa alichokifanya msomi huyu ni kitendo cha kumtetea tena Dania na kupewa likizo kwenda hadi Afrika ya Kusini kwa matibabu. Baada ya kurudi matibabu alimrudisha tena kazini jambo ambalo halikuwa rahisi (uk 89). Kitendo chengine cha kisomi alichikifanya Mama Mlole ni kile cha kuwapatanisha Gaddi na Dania na baadae kutoa maamuzi ya busara ya kumchagua Gaddi kuwa mkuu wa kitengo na Dania kuwa msaidizi wake. Sambamba na hilo mama Mlole alichukua fursa ya kumuelimisha Gaddi kuhusu barua kali aliyomuandikia Dania na kumtaka asiiweke katika faili (uk.93).

Mwandishi pia alimsawiri Dania kama msomi ingawa aliathirika na pombe kali baada ya kuathirika kwa penzi la Jerry. Kwa ujumla tunaweza kusema kwamba wanawake waliowengi sasa ni wasomi wakubwa na wenye uwezo mkubwa katika fani mbalimbali kama vile ualimu, udaktari, uhasibu, uongozi, uarubani na fani nyingi nyenginezo. Jambo hili limewafanya wanawake waweze kujiamini na kuwa viongozi bora kitaifa na kimataifa. Huu ni mfano wa kuigwa katika jamii zetu.

### 4.4.21 Mwanamke kama Mtu Msamehevu

Kila binaadamu ni mtenda makosa. Hata hivyo binaadamu aliye bora zaidi ni yule anayetambua makosa yake na akafanya haraka kuomba msamaha na

kujizatiti kutorejea tena kosa au makosa hayo. Tabia ya kusamehe au kusameheana ni jambo kubwa na muhimu kwa binaadamu yoyote. Kusameheana kunajenga upendo, masikilizano, ushirikiano na moyo wa kusaidiana. Tabia ya kusameheana humuepusha mwanaadamu na chuki, husda, choyo, ubinafsi, tamaa, kiburi na tabia mbovu zinazolingana na hizo. Suala la kusameheana lina nafasi kubwa katika kujenga jamii yenye umoja na mashirikiano. Umoja na mashirikiano ni mojawapo ya silaha yenye kuleta maendeleo.

Kwa kutumia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kupita riwaya ya Mfadhili kupitia data alizozikusanya mtafiti amebaini kuwa suala la kusameheana limejitokeza kupitia usawiri wa mwanamke. Katika kulichunguza hilo mwadishi amewatumia wahusika Mama Mlole, Bi Hanuna, na Nunu.

Mama Mlole aliamua kumsamehe Gaddi na Dania makosa tofauti ambayo kama si busara zake wangeweza kufukuzwa kazi. Pia Mama Mlole alimtaka Gaddi ambae ni mfanyakazi wake nae amsamehe Dania jambo ambalo Gaddi alilitenda. Bi Hanuna nae pamoja na jazba kubwa aliyokuwa nayo lakini mwisho baada ya kuupata ukweli aliamua kumsamehe Dania na Nunu ambapo aliwachukia mno hapo kabla.(uk 54 na 55). Kwa upande mwengine Nunu aliamua kusamehe rafiki yake Dania ambae alikuwa hataki kabisa kufuata ushauri wake. Wahusika wote hao walisameheana na baada ya hapo walijenga upendo mkubwa miongoni mwao. Hii inatupa mwanga kwamba wanawake ni watu wenye huruma sana na mapenzi. Kwa hakika wanawake kama hawa wanafaa kuigwa.

**Jadweli 4.1: Muhtasari wa Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya ya Mfadhili**

| Na | Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya ya Mfadhili |
|---|---|
| 01 | Mwanamke kama mshauri mwema |
| 02 | Mwanamke kama muhusika muwajibikaji kazini (bidii katika kazi) |
| 03 | Mwanamke kama muhusika mwenye mapenzi ya dhati |
| 04 | Mwanamke kama chombo cha starehe kwa mwanamme |
| 05 | Mwanamke kama muhusika mlevi |
| 06 | Mwanamke kama muhusika mwenye busara na hekima |
| 07 | Mwanamke kama muhusika msaliti |
| 08 | Mwanamke kama kiongozi bora |
| 09 | Mwanamke kama rafiki wa kweli na mwenye kutimiza ahadi |
| 10 | Mwanamke kama muhusika msuluhishi |
| 11 | Mwanamke kama muhusika asiyetaka ushauri |
| 12 | Mwanamke kama muhusika mwenye huruma na imani |
| 13 | Mwanamke kama mroho wa madaraka |
| 14 | Mwanamke muhusika aliyedhalilishwa |
| 15 | Mwanamke kama muhusika aliyesababisha mgogoro |
| 16 | Mwanamke kama muhusika asiyekata tama |
| 17 | Mwanamke kama muhusika anayekwepa majukumu na asiye na maadili mazuri kazini |
| 18 | Mwanamke kama muhusika aliyekata tamaa ya kuishi (uhai) |
| 19 | Mwanamke kama muhusika mwenye msimamo |
| 20 | Mwanamke kama muhusika msomi (mwenye elimu) |
| 21 | Mwanamke kama muhusika msamehevu |

Data kutoka katika Riwaya ya Mfadhili, Julai 2017

## 4.5 Sababu za Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya Teule ya Mfadhili

Mtafiti anaamini kuwa katika taswira mbalimbali alizosawiriwa mwanamke kupitia riwaya teule ya *Mfadhili* kuna sababu za kusawiriwa au mwanamke huyo kutenda matendo hayo. Maelezo yaliyotangulia (4.4) yamefafanua kwa kina usawiri wa mwanamke katika riwaya teule ya *Mfadhili*. Taswira mbalimbali zimejengwa na kuhusishwa na nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Katika sehemu hii, mtafiti ameeleza kwa kina sababu za usawiri wa mwanamke kama alivyoongozwa na lengo

mahsusi la pili la utafiti huu. Lengo hili linasema kwamba: Kuelezea sababu zinazomfanya mwanamke huyo asawiriwe hivyo alivyosawiriwa katika riwaya teule ya *Mfadhili.* Lengo mahususi hilo limekwenda sambamba na swali la msingi la pili la utafiti huu lisemalo: Ni sababu zipi zilizomfanya mwanamke huyo asawiriwe hivyo alivyosawiriwa katika riwaya teule ya *Mfadhili*?. Mtafiti kwa kuzingatia lengo mahsusi la pili na swali la pili la utafiti huu amefanya uchambuzi wa kina kuhusu sababu za usawiri wa mwanamke katika riwaya teule ya *Mfadhili* huku akirejelea taswira ya mwanamke huyo kwenye (4.4. 1 – 4.4.21) kama ifuatavyo:

### 4.5.1 Kuimarisha Uhusiano Mwema Baina ya Watu

Katika kufanikisha vyema sababu za mwanamke kuwa mwenye kuimarisha uhusiano mwema baina ya watu, mtafiti amerejelea taswira ya mwanamke kuwa ni mwenye kutoa ushauri mwema (4.4.1). Amebaini kuwa mwanamke huyo ana sababu kubwa ya kufanya hivyo. Hii ina maana kwamba mwanamke huyo ndio kiungo muhimu katika kuimarisha uhusiano mwema baina ya watu. Jambo hili huwafanya watu waondokanae na mizozo /migongano baina yao, iwe kazini au kwengineko. Mwanamke huyo hutekeleza dhima hiyo huku ikizingatiwa kwamba, yeye ni msimamizi wa majukumu mbalimbali. Mfano mzuri ni Mama Mlole pale alipomshauri Gaddi kufuta barua chafu aliyomwandikia Dania (uk 92). Mfano mwengine ni ushauri alioutoa Nunu kwa rafiki yake Dania ili aachane na mapenzi ya unafiki yaliyokuwepo baina yake na Jerry (uk 87).

Kwa hakika bado nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kupitia mihimili yake imeendelea kutumika. Katika kipengele hiki nadharia hii imetumika mkazo hoja

inayomuelezea mwanamke kuwa ni miongoni mwa wahusika wenye nia njema kwa maendeleo ya umma na ni mfano mwema wa kuigwa na jamii.

### 4.5.2 Kutekeleza Wajibu kama Mfanyakazi

Sababu nyengine ya msingi ambayo mtafiti ameibaini ni mfanyakazi kutekeleza wajibu wake. Mtafiti amerejelea taswira ya mwanamke kama muhusika muwajibikaji (4.4.2) na kubaini kwamba kuwajibika kazini ni sababu kubwa inayomfanya mfanyakazi huyo kuonekana kipimo chake kazini kuwa ni kizuri. Mfano mzuri ni ule aliouonesha Agnes; mfanyakazi wa Kampuni alivyotimiza wajibu wake pale kazini. Alitekeleza wajibu wake vizuri kwa kumkaribisha Nunu kwa uchangamfu na kwa bashasha kubwa ingawaje alikuwa hamjuwi. Alitimiza wajibu wake huo bila ujeuri. Nunu aliridhika na kuondoka na furaha kutokana na majibu mazuri ya dada huyo (uk 4 na 5).

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kupitia mihimili yake bado inasisitiza suala zima la uwajibikaji kazini. Kuwajibika kazini ni nyezo muhimu inayotumika kukuza uchumi na hata kuimarisha uhusiano mzuri baina ya mwajiri na muajiriwa. Swali la uwajibikaji kazini linajenga umoja na mshikamano miogoni mwa wanajamii wenyewe. Kwa misingi hiyo bado mwanamke ana kila sababu za kuendelea kuwajibika ipasavyo ili kuimarisha maendeleo yake na taifa kwa ujumla.

### 4.5.3 Kujenga Imani, Uhusiano wa Kweli usio na Shaka

Katika kujenga imani na uhusiano wa kweli baina ya wanajamii wenyewe, mtafiti amerejelea taswira ya mwanamke kama mtu mwenye mapenzi ya dhati

kama ilivyochambuliwa kwenye (4.4.3). Katika kipengele hicho mtafiti amebaini kwamba mwanamke anayo sababu kubwa ya kujenga imani, na uhusiano akiamini kwamba jambo hilo litajenga mashirikiano makubwa kwa familia, wanajamii na taifa kwa ujumla. Kutokana na sababu ya kujenga imani na uhusiano wa kweli, kuimarisha udugu na upendo wa dhati, mtafiti baada ya kukusanya data za utafiti huu amelibaini hilo katika kurasa mbalimbali ndani ya riwaya hii. Mifano inayohusiana na maswali ya kujenga imani na uhusiano imejitojeza kwenye (uk 7,17, 55, 86, 98, 99,123,125,144, 145,146).

Katika mifano ya kurasa hizo hapo juu mtafiti amewabaini wanawake kadhaa wakionyesha uhusiano huo kupitia wahusika kama vile Mama Mlole kwa wafanyakazi wake, bi Hanuna kwa ndugu yake Gaddi, Nunu kwa Boaz, Nunu kwa rafiki yake Dania, Dania kwa Jerry, Mama Dania kwa mtoto wake Dania, bi Hanuna kwa Dania, Dania kwa Juniour na wengineo. Katika kuchukua mfano wa wahusika hao mtafiti amebaini uhusiano na imani kubwa aliyoinesha Bi Hanuna kwa Dania kila mmoja akiwa amemshiba mwenzake kabla uhusiano huo haujaingiliwa na kuharibiwa na Jerry (uk. 98). Pia mtafiti amebaini tena mfano wa mahusiano na imani kubwa iliyosukumwa na udugu wa kidamu aliyokuwa nayo Bi Hanuna kwa mdogo wake Gaddi kutokana na uchungu alioupata mdogo wake baada ya kusalitiwa na Dania (uk. 125).

Nadharia ya ufeministi wa Kiafrika kupitia mihimili yake inahimiza imani, udugu na upendo. , Kwa kufanya hivyo wanajamii watakuza mahusiano ambayo yataondoa chuki na fitna na kujenga jamii bora kabisa. Dhana hii haikusudiwi

kwa jinsia moja tu bali ni jinsia zote, wanawake na hata wanaume kwa maslahi ya taifa.

### 4.5.4 Sababu ya Tamaa, Matamanio, na Kujridhisha Kimwili

Katika kukabiliana na tamaa na kujiridhisha kimwili, mtafiti amerejelea taswira ya mwanamke kama chombo cha starehe (4.4.4). Pia mtafiti baada ya kukusanya data zake vizuri katika utafiti huu amemrejelea mwanamke kama msaliti (4.4.7). Mtafiti amebaini kwamba sababu kubwa iliyomfanya mwanamke huyo kuwa chombo cha starehe na kuwa msaliti ni tamaa ya pesa na wakati mwengine kujiridhisha tu kimwili.

Baada ya kazi kubwa aliyoifaya mtafiti ya kukusanya data na kwa kuhusisha (4.4.4), aliyabaini hayo kupitia mahusiano ya kimapenzi kati ya Dania na Jerry. Wawili hawa walikuwa wakitoka kila siku kwenda katika starehe na mwisho kurudi kufanya starehe nyengine katika nyumba ya aidha Jerry au Dania (uk. 82). Mapenzi kama hayo tena yalifanyika baina ya Gaddi na Dania (uk. 99). Wakati fulani mapenzi yalifanyika kati ya, kati Nyambuja na rafiki yake Gaddi. Sambamba na hilo mtafiti akihusisha (4.4.7) amebaini sababu ya tamaa na matamanio ya kimwili ndio iliyomfanya Nyambuja kumsaliti mumewe (Gaddi). Hili ilitokea pale ambapo Nyambuja aliandika barua kule Arusha na kumuachia mumewe ili kukata uhusiano wao. Alifikia uamuzi huo ilia pate fursa nzuri ya kufanya mapenzi na rafiki wa mumewe (uk.65). Sambamba na hilo mtafiti kupitia mwandishi wa riwaya hii ya *Mfadhili* amebaini pia usaliti

uliofanywa na Dania pale alipoamua kurudiana tena na Jerry kwa sababu ya tamaa mbaya ya kimwili.

Nadharia ya Ufeministi ya Kiafrika kupitia mihimili yake inapinga vikali hali hiyo. Nadharia hii kwamba mahusiano yasiyozingatia misingi na tama za kimwili ni udhalilishaji mkubwa wa wanawake. Njia pekee ya kuweza kujikomboa na idhilali hiyo kwa wanawake ni kujitambua na kujiamini. Vilevile wanawake wanaweza kujikomboa kwa kufanya kazi za kujiajiri wenyewe yaani ujasiriamali. Kufanya hivyo kutawawezesha kupata kipato cha halali na pia wataweza kukuza uchumi na kujipatia maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

**4.5.5 Sababu ya Kuondoa Mawazo Potofu**

Kuondoa mawazo hasa potofu sio jambo baya endapo njia itakayoitumika inakubalika., mtafiti katika kulifahamu hilo amerejelea taswira ya Mwanamke kama Mlevi (4.4.5). Mtafiti amebaini kwamba sababu kubwa inayowafanya wanawake hao kulewa, ni kuamini kwamba pombe itawasaidia sana katika kuondoa mawazo machafu katika akili zao.Wamefanya hivyo huku wakiwa wameshindwa kutafakari kwamba pombe au ulevi wa aina nyengine yoyote una athari kubwa katika mwili wa mwanaadamu.

Mtafiti baada ya kukusanya data za kutosha amebaini kwamba Dania alikuwa akitumia ulevi aina ya pombe.Mwanamke huyo aliamua kufanya hivyo kwa makusudi kwa madai ya kuondoa mawazo aliyokuwa nayo baada ya kitendo cha kusalitiwa na Jerry. Awali Dania alimtarajia Jerry kuja kutoka Marekani,

kwa la kutekeleza ahadi yao ya kufunga ndoa. lengo kitendo cha Jerry kutokuhudhuria siku iliyotarajiwa kuwa ya ndoa yao kilimfanya Dania kuchanganyikiwa na ndipo alipotumia njia ya kunywa pombe ili kuondoa mawazo ya kumfikiri sana Jerry. Unywaji wa pombe uliokithiri baadae ilisababisha madhara makubwa kwa Dania (uk 105).

Bado nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kupitia mihimili yake inaendelea kuchukua nafasi katika eneo hili. Nadharia hii imekuwa ikisisitiza tabia njema za wanawake ikiwa ni pamoja na kukuza maadili na kukataza maovu. Unywaji wapombe ni mojawapo ya maovu makubwa. Unywaji wa pombe unaathari kubwa katika kuvuruga na kuharibu afya ya mwili..

### 4.5.6 Kujenga Upendo wa Dhati na Huruma

Katika kujega upendo wa dhati na kuhurumiana hasa wakati wa shida kwa wafanyakazi, jamii, na hata marafiki mtafiti amelibanisha hilo kwa kurejelea taswira ya mwanamke kama ilivyofafanuliwa kwenye (4.4.6). Pia mtafiti amerejelea taswira ya mwanamke kuwa ni rafiki wa kweli na mwenye kutimiza ahadi. pia mtafiti amelibainisha hilo tena kwa kurejelea taswira ya mwanamke kuwa muhusika mwenye huruma (4.4.12). Mtafiti amebaini kuwa mwanamke huyo ana kila aina ya sababu ya kufanya hivyo.

Mtafiti baada ya kazi kubwa ya ukusanyaji wake wa data amelibaini hilo katika (4.4.6) pale Nunu alipokuwa akimnasihi sana Bi Hanuna ili aipokee ile barua aliyopewa na Dania ingawa Bi Hanuna hakuwa tayai kufanya hivyo

(uk. 27 na 29). Mfano mwengine mzuri ni ule aliounesha Mama Mlole kwa mfanyakazi wake Gaddi Bullah baada ya sakata ya kutaka kufukuzwa kutokana na uzembe alioufanya kule Arusha. Kule Arusha Gaddi Bullah alitia saini cheki isiyo halali., Hata hivyo kwa busara na hekima, mama huyu aliamua kuitisha jopo la viongozi na kuwashawishi viongozi wenzake kumpa uhamisho kutoka Arusha ili kuja tena kuendelea na kazi Dar es Salaam. Mama Mlole alifanikiwa kulishawishi jopo la uongozi kukubaliana na wazo alilolitoa (uk. 88). Sambamba na hilo mtafiti pia amebaini upendo mwengine kama huo aliporejelea taswira ya mwanamke kama Rafiki wa kweli na Mwenye kutimiza ahadi (4.4.9). Mtafiti amelibaini hilo wakati Nunu aliendelea kutimiza ahadi yake ambayo alimuahidi rafiki yake {Nunu] kwamba ataipeleka barua aliyopewa na Dania ili amfikishie Gaddi. Hapana shaka huu ni upendo wa dhati wa marafiki hawa.

> “ Eeeh, jamani sasa hili balaa gani hili! Nilimuahidi kuwa nitahakikisha kuwa Gaddi anapatikana na sasa nimeshidwa kutimiza ahadi hii muhimu sana kwa rafiki yangu!” Nunu alilalama na kuanza kulia te na”(uk.19).

Mwandishi katuonesha tena upendo wa dhati wa Nunu pale alipoona ubaya wa Jerry na kumtaka Dania aachane na Jerry ingawa Dania aliendelea kishikilia msimamo wake (uk. 114). Pia kwa kurejelea (4.4.12) mtafiti amebaini kwamba mwanamke ni mtu mwenye imani kubwa na huruma nyingi. Hili limejitokeza kwa Bi Hanuna alipokuwa akimlilia Dania kutokana na hali yake mbaya sana aliyokuwa nayo kutokana kukosa mtu wa kumfadhili ini., Pamoja na Bi Hanuna kumchukia Dania lakini wakati huo ilimjia huruma akajikuta anamlilia kwa majonzi na kumuhurumia (uk. 54 na 55 ).

Kwa hakika nadharia ya ufeministi kupitia mihimili yake inaendelea kusisitiza juu ya marafiki na wanajamii wote wakiwemo wafanyakazi na hata viongozi kushikamana na kusaidiana. Ushirikiano na mshikamano hujenga imani na upendo miongoni mwa wanajamii wana wake wakiwemo. Wanawake na wanajamii kwa ujumla wakifanya hivyo watasaidia sana kuimarisha juhudi za maendeleo ya watu na taifa kwa ujumla.

### 4.5.7 Sababu ya kujenga Imani na Demokrasia, Mashirikiano, na Uhusiano Mwema

Hapana shaka kwamba mashirikiano, usawa kwa wote, na uhsiano mwema ni kitu muhimu sana. Mambo haya ni muhimu makazini na hata katika familia na ndani ya jamii ambayo mwanaadamu anaishi katika maisha yake ya kila siku. Mtafiti amerejelea taswira ya mwanamke kama Kiongozi Bora (4.4.8) pamoja na taswira ya mwanamke Kama Msuluhishi (4.4.10). Mtafti ameona kuwa kuna kila aina ya sababu ya mwanamke huyo kufanya hivyo.

Mtafiti baada kukusaya data zake kwa umakini sana akihusisha kipengele (4.4.8) amebaini kwamba usimamiaji wa demokrasia na usawa uliofanywa kwa na Mama Mlole ambae ni kiongozi wa juu wa kampuni alipotoa maamuzi ya ugomvi uliojitokeza kati ya Dania na Gaddi. Dania aling’ang’ania ofisi aliyoicha baada ya kuona ofisi hiyo imepewa kiongozi mwengine yaani Gaddi. Mama Mlole alitoa maamuzi ya kidemokrasia yaliyozingatia hekima, busara, na usawa. Alitoa uamuzi kwamba Gaddi ataendelea kuwa mkuu wa kitengo na Dania atakuwa msaidizi wake (uk.73 na 74). Sambamba na hilo baada ya

kukusanya data na kuhusisha ushahidi wa kutosha na kwa kuhusisha (4.4.10) mtafiti mtafiti ameona kwamba sababu kubwa ya kujenga mashirikiano na uhusiano mwema baina ya wafanyakazi ni kuwepo suluhu ya ugomvi iliyofanywa na mama Mlole. Mama Mlole alifanya suluhu kuondoa mfarakano kati ya Dania na Gaddi. Mfarakano huu ulikuja pale Dania alipopokea barua kali kutoka kwa Gaddi. Barua hii ilipomfikia Mama Mlole alitumia busara na kwa kwa hivyo akamuelewesha Gaddi madhara ya barua ile kwa Dania endapo barua ile itawekwa katika faili lake. Gaddi alimuelewa bosi wake na kubadilisha maamuzi (uk 92). Katika kuteleleza maamuzi hayo Gaddi aliamua kumsamehe Dania na hapo ndipo mapenzi na mashirikiano baina yao yalipoanzia. Tuangalie mwandishi anavyosema:

> Kwa mshangao mkubwa alimshuhudia Gaddi akiichukuwa ile barua yake ya maelezo, ile barua kali aliyo mwandikia hapo awali na nakala ya barua ile iliyokwenda kwa Mama Mlole na kuzipanga pamoja. Kisha alitoa kiberiti cha gesi na kuzitia moto zote palepale ofisini. Macho yalimtoka Dania na kumtazama kwa mshangao mkubwa kabisa. Hilo suala limeisha kama barua hizi zinavyomalizwa na huu moto! .. Oooh, Bosi! Ahsante sana bosi!" Dania alisema kwa hamasa huku akiinuka na kumpa mkono Gaddi ambaye nae aliinuka na kuupokea ule mkono huku akicheka (uk 94 na 95).

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kupitia mihimili yake inatilia mkazo na kutoa msisitizo mkubwa juu ya suala zima la kujenga demokrasia ya kweli miongoni mwa wanawake na wajamii wote. Pia nadharia hii inahimiza upendo, udugu, mashirikano baina ya watu wote Nahari hii pia inatoa changamoto juu ya viongozi wote kujenga uhusiano mwema na kusameheana kwa kufanya suluhu pale panapotokea mfarakano. Hali hii itapelekea kujenga uhusiano mwema kwa wanajamii wenyewe na taifa kwa ujumla.

### 4.5.8 Sababu ya Ujeuri, Chuki Binafsi na Kujionyesha

Ni jambo lisilo na shaka kwamba ujeuri, chuki binafsi na kujionyesha ni vitu visivyoleta faida yoyote ndani ya jamii zetu. Mambo hayo yanaweza kuleta mfarakano mkubwa iwapo hayatochukuliwa tahadhari kubwa. Katika kuliangalia hili kwa undani mtafiti amerejelea taswira ya mwanamke kama Mroho wa Madaraka (4.4.13) pamoja na taswira ya mwanamke anayekwepa Majukumu na asiye na Maadili ya Kazi (4.4.17). Mtafiti ameona kuna sababu za msingi za mwanamke kufanya hivyo.

Mtafiti baada ya ukusanyaji wake wa data akihusisha na kipengele cha (4.4.13) amebaini kwamba mgogoro mkubwa na chuki nyingi zilijitokeza baina ya Gaddi na Dania. Kila mmoja aliamini kuwa yeye ndie mwenye haki ya kuwa kiongozi katika kitengo walichokuwa wakigombania. Hata hivyo baadae mgogoro huo uliingiliwa kati na Mama Mlole na kutolewa maamuzi. Pia mtafiti katika ukusanyaji wake wa data na kwa kuhusisha kipengele cha (4.4.17) amebaini sababu za Dania kukwepa majukumu ya kazi ni chuki binafsi, dharau na kiburi alichokijenga dhidi ya bosi wake (Gaddi). Uthibitisho wa hili ni pale Gaddi alipomtaka Dania kuandaa ripoti kwa ajili ya kuwasilisha mkutanoni siku inayofatia. Dania kwa makusudi hakuandaa ripoti hiyo na ikatokea aibu na chuki baina yao.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kupitia mihimili yake inakataza kabisa tabia mbaya ikiwa ni pamoja kujengeana fitna. Kujengeana fitina si jambo zuri

hasa kwa wanawake kwani linaharibu mfumo mzima, wa maendeleo ya wanajamii wenyewe na taifa kwa ujumla.

### 4.5.9 Sababu ya Kukosa Maamuzi ya Busara, Hekima na Ustahamilivu

Katika maisha ya mwanaadamu maamuzi ya busara, hekima, na ustahamilivu ni jambo muhimu sana.Vitu hivi ni adimu sana na si watu wengi waliojaaliwa kuwa navyo. Yule anaejaaloiwa kuwa navyo basi anapata mafanikio mazuri katika kuendesha mambo mbalimbali ya kijamii. Mtafiti amerejelea taswira ya mwanamke kama mtu aliyedhalilishwa (4.4.14) pamoja na taswira ya mwanamke kama mtu aliyesababisha mgogoro (4.4.15). Mwanamke anayo sababu ya kukosa maamuzi ya busara, hekima ustahamilivu. Kwa kuhusisha (4.4.14), mwanamke kama mtu aliyedhalilishwa, mtafiti baada ya kukusanya data za kutosha kupitia mwandishi wa riwaya hii amebaini malumbano makubwa yaliyochanganyika na matusi ya kudhalilisha aliyoyafanya Gaddi kwa Dania. Kila mmoja alijiona kuwa ana haki ya kukaa katika ofisi kuliko mwenzake. Mtafiti amebaini kwamba hakukuwa na hekima wala busara iliyotumika katika kuelimishana juu ya jambo hili. Kwa sababu hiyo wawili hawa walikosa subira (uk. 72).

Vile vile mtafiti kupitia mwandishi wa riwaya hii ameonesha tena ukosefu wa subira na ustahamilivu (4.4.15) kwa kusawiriwa mwanamke kama mtu aliyesababisha mgogoro. Baada ya mtafiti kukusanya data za kutosha aliridhika kutokana na sababu za ukosefu wa subira na ustahamilivu. Hali hii ilisababisha migogoro ya mbalimbali miongoni mwao ni: (i) Mgogoro uliojitokeza baina ya Nunu na Bi Hanuna. Sababu ya mgogoro huu ilikuwa ni Nunu kumlazimisha Bi

Hanuna kuipokea barua inayokwenda kwa Gaddi (uk 26). (ii) Mgogoro uliojitokeza baina ya Dania na Gaddi. Hii pia sababu nyingine iliyosababisha watu kukosa subira ni ile aliyoionyesha Dania kwa kumtukana Gaddi na kumuita gaidi jambo ambalo lilimchukiza sana Gaddi na hata Gaddi nae kuamua kumuita shetani. Nadharia ya Ufeministi ya Kiafrika inasisitiza umoja, mashirikiano na mshikamano, miongoni mwa wanajamii na inapinga vikali suala la udhalilishaji wa watu wote hususan wanawake. Nadharia hii inapingana na aina yoyote ya mgogoro, chuki, lakini inawataka wanajamii wote kuwa na subira ndani ya jamii zetu.

### 4.5.10 Sababu ya Kushikilia Msimamo alionao Mwanamke

Msimamo sio kitu kibaya endapo msimamo huo utaleta faida kwa wanaoushikilia. Kitu kinachowaathiri watu wengi ni kushikilia msimamo ambao matokeo yake ya mwisho ni mabaya. Jambo la kushililia misimamo mibaya humsababisha muhusika kujutia kitendo alichokifanya. Katika kuliangalia hili mtafiti amerejelea taswira ya Mwanamke kama mtu asiyetaka ushauri (4.4.11). Pia mtafiti amerejelea taswira ya mwanamke kama mtu mwenye msimamo (4.4.19). Katika ukusanyaji wake wa data mtafiti amebaini kuwa ipo sababu kubwa ya mwanamke kufanya hivyo. Kwa kuhusisha na (4.4.11), mtafiti amebaini kuwa sababu kubwa ya kushikilia msimamo huu ni kuwa na matamanio na tamaa bila kujua nini hatma ya msimamo huo. Mwandishi katuonesha hilo kupitia Dania. Wakati ambapo mwanamke huy pale alikataa ushauri wa Nunu wa kumtaka aachane na Jerry na ashirikiane na Gaddi. Dania hakukubaliana na ushauri huo na badala yake aliendelea kushikilia msimamo wake wa kuendelea na mapenzi na Jerry

hadi aliposalitiwa mara ya pili (uk.116 na 127). Vilevile mtafiti amebaini sababu nyingine ya mwanamke kushikilia msimamao wake alionao. Hili limeonekana pale Nunu aliposhikilia kwamba lazima barua imfikie Gaddi ili akate kiu ya rafiki yake Dania ya kupata msamaha kutoka kwa wa Gaddi kabla kukata roho (uk 33).

Kwa kuzingatia Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inawaongoza watu wote kuwa wema. Wajilazimishe kuachana na tabia mbaya. Nadharia hii inatoa tahadhari kwamba juu ya wanawake. Ni vyema kwa wanawake kujishughulisha na ujasiri amali ili waweze kujipatia maendeleo yao binafsi na taifa kwa ujumla.

**4.5.11 Sababu ya Kukosa Mfadhili wa Ini**

Ufadhili ni aina moja ya msaada ambayo mtu anaweza kutoa au kupokea kutoka kwa mtu, watu, familia na hata taifa. Mwandishi wa riwaya hii amemsawiri mwanamke kama mtu aliyehitaji ufadhili. Katika kuliangalia kwa kina suala hili mtafiti amerejelea taswira ya mwanamke kama mtu aliyekata tamaa ya kuishi (4.4.18). Baada ya mtafiti kukusanya data za kutosha amebaini kwamba, sababu ambayo imemfanya mwanamke (Dania) kukata tama ya kuishi ni kukosa ufadhili. Kama ilivyoshauriwa na dokta Virani baada ya uchunguzi wake wa kina ilihitajika kwamba lazima Dania afanyiwe upasuaji na aingizwe ini jengine. Jambo hili pekee ndilo litakalomfanya apone maradhi yake. Kukata tama kulizidi kuongezeka siku hadi siku kila hali ilipokuwa inazidi kuwa mbaya.

> "Dania alijua kuwa anasubiri kifo tu sasa, " Nunu rafiki yangu ….. mimi nakufa sasa! Nilifanya kosa kubwa la maisha yangu na sasa ninalipa kutokana na kosa hilo…Nilimuona Jerry bora

> kuliko Gaddi nawe ukaniambia najidanganya sikukusikia sasa nimedhihirisha mwenyewe…. Hii ndio ile mkaidi hafaidi ila siku ya iddi….Najuta...”
> Nakuomba umtafute Gaddi Nunu nakuomba umsihi aje anione japo kidogo. Nipate kumtaka radhi kwa mambo niliyomfanyia…Kitu pekee kitakachonifanya niende mbele ya haki kwa amani ni kujuwa kuwa Gaddi Bullah amenisamehe”(uk. 134 na 135).

Baada yote hayo mwisho wake alijitokeza mfadhili (GaddiBullah) kutoa ini hilo kuokoa maisha ya Dania (uk 137). Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kupitia mihimili yake inawataka wanawake kuwa na subra na kutokukata tamaa na pia tuwe na moyo wa kusaidiana hasa wakati wa shida na tuwe tayari kuokoa maisha ya wenzetu pale inapobidi ili kujenga imani na upendo wa kweli katika maisha yetu ya kila siku.

**4.5.12 Sababu ya kupata Maendeleo ya Kielimu, Kijamii, Kiuchumi na Kifikra.**

Maendeleo ni kujitokeza kwa mabadilko kutoka hatua moja dhaifu kwenda katika hatua nyengine iliyobora zaidi. Maendeleo yanaweza kuwa ya kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni, kielimu na hata kifikra. Maendeleo yote hayo hayawezi kupatikana kama mtu hana elimu. Elimu ni jambao kubwa amabalo linaweza kumkomboa mtu na kumwezesha kupata maendeleo kutoka hatua moja kwenda hatua nyengine. Hapana shaka elimu ndio ufunguo wa kila kitu.

Katika kuliangalia suala hili mtafiti amerejelea taswira ya mwanamke kama mtu mwenye elimu kama ilivyofafanuliwa kwenye kipengele (4.4.20). Baada ya kukusanya data za kutosha mtafiti amebaini kuwa mwanamke mwenye elimu ana kila sababu ya kupata maendeleo kiuchumi, kijamii na hata kifikra. Mtafiti

ametolea mfano wahusika wanawake ambao wamesawiriwa kama wasomi. Amemtumia Dania kama kigezo muafaka cha mwanamke wa aina hiyo. Kutokana na usomi wake Dania alipewa ukuu wa kitengo cha kampuni kabla ya kuja bwana Gaddi na kuwekwa msaidizi mkuu wa kitengo baada ya kuja Gaddi (uk…79). Pia katika ukusanyaji wa data zake mtafiti amebaini kwamba elimu ni sababu moja wapo ya kupata maendeleo ya kiuchumi. Mwandishi alitumia mfano wa Mama Mlole amabae alikuwa na elimu. Elimu hiyo ilimtanua kifikra na ndio sababu iliyomfanya kupewa uongozi. Lakini kwa usahidi zaidi mtafiti amebaini kwamba mwandishi amemsawiri mwanamke huyu kuwa msuluhishi (uk 73), kiongozi (uk 88) na mtu mwenye busara na hekima (uk 129). Mambo haya yote haya yamechangiwa na suala zima la elimu. Kwa hivyo tunaweza kusema kwamba Mama Mlole ni mwanamke ambae anaitumia vyema elimu yake kwa maslahi yake na umma.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kupitia mihimili yake inahimiza sana wanawake kujikomboa katika Nyanja zote za kiuchumi, kijamii, kifikra na kielimu. Elimu anayoipata mwanamke inatarajiwa iweze kumletea maendeleo ambayo yataweza kukwamua kimaisha yeye mwenyewe, familia yake na taifa lake.

### 4.5.13 Sababu ya Kujutia Makosa aliyoyafanya

Hakuna binaadamu ambae hafanyi makosa. Kila mtu ana udhaifu wake. Hata hivyo, udhaifu pia umetofautiana baina ya mtu mmoja na mwengine. Kwa maana nyengine ni kusema hakuna yoyote aliyemkamilifu. Kitu cha msingi kwa kila binaadamu ni kutambua kosa lake na kujutia kosa hilo. Ni vyema pia kwa

aliyekosea kutafuta njia kutubu/kuomba radhi kwa aliyemkosea. Katika kuliangalia suala hili mtafiti amerejelea taswira ya mwanamke kama mtu msamehevu (4.4.21). Mtafiti baada ya kusoma vizuri kitabu teule na kukusanya kwa umakini data zake amebaini sababu mbali mbali zilizomfanya mwanamke kujutia makosa yake. Jambo hili limejitokeza pale mwandishi alipomsawiri Bi Hanuna akimlilia sana Dania pale kitandani baada ya kuiona hali yake kuwa ni mbaya kiasi cha kutisha mno. Dania alifikia katika umahtuti, akawa kama kwamba alikuwa akisubiri dakika yake ya kifo tu. Hili lilitokea pale ambapo Bi Hanuna alichukuliwa kwa nguvu na Nunu (katekwa nyara) kwa lengo la kuja kujionea mwenyewe hali ya Dania. Wakati huo Bi Hanuna alikuwa anamkatalia Nunu kuipokea barua ya Gaddi (uk. 53).

Mwandishi pia amemsawiri Dania na jinsi alivyojutia makosa yake kutokana na kitendo cha kumsaliti Gaddi. pamoja na ushauri wa mara kawa mara aliokuwa akipewa na rafiki yake Nunu, baada ya mwisho kutambua kuwa Jerry hakuwa mtu mzuri kwake ndipo alipoamua sasa kumpenda Gaddi lakini alikwisha chelewa kwani Gaddi hakuwa mtu wa kupendwa tena kutokana na yeye kusubiri dakika yake ya kifo tu (uk. 141) .

Nadharia ya Ufeministi kupitia mihimili yake inawahimiza wanawake wachague watu wenye mapenzi ya kweli katika maisha yao. Waache kuchagua wenza kwa njia za kukurupuka. Pia wwanawake wanasisitizwa kuzingatia ushauri wa marafiki zao ili kupata mawazo mem yenye manufaa kwao. Pia watu wa jinsi zote mbili wanashauriwa kushikamana na mapenzi ya dhati huku wakijua kwamba

huu si wakati wa kudanganyana. Watu wakiwa wakweli katika mapenzi yao watapata kushirikiana na kujenga maisha ya furaha na kwa sababu hiyo maendeleo yatapatikana.

**Jadweli 4.2: Muhtasari wa Sababu za Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya teule ya Mfadhili**

| Na | Sababu za Usawiri wa Mwanamke huyo katika riwaya ya Mfadhili |
|---|---|
| 01 | Sababu ya Kuimarisha Uhusiano Mwema baina ya Watu |
| 02 | Sababu ya Kutekeleza Wajibu wake kama Mfanyakazi (muajiriwa) |
| 03 | Sababu ya Kujenga Imani, Uhusiano wa Kweli usio na Shaka |
| 04 | Sababu ya Tamaa, Matamanio, na Kujiridhisha Kimwili |
| 05 | Sababu ya Kuondoa Mawazo potofu |
| 06 | Sababu ya Kujenga Upendo wa Dhati na Huruma |
| 07 | Sababu ya Kujenga Demokrasia, Mashirikiano na Uhusiano Mwema |
| 08 | Sababu ya Ukosefu wa Nidhamu, Ujeuri, Chuki binafsi na Kujionyesha |
| 09 | Sababu ya Kukosa Maamuzi ya Busara, Hekima na Ustahamilivu |
| 10 | Sababu ya Kushikilia Msimamo Wake |
| 11 | Sababu ya Kukosa Mfadhili |
| 12 | Sababu ya Kupata Maendeleo ya Kielimu, Kijamii, Kiuchmi na Kifikra |
| 13 | Sababu ya Kujutia Makosa Aliyoyafanya |

Data kutoka riwaya ya Mfadhili, Julai 2017

# SURA YA TANO

# 5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii ni ya mwisho katika utafiti huu. Sura hii inahusiana na Muhtasari, Hitimisho na Mapendekezo ya utafiti huu.

## 5.2 Muhtasari

Utafiti huu unahusu mada ya utafiti isemayo: Kutathmini usawiri wa mwanamke katika riwaya ya Mfadhili. Utafiti huu uligawanywa katika sura zifuatazo:

**Sura ya kwanza; Utangulizi wa ujumla:** Vipengele vilivyojadiliwa ni pamoja na; Utangulizi, Usuli wa mada, Tatizo la utafiti, Malengo ya utafiti, (Lengo kuu na malengo mahsusi) Maswali ya utafiti , Umuhimu wa utafiti, Mipaka ya utafiti, Muundo wa tasnifu na Hitimisho.

Katika utafiti huu mtafiti aliongozwa na malengo ya aina mbili, Lengo kuu na malengo mahsusi. Lengo kuu lilikuwa ni Kutathmini Usawiri wa Mwanamke katika riwaya ya *Mfadhili* . Malengo mahsusi yalikuwa mawili (i) Kubainisha taswira mbalimbali za mwanamke alivyochorwa katika riwaya ya *Mfadhili*. (ii) Kuelezea sababu zilizomfanya mwanamke huyo asawiriwe hivyo alivyosawiriwa katika riwaya teule ya Mfadhili. Sambamba na hilo utafiti huu uliambatana na maswali mawili ya msingi: (i) Ni taswira zipi zilizobainishwa

na kuchorwa katika riwaya ya *Mfadhili?* (ii) Ni sababu zipi zilizomfanya mwanamke huyo asawiriwe hivyo alivyosawiriwa katika riwaya teule ya *Mfadhili*?

**Sura ya pili; Mapitio ya kazi Tangulizi na Mkabala wa Kinadharia:** Sura hii ilijumuisha mada ndogo ndogo zifuatazo; Utangulizi, Ufafanuzi wa istilahi muhimu, Mapitio ya kazi Taangulizi, Nadharia iliyotumika ambayo ni nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika na mwisho Hitimisho.

**Sura ya tatu; Mbinu za Utafiti:** Katika sura hii vipengele vifuatavyo vilijadiliwa: Utangulizi, Maana ya mbinu za utafiti, Eneo la Utafiti na sababu za eneo la utafiti, Mbinu ya Usampulishaji, Ukusanyaji wa data, na mbinu za ukusanyaji wa data, Mbinu za uchambuzi wa data iliyotumika ambayo ni ya kimaelezo na mwisho palibainishwa Hitimisho.

**Sura ya nne, Uwasilishaji, Uchambuzi wa Data za utafiti:** Vipengele vilivyojadiliwa katika sura hii ni pamoja na: Utangulizi, Usuli wa mwandishi Hussein Issa Tuwa, Muhtasari wa riwaya ya *Mfadhili,* Uchambuzi wa usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Mfadhili* na sababu za usawiri wa mwanamke huyo na Mwisho mtafiti ameweka hitimisho.

**Sura ya tano; Muhtasari wa Utafiti, Hitimisho na Mapendekezo**: Vipengele vilivyojadiliwa ni pamoja na Muhtasari wa tasnifu (sura tano), Hitimisho la tasnifu, na Mapendekezo kitaaluma, kwa serekali, kwa watafiti wengine na jamii.

Kwa ujumla tunaweza kusema kwamba kulingana na mada husika ambayo inahusiana na kutathmini Kutathmini Usawiri wa Mwanamke katika riwaya ya *Mfadhili,* na kwa mujibu wa data mbalimbali alizozikusanya mtafiti katika katika uchambuzi wake, tunaweza kusema kwamba usawiri huo umechangiwa na mambo kadhaa yakiwemo , mazingira ya kazini na nyumbani, mambo ya kifamilia, mapenzi ya uongo na ya kweli, ndoa na usaliti, tamaa na fedha, uongozi na imani, migogoro n.k. Sambamba na hilo uchambuzi wa utafiti huu uliongozwa na malengo mahsusi ya utafiti. Kwa muhtasari ufafanuzi wa malengo mahsusi hayo ni kama ifuatavyo:

### 5.2.1 Lengo Mahsusi la Kwanza

Lengo mahsusi la kwanza la Utafiti huu lilikuwa ni ; Kubainisha taswira mbalimbali za mwanamke alivyochorwa katika riwaya ya *Mfadhili.* Lengo hili lililoongozwa na na swali la msingi la kwanza lisemalo: Ni taswira zipi zilizobainishwa na kuchorwa katika riwaya ya *Mfadhili*?

Katika utafiti huu mtafiti alibaini kuwa mwanamke amesawiriwa katika hali mbili hali chanya kwa upande mmoja hali na hasi kwa upande wa pili. Tukirejelea mfano wa wa hali chanya ulivyojitokeza katika riwaya hii mwanamke amesawiriwa kama Mshauri mwema, muwajibikaji kazini, rafiki wa kweli na mwenye kutimiza ahadi. Pia katika hali hii mwanamke amesawiriwa kuwa mtu mwenye mapenzi ya dhati, mwenye busara na hekima, kiongozi bora, msuluhishi na mwenye imani nk .

Kwa upande mwengine mtafiti amebaini kuwa mwanamke amesawiriwa pia katika hali hasi. Tukirejelea katika riwaya hii, mifano ambayo inaonyesha mwanamke kusawiriwa katika hali hasi ni pamoja na mwanamke kama : Mlevi, Msaliti, Mroho wa madaraka, Anayekwepa majukumu ya kazi, Anayedhalilishwa, Chombo cha starehe, Asiyetaka ushauri nk. Mtafiti baada ya tathmini hiyo anashauri kwamba ni vyema uswiri wa mambo mema ukafuatwa na usawiri wa mambo maovu ukaachwa katika jamii zetu.

### 5.2.2 Lengo Mahsusi la Pili

Lengo mahsusi la pili la utafiti huu ilikuwa ni kueleza sababu zilizomfanya mwanamke huyo asawiriwe hivyo alivyosawiriwa katika riwaya teule ya mfadhili. Lengo hilo la pili linakwenda sambamba na swali la msingi la pili lisemalo: Ni sababu zipi zilizomfanya mwanamke huyo asawiriwe hivyo alivyosawiriwa katika riwaya ya *Mfadhili*? Kwa hakika hapa baada ya mtafiti kukusanya data amebaini sababu nyingi miongoni mwa hizo ni pamoja na : Tamaa ya fedha na matamanio ya kimwili, Kujenga demokrasia na usawa kwa wote, Upendo wa dhati na huruma, kujenga mashirikiano na uhusiano mwema, Ujeuri chuki na kujionesha pamoja na Kujutia makosa aliyoyafanya.

## 5.3 Hitimisho

Kwa kuhitimishia tunaweza kusema kwamba mwanamke ni muhusika binaadamu kama walivyo binaadamu wengineo wana mapungufu yao na pia wanayo mazuri na ndio maana mtafiti akamsawiri mwanamke huyo katika hali mbili kuu hizo yaani chanya na hasi kama ambavyo nimezitaja hapo awali. Kwa udhati kabisa tathmini ya usawiri huo unaakisi maisha halisi ya

wanajamii na maendeleo yao katika jamii ya Kiafrika ikiwemo Tanzania lakini pia mtafiti amebaini kwamba mwanamke huyu anaweza kubadilika baada kushauriwa na kuenda sambamba na kushiriki katika harakati zote za kiuchumi kielimu, kisiasa na kijamii. Hali hii humfanya aendelee kuonekana ni mwenye thamani na kuhitajika.

## 5.4 Mapendekezo

Kwa udhati kabisa ni ukweli usiopingika kwamba kazi ya utafiti wa aina yoyote si kazi nyepesi. Kazi hizi zinahitaji uvumulivu mkubwa, umakini, na muda wa kutosha na hata uwezo mkubwa wa kitaaluma katika kuifanikisha. Wakati mwengine utafiti huhitaji pia gharama za fedha ili kuyafikia malengo ya utafiti huo. Utafiti huu umehusu: Kutathmini Usawiri wa Mwanamke katika riwaya ya *Mfadhili*. Kwa hakika ni imani ya mtafiti kwamba ametimiza shauku aliyokusudia kwa kuzingatia malengo na maswali ya utafiti kama yalivyopangwa. Katika utafiti ni vyema kutoa mapenekezo yafaayo. Kwa hivyo katika utafiti huu mtafiti anatoa mapendekezo yafuatayo:-

### 5.4.1 Mapendekezo ya Kitaaluma

Wanataaluma kama vile wahadhiri, walimu, watunga mitaala, wasomi na hata wanafunzi wa somo la fasihi wana nafasi kubwa ya kukuza taaluma zao kwa kuzingatia maeneo muhimu ambayo bado hayajafitiwa. Kwa mfano mtafiti ametathmini kuhusu usawiri wa mwanamke katika riwaya ya Mfadhili. Katika kazi hii mtafiti amemgusia mwandishi mmoja tu yaani Hussein Issa Tuwa mwandishi kutoka Tanzania Bara. Upo uwezekano mkubwa wa kufanyiwa

utafiti waandishi wengine kutoka Zanzibar. Pia mtafiti amejikita katika kitabu kimoja tu. Kwa hivyo upo uwezekano wa kufanya utafiti huu katika vitabu viwili na pia mtafiti amefanyia riwaya lakini upo pia uwezekano wa kufanya utanya utafiti kama huu kwa kuzingatia vitabu vya tamthilia au hata vya mashairi pia inawezekana pia kufanyia maeneo mengine kama vile fani na hata maudhui.

### 5.4.2 Mapendekezo kwa Serikali

Kwa upande mwengine Serikali nayo inayo wajibu wa kuhamasisha a kufanya tafiti za kitaaluma. Ni muhimu kufanya tafiti za taaluma ya fasihi ili kuweza kuimarisha taalima hiyo katika kukuza maendeleo ya elimu nchini Tanzania na kwengineko duniani. Juhudi hizo za makusudi zitasaidia kuamsha ari ya wanajamii kujifunza na kuweza kuisaidia serikali katika maendeleo ya taifa kwa kuongeza idadi ya wasomi (wataalamu) waliobobea katika fani mbali mbali fasihi ikiwa ni moijawapo. Kwa mnasaba wa hilo ni vyema serikali ikaandaa kifungu maalumu au bajeti maalum kwa wanataaluma na wasomi chipukizi wa Fasihi, kwa lengo la kuendelea kufanya tafiti mbalimbaliza fasihi katika utanzu wa riwaya na tanzu nyenginezo za waadishi mbalimbali duniani, bara la Afrika ikiwemo Tanzania. Hali hii itajenga ushindani wa kitaaluma ikiaminiwa kuwa tasnifu hii ni mojawapo ya marejeleo muhimu kwa wapenzi na wanataaluma wa fasihi.

### 5.4.3 Mapendekezo kwa Jamii

Jamii nayo ina dhima kubwa ya kujifunza taaluma mbalimbali ikiwemo taaluma

ya fasihi. Mtafiti anapendekeza kuwa wanajamii wawe na utamaduni wa kusoma vitabu, kwa bidii kubwa. Utamaduni huu wa kusoma vitabu utasaidia sana kuongeza maarifa na kuwafanya wanajamii hao kuweza kuteua meme na kuacha yaliyo maovu. Sambamba na hilo tabia ya usomaji wa vitabu ikiwa ni pamoja na vitabu vya fasihi kama riwaya, tamthilia na mashairi, tasnifu na makala mengineyo ya kitaaluma ikiwemo tasnifu hii ambayo itakuwa ni nyenzo muhimu katika kuinua upeo wa maarifa ya akili kwa manufaa binafsi na taifa kwa ujumla.

**5.4.4 Mapendekezo kwa Watafiti wengine**

Kwa hakika utafiti huu utakuwa ni chachu kwa watafti wengine hususan wale wanaofanya somo la fasihi . Mtafiti mejaribu kukusanya mambo mengi ya kitaaluma katika ukusanyaji wake wa data. Mtafiti anaamini kwamba data hizo pia zitaweza kuwasaidia watafiti wengine katika tafiti zao mbalimbali za kitaaluma ikizingatiwa kwamba kuna uwiano mkubwa katika tanzu za fasihi ikiwemo riwaya, tamthilia na hata mashairi. Pia usawiri wa mwanamke katika Nyanja mbalimbali katika riwaya ya *Mfadhili* itasaidia kuwa kama marejeleo kwa watafiti ambao watapenda kuchukuwa uwanja wa fasihi katika kurejelea hizo tanzu nilizozitaja hapo awali. Mtafiti anaamini kwamba pamoja na kwamba yeye amejikita kwa mwandishi mmoja tu lakini utafiti huu unaweza kutumika kwa watafiti wengine wanaofanya utafiti kama huu kwa waandishi wengine zaidi ya hayo utafiti huu pia unaweza kuwasidia wanafunzi wengine wa sekondari katika kufanya marejeleo yao ya kifasihi. Mtafiti anapendekeza kwamba watu wengine wafanye tafiti mbalimbali kuangalia usawiri wa wahusika wa

aina mbalimbali. Utafiti huu ni vyema ufanywe kwa kutumia vitabu vya waandishi mbalimbali.

## MAREJELEO

Adam, J. na Kamuzora, F (2008). *ResearchMethods for Business and Social Studies,* Morogoro: Mzumbe Book Project.

Babbie, E (1999). *The Basic of Social Research.* Belmont: Wadsworth Publishing Company. .

Bakari, K. (2007). *Kiswahili Cha Asili Cha Kina Mama Wa Visiwani Zanzibar*

Baraza la Kiswahili la Zanzibar –BAKIZA (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha,* Nairobi: Oxford University Press.

Buliba, A na wenzake, (2014). *Misingi ya Nadharia na Utafiti,* Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Limited

Caleb, C. W. (2013). *"Taswira ya mwanamke katika tamthiliya ya Nguzo mama na Mma Ee".* Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Enon, J. C. (1998). *Educational Research Statistics anda Measurement.* Kampala: Makerere University Press.

Githuci, M.G (2013) *Ujagina wa mwanamke katika Pango.* Tasnifu ya uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)

Hornby, A. S. (2005). *Oxford Advanced Learner's Dictionary*, 7th ed. Oxford: Oxford University Press.

Kothari, C. K. (2008). *Research Methodology, Method and Techniques*. New Delhi: New Delhi Wiley Eastern Limited.

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques,* New Delhi: New Age International (P) Limited Publishers.

Madumullah, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili, Historia na Misingi ya Uchambuzi*, Nairobi: Sitima Printers and Stationary.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: EAE P Ltd.

Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Ndungo, C. W. na Mwai, W. (1991). *Kiswahili Studies Part Two*: *Misingi ya Nadharia ya Fasihi ya Kiswahili*. Nairobi: University of Nairobi.

Njogu, K. na Chimerah, R; (1999). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation Ltd.

Njogu, K. na Wafula, R. M. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: The Jomo Kenyata Foundation.

Ntaragwi, M. (2004). *Uhakiki wa kazi za fasihi,* Augustana College: Rock Island.

Sengo, T. S. Y. (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi.* Dar es Salaam: AERA.

Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi.* Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Shafi, A. S (1999). *Vuta N'kuvute.* Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Strobel, M. (1979) *Muslim Women in Mombasa.* New Haven and London: Yale University Press.

Tuwa, H. I. (2007) *Mfadhili*. Dar es Salaam: Macmillan Aidan Ltd.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa.

Yin, R. K. (1994). *Case Study Research: Design ad Methods*, (2n eds) Thousands Oaks Calif: SAGE publishers.